

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao cha Kwanza- Tarehe 28 Januari, 2020

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa mamlaka niliyonayo chini ya Kanuni ya 5(1) na kama ilivyokubaliwa na Kamati ya Uongozi tarehe 23 Januari, 2020 kuanzia sasa hapa Bungeni Wimbo wa Taifa utapigwa na kuimbwa sambamba na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na uimbaji huo utaongozwa na kwaya ya Bunge. Wimbo wa Taifa.

WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI ZILIIMBWA NA KWAYA YA BUNGE

SPIKA: Naomba tukae, samahani kidogo.

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kabla kwaya hawajaondoka, naomba Waheshimiwa Wabunge tuwapigie makofi. *(Makofi)*

Ahsanteni sana sana ni mwanzo nzuri tunaamini huku mbele kwaya yetu itafika mahali ambapo hata katika shughuli za Kitaifa itakuwa ni moja ya kwaya ambazo zinaweza zikashiriki kuweza kutuimbua. Tunawapongeza sana sana, nimefurahi mno na tunawashukuru Jeshi la Polisi kwa kutoa Mwalimu aliyewafundisha namna ya kuimba, naamini wataendelea kuboreka na Waheshimiwa Wabunge kwaya hii ni yetu, wakati mwingine pia tutajunga nayo. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Katibu!

NDG.STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WABUNGE:

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge katika Mkutano wa 17 wa Bunge, Bunge hili lilipitisha Muswada mmoja wa Sheria ya Serikali ufuatao:-

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 7 wa mwaka 2019 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.7) Bill, 2019)*. Kwa taarifa hii napenda kuliarifu Bunge kwamba tayari Muswada huo mmoja umepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa sheria ya nchi inayoitwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria

Mbalimbali (Na. 7), Sheria Na. 14 ya mwaka 2019 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.7) Act No. 14 of 2019*).

Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 8) wa mwaka 2019 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.8) Bill, 2019*).

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 8) wa mwaka 2019 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.8) Bill, 2019*).

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA – K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 8) kwa mwaka 2019 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.8) Bill, 2019*).

SPIKA: Ahsante. Sasa kabla hatujaendelea na shughuli inayofuata naomba niwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameniandikia na kupitia kwangu kuja kwenu kama ifuatavyo, nawasomea kama ilivyo:-

“Kwa furaha na unyenyekevu mkubwa nimelipokea Azimio Namba 18 la mwaka 2019, Mheshimiwa Rais amelipokea lililotolewa na Bunge tukufu katika Mkutano wa 17, Kikao cha Tisa - tarehe 15 Novemba, 2019 hapa Dodoma. Kupitia kikao hicho Bunge lilitoa azimio la pongezi kwa Mheshimiwa Rais binafsi na kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwa utendaji mzuri katika kipindi cha miaka minne iliyopita. (*Makofi*)

Azimio hilo limebainisha maeneo mbalimbali ya mafanikio katika utekelezaji wa shughuli za Serikali na kuleta mageuzi ya kijamii na kiuchumi nchini. Bila shaka azimio hilo limetolewa baada ya utathmini wa kina wa utendaji wa Serikali. (*Makofi*)

Hivyo Mheshimiwa Rais anasema anatumia fursa hii kulishukuru Bunge Tukufu kwa kutathmini na kutambua jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano katika kuleta mageuzi nchini pamoja na mchango wake binafsi katika dhamana kubwa na Bunge kutambua mchango wake binafsi Mheshimiwa Rais na dhamana kubwa na adhimu aliyopewa na Watanzania katika kuliongoza Taifa letu. (*Makofi*)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Lakini wakati akitoa shughuli zake kwetu za dhati kwa Bunge hili anatambua kuwa mafanikio haya makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne ni matokeo ya jitihada za pamoja na mashirikiano ya mihimili yote mitatu ya Serikali na hususan Bunge tukufu ambalo ndilo limekuwa likijadili na kupitisha bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa mipango, mikakati na miradi mbalimbali ya Serikali. Zaidi ya hayo Mheshimiwa Rais anatambua mchango mkubwa uliotolewa na Watanzania wote katika kuelewa na kuunga mkono mwelekeo na jitihada za Serikali yao. (Makofi)

Hivyo basi, Mheshimiwa Rais anatumpeleza sisi wote pamoja na Mheshimiwa Spika na Bunge lote kwa ujumla katika utekelezaji mwema wa dhima yetu kuu ya kuisimamia Serikali. Rai ya Mheshimiwa Rais kwa Spika na kwa Bunge ni kwamba tuendelee kushirikiana ili kujenga Taifa letu katika misingi ya amani, umoja na mshikamano ili hatimaye tuufikie ukombozi wa kweli kiuchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Rais anahitimisha kwa kurejea tena shukrani zake za dhati na kuniomba mimi nizifikishe salamu hizi kwenu Waheshimiwa Wabunge. Kwa pamoja tunajenga Taifa letu." Mwisho wa kunukuu. (Makofi)

Ahsanteni sana kwa kuzipokea salamu hizo. Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali, swali la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI linaulizwa na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mbunge wa Mtera. Mheshimiwa Lusinde, tafadhali.

Na. 1

Barabara ya *Mvumi Mission* Kuwekewa Lami

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya *Mvumi Mission* itajengwa kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu sana na ni malalamiko ya wananchi wa Mkoa wa Dodoma nzima kwamba barabara ya kwenda Hospitali ya *Mvumi Mission* iwekwe lami. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mbunge wa Mtera kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Barabara wa mwaka wa fedha 2019/2020 imetenga kiasi cha shilingi milioni 375 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya *Mvumi Mission* kwa kipande chenye urefu wa kilometa moja kwa kiwango cha lami. Maandalizi ya ujenzi yameshaanza na ujenzi unatarajia kukamika ifikapo mwezi Agosti, 2020.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja katika Jimbo la Mtera kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Lusinde, kwa mwendo wa kilometa moja sijui itafika mwaka gani? Swali la nyongeza Mheshimiwa Lusinde.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri katika jibu lake amesema ujenzi umeshaanza. Je, yuko tayari kuongozana na mimi kesho ili akaone ujenzi kama umeanza au watu wake wamemdanganya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kutokana na kunyesha kwa mvua barabara nyingi siyo tu zimeharibika bali zimeoza na hii imepelekea wazazi kupata shida kufika hospitali hasa kwa barabara ya Huzi kuja Manda ambapo ukitoka Manda kuja Huzi kuja kwenye Kituo cha Afya cha Mpayungu, lakini *Mvumi Mission* hakuingiliki pande zote, madaraja yamezingirwa na maji na yamevunjika.

Mheshimiwa Naibu Waziri anatuambiaje kuhusu kutengeneza kwa haraka ili kunusuru maisha ya akinamama na watoto na wagonjwa akinababa ili waweze kufika hospitali? Ahsante sana.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lusinde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jibu langu la msingi nimesema kwamba maandalizi ya ujenzi wa barabara umeshaanza si kwamba barabara umeanza, maandalizi yamekwishaanza. Kama tumeshaanza niko tayari nipo tayari kuongozana naye kwenda kuangalia hatua ambayo imekwishafikiwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ambalo kimsingi ni swali ambalo linahusu Wabunge wote humu ndani kwamba baada ya mvua ambazo kimsingi zimeanza na zinaendelea sana barabara nyingi zimeharibika, Mheshimiwa Waziri wa Nchi ameshaagiza Meneja wa *TARURA* wa Tanzania na Mameneja wa Mikoa na Wilaya wafanye tathmini na walete bajeti ili tufanye utengenezaji wa haraka katika maeneo mbalimbali ili huduma muhimu ziweze kufanyika.

Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kuwaelekeza pia, Meneja wa *TARURA* wa Mikoa na Wilaya kwamba kazi ambayo wamepewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi waifanye haraka sana na kuchukukua hatua ya dharura ili kuhakikisha kwamba huduma za afya zinaendelea, vijana wanaenda shule na watumishi wa Serikali na watumishi wengine wanafanya shughuli zao za maendeleo. Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Nape Nnauye, swali la nyongeza.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mtama, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake wa kuamua kutupa watu wa Mtama Halmashauri yetu. Sasa je, Serikali iko tayari kumuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga barabara za Mji wa Mtama na kuzikarabati zile ambazo zimeharibiwa na mvua ili Mji wa Mtama sasa uwe na hadhi ya kubeba Halmashauri hii ambayo Mheshimiwa Rais ametupa? (Makofi)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nape, Mbunge wa Mtama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Nape na Halmashauri zingine zote kwamba Serikali ipo tayari kutenga fedha za kutosha kujenga barabara katika Makao Makuu ya Halmashauri mpya na zile za zamani, pia na kujenga majengo muhimu katika maeneo hayo ili huduma ziweze kutolewa kwa uhakika zaidi. Ahsante.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na swali la pili la siku ya leo, litaulizwa na Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, uliza swali lako tafadhali.

Na. 2

Msongamano wa Wanafunzi Shule ya Msingi Vikindu

MHE. RUTH H. MOLLEL aliuliza:-

Shule ya Msingi Vikindu katika Wilaya ya Mkuranga ina mikondo miwili (A na B) darasa la kwanza hadi la saba na mwaka 2019 darasa la kwanza na la pili yalikuwa na wanafunzi 300 kila darasa.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha uwiano wa mwalimu na mwanafunzi wa 1:45 unazingatiwa kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya Msingi?

(b) Je, kwa msongamano huo tunaweza kupata wanafunzi walioelimika na kukidhi malengo ya Tanzania ya viwanda?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, Mbunge wa Viti maalum kama ifuatavyo swali lake ambalo lina sehemu (a) na (b):-

(a) Mheshimiwa Spika, ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi katika Halmashauri ya Mkuranga limetokana na juhudi za Serikali za kuhamasisha wananchi kuandikisha wanafunzi shuleni kupitia mpango wa elimu msingi bila malipo. Ili kukabiliana na msongamano wa wanafunzi katika Shule za Msingi Vikindu, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kujenga Kituo Shikizi cha Juhudi, Kitwangi, Mitawa na Muungano. Kituo Shikizi cha Muungano kilichopo katika Kijiji cha Vikindu kinatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2020 na kitakuwa na uwezo wa

kupokea wanafunzi 300. Mkakati mwingine ni wanafunzi kusoma kwa kupokezana yaani *double section* ambapo kuna madarasa ya asubuhi na ya mchana.

(b) Mheshimiwa Spika, kama ilivyoenezwa kwenye sehemu (a) hatua mbalimbali zimechukuliwa na zinaendelea kuchukuliwa na Serikali ili kuhakikisha msongamano wa wanafunzi madarasani unapungua na kuwezesha kupata elimu bora. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Ruth Mollel swali la nyongeza tafadhali.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Shule Shikizi ya Muungano ilijengwa na nguvu za wananchi kwa muda mrefu na mpaka leo tunaambiwa kwamba hiyo shule itakamilika Februari. Je, Serikali haina takwimu za wanafunzi wanaomaliza kusudi hii miundombinu ianze kutengenezwa mapema ili wanafunzi waweze kwenda kwenye shule zao?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; je, umeme ni lini utaunganishwa katika hiyo shule? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo ya nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, swali la kwanza angependa kujua kama Serikali ina takwimu; naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina takwimu za idadi ya wanafunzi ambao wapo katika maeneo yetu mablimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika eneo hili, Jimbo la Mkuranga kwa Mheshimiwa Abdallah Ulega pamoja na Mheshimiwa Mbunge na wengine wamefanyakazi kubwa sana ya kusaidia na kuchangia kupitia Mfuko wa Jimbo, wadau mbalimbali na Mbunge mwenzake wa Viti Maalum katika Mkoa ule wamefanyakazi kubwa sana ya ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshafanya tathmini, tunajua ni kweli kwa mwaka huu wanafunzi baadhi walibaki kwa muda mrefu nyumbani baada ya kuwa na upungufu wa miundombinu, lakini tulivyofanya tathmini sasa hivi tumekubaliana, tumefanya *projection* kwamba hii changamoto ya miundombinu itakwenda kupungua, lakini tushirikiane, Serikali, Wabunge, wadau mbalimbali ili tuweze kuboresha miundombinu yetu hii. Ni matarajio yetu ni kwamba hii hali ya kuwa na uongufu itaendelea kupungua kadri muda utakavyokuwa unakwenda.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili, ametaka kujua kama ni lini umeme utaunganishwa katika shule hii; naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la umeme ni suala ambalo sisi wote tushirikishane pale kwa sababu hii ni sehemu ya umma tunatoa huduma. Lakini kwamba tutaweza kuweka miundombinu katika shule zote haiwezekani kwa maana ya Serikali sisi wenyewe. Mheshimiwa Mbunge ni mdau muhimu na wadau wengine wote tushirikiane tuone, tujue ni kiasi gani kinaweza kikasaidia shule hii kupata umeme ili tuweke katika eneo hilo. Ahsante.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Elimu, Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, suala hili la upungufu wa madarasa limekuwa likijirudia mara kwa mara na Waziri anasema wana takwimu. Mwaka juzi wanafunzi 133,000 walifaulu lakini wakashindwa kuchanguliwa kwa sababu ya madarasa, lakini mwaka huu tena zaidi ya wanafunzi 58,000 wamefaulu darasa la saba lakini wamekosa madarasa.

Mheshimiwa Spika, swali langu, ni kwa sababu gani Serikali kama ina *projection* na inajua ni wanafunzi wangapi wanaweza kufaulu na wako darasa la saba, ni kwa sababu gani hawana mpango mahususi kuhakikisha kwamba kila mwaka wanatenga fedha kwa ajili ya madarasa ili angalau kwa miaka mitano tuhakikishe kwamba tatizo hili sugu limekwisha na wanafunzi wetu wanapomaliza darasa la saba wanakwenda shuleni kama wengine. Kwa sababu tunavyozungumza leo kuna Wanafunzi Dar es Salaam na Mikoa mingine wamefaulu darasa la saba lakini watakwenda kuanza mwezi wa tano, haoni kwamba hili ni tatizo? Ahsante sana.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI tafadhali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru dada yangu Mheshimiwa Susan Lyimo kwa sababu amekuwa na mchango mkubwa sana katika elimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya kila liwezekanalo na kwa mfano, mwaka huu tulikuwa na wanafunzi takribani 759,000 waliofaulu na hii inaonekana kutokana na juhudi kubwa ndiyo maana mwaka huu ufaulu umepanda kwa wastani wa asilimia 3.7 ambayo ni mafanikio makubwa sana yaliyowahi kutokea.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana licha ya ufaulu huo ulikuwa mkubwa lakini zaidi ya asilimia 92 na wanafunzi wote tuliowachangua katika awamu ya kwanza tulibakisha wanafunzi 58,000 ambao hata hivyo wanafunzi wote hivi sasa tumeshawachangua na hivi sasa kuna shughuli kubwa sana ya umaliziaji baadhi ya madarasa 1,080 ambayo naomba niwahakikishe Watanzania kwamba ukiona juhudi wanafunzi wanafaulu ni *impact* kubwa ya Serikali ya uwekezaji iliyosababisha mpaka wanafunzi waweze kufaulu zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tushikamane kwa pamoja kuona ufaulu mkubwa kwetu sisi iwe ni mafanikio makubwa kwamba Tanzania inasonga mbele katika suala zima la kuhakikisha kila Mtanzania anapata elimu. Ahsante.

SPIKA: Swali linalofuata Mheshimiwa Yahaya Omar Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, uliza swali lako Mheshimiwa Massare.

Na. 3

Barabara Inayopita Katikati ya Mji wa Itigi

MHE. YAHAYA O. MASSARE aliuliza:-

Ipo ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kilometa nane oinayopita katikati ya Mji wa Itigi.

Je, ni lini sasa barabara hii itaanza kujengwa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Waitara tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kukamilisha usanifu wa barabara inayopita katikati ya Mji wa Itigi yenye urefu wa takribani kilometa nane. Usanifu huo umefanywa kama sehemu ya usanifu wa barabara ya Mkiwa - Itigi - Rungwa - Makongolosi yenye urefu wa kilometa 413 uliosimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania yaani *TANROADS*. Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara inayopita katikati ya Mji wa Itigi kwa kiwango cha lami itakayojengwa chini ya mradi wa ujenzi Mkiwa -Itigi - Rungwa - Makongolosi ili kufungua fursa za kiuchumi na kijamii katika maeneo hayo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Massare swali la nyongeza nimekuona.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Serikali ambayo kidogo yana ukakasi, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya Mkiwa - Rungwa hadi Makongolosi imekuwa ikitengewa pesa kwa muda mrefu toka nimeingia katika Bunge hili na hata Mheshimiwa Rais aliwahi kusimama katika mkutano wa hadhara akiwaambia wananchi wa Itigi kwamba sasa inajengwa na mkandarasi alipatikana lakini hatujui kilichotokea.

Sasa je, Serikali hususani Wizara hii ambayo inayohusika na barabara hii ambayo inahusika na *TANROADS*, Wizara ya Ujenzi, wako tayari sasa kusema mbele ya Bunge lako tukufu ni lini wataanza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kilometa 56.9 ambazo zimetajwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, barabara hii inapita katikati ya Mji wa Itigi, mji wa kibiashara na wananchi wanajishughulisha katika kuhangaika kutafuta maisha yao vizuri, barabara hii sasa imegeuka mto inapitisha maji. Je, ni lini Serikali itafanya haraka kukarabati barabara hii kwa dharura?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, tumemsikia Mheshimiwa Mbunge na kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba tumeshafanya usanifu na tutawasiliana na wenzetu wa *TANROADS* tuangalie namna bora ya haraka zaidi kuweza kurekebisha hali hii katika Jimbo lake. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama sasa anavyozungumza Mji wa Itigi unapitisha maji; naomba nimuagize Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Singida na Wilaya hii afanye tathmini ili alete maombi tuone hatua ya haraka zaidi ya kuweza kurekebisha hali hii ili maji yasiweze kupita katika eneo hili na huduma ziweze kuendelea. Ahsante.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa James Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, ahsante, nilitaka kujua; kwa kuwa gharama ya kutumia *asphalt* yaani kujenga lami kama zinavyoonekana ni ya ghali na kwa kuwa ahadi za Mheshimiwa Rais ikiwemo barabara za Himo Mjini, Kahe na ya kwenda Kilema kwenye maeneo ya mwinuko zinahitajika zijengwe ili zipitike wakati wote. Nataka kujua, Serikali imefikia wapi kupitia wataalam kuja na teknolojia nyingine ya kutumia *calcium oxide* na *moram* ambayo ni rahisi kuliko hii ya *asphalt* ili ziweze zikatumike kwenye barabara zote nchi nzima na barabara zote ziweze kupitika kwa sababu ziko kwenye hali mbaya sana?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI majibu tafadhali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kijibu swali la kaka yangu James Mbatia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli gharama ya kutumia *asphalt* ni kubwa lakini mara nyingi sana mahitaji ya barabara aina gani ya teknolojia ijengwe ni kutokana na jinsi gani ya ile barabara mahitaji yake yalivyo. Ndiyo maana ukiangalia katika ofisi yetu sasa hivi kuna barabara tunazijengwa kwa *double surface dressing* na hizi *cost* yake unaona kwamba inarange katika ya shilingi milioni 300 mpaka milioni 500 lakini barabara ya *asphalt* inakwenda mpaka *one billion per kilometer*.

Sasa unakuja kuona ukiangalia hizi barabara ambazo sasa hivi tunazijenga katika miji mbalimbali tunatumia *asphalt* kwa sababu mizigo inayopita huko na kwa sababu tunalenga katika ajenda ya kiuchumi lazima tutengeneze barabara ambazo zitaweza kupitisha magari mazito kuhakikisha tunachochea uchumi wa eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ushauri uliozungumza katika kitengo chetu cha ofisi yetu kuna watu wanafanya *research* maalum kwa aina mbalimbali ya barabara ya madaraja na ndiyo maana hata ukienda kule Kigoma tumeamua sasa hivi kuna teknolojia nyingine tumetoa Belgium ya ujenzi wa madaraja, kwa hiyo hiyo yote ni juhudi ya Serikali kuangalia nini tufanye katika maeneo gani, lengo kubwa ni kuhakikisha Wananchi wote waweze kufika.

Kwa hiyo, ushauri wako unachukiliwa lakini naamini kwamba Serikali inafanya juhudi kubwa kuhakikisha Wananchi wanapata huduma nzuri ya barabara. Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Kabla hatujavuka TAMISEMI niseme tu kwamba ni kweli mvua inanyesha karibu kila mahali nchi nzima, lakini kwa taarifa tulizonazo hivi sasa ni kwamba katika Mkoa wa Lindi katika Jimbo la Mheshimiwa Waziri Mkuu kule Ruangwa kuna mafuriko na kwa hiyo tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwa hali hiyo muweze kuiona, lakini pia Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa upande wa maafa pia waweze kuangalia hali hiyo.

Ahsante, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali la Mheshimiwa Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, uliza swali lako tafadhali.

Na. 4

Malimbikizo ya Madeni kwa Wazabuni

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA aliuliza:-

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu ya malimbikizo ya madeni mbalimbali ya wazabuni wanaotoa huduma mbalimbali ikiwepo huduma ya kupeleka chakula kwa wanafunzi magerezani na matengenezo ya magari.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kulipa madeni hayo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Naibu Waziri Engineer Masauni.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika nyakati tofauti imekuwa na mkakati wa kulipa madeni yake ya ndani ikiwemo madeni ya watoa huduma, chakula cha wafungwa na matengenezo ya magari katika magereza yote nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 hadi mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya kiasi cha fedha shilingi 23,563,630,710.61 zimelipwa kwa ajili ya watoa huduma za uendeshaji, chakula cha wafungwa na matengenezo ya magari yakiwa ni madeni ya mwaka wa fedha 2014/2015 hadi 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, madeni ya mwaka 2012/2013 mpaka mwaka 2013/2014 na 2017/2018 tayari yameshahakikiwa, kinachosubiriwa ni fedha kutoka Hazina kwa ajili ya kulipa. Hata hivyo, madeni ya mwaka wa fedha 2018/2019 tayari yameandaliwa yanasubiri uhakiki kutoka Hazina ili kuhakiki madeni hayo na baadaye kuyalipa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kulipa madeni ya wazabuni wanaotoa huduma mbalimbali ikiwemo chakula cha wafungwa na matengenezo ya magari kadri ya fedha itakavyopatikana.

SPIKA: Mheshimiwa Mwakasaka nimekuona.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwa kuwa madeni haya ni ya muda mrefu na imetokea mara nyingi Serikali imekuwa ikilipa madeni yaliyokuja baadaye wanaacha yale ya nyuma. Sijui ni vigezo gani vinatumika kuacha madeni yale ya muda mrefu na kulipa yale ambayo yamekuja baadaye?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wazabuni wengi wanaodai magereza kwa maana wale wanaofanya zabuni ya chakula wengi sasa wana hatari ya kuuziwa nyumba zao hasa wale ambao wamekopa katika taasisi mbalimbali za fedha. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha hawa wazabuni mbalimbali inawakomboa wasiweze kuuziwa nyumba zao na taasisi za kifedha?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Engineer Masauni majibu tafadhali kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, madeni ambayo yanalipwa ni miongoni mwa madeni ambayo tumeshalipa kama ambavyo nimeeleza katika jibu la msingi pia yako madeni ya zamani na nilieleza kwamba madeni mengine ambayo hayajalipwa ni kutokana na kwamba mengine yameshahakikiwa na hivyo basi pale fedha ambapo zitapatikana yatalipwa. Naamini kabisa yatakapokuwa yamekamilika madeni hayo kulipwa kama ambavyo nia ya Serikali ilivyo basi yale matatizo ambayo yanakabiliwa na hawa wazabuni yataweza kupatiwa ufumbuzi. Ni dhamira ya Serikali kuhakikisha madeni haya yanalipwa ili kuepusha usumbufu wowote kwa wazabuni wetu.

SPIKA: Ahsante sana. Tuchukue kwanza mzoefu wa mambo ya magereza sijui nani hapa! Mheshimiwa Esther Matiko. *(Kicheko)*

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ni dhahiri kwamba Serikali imekuwa haitoi kipaumbele kwenye huduma muhimu za binadamu badala yake wamekuwa wakiwekeza zaidi kwenye vitu.

Mheshimiwa Spika, magereza ni moja ya sehemu ambazo inatakiwa wapewe vipaumbele na wapewe huduma stahiki kama inavyoelekeza. Wazabuni wengi wanadai na wameacha kutoa huduma za vyakula na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha zaidi nilitaka nijue, Serikali ni lini itatoa nguo kwa wafungwa ambao mnasema kabisa wakishafungwa wavae yale mavazi. Niliona hiyo nikiwa Segerea, lakini juzi nilivyotembelea Gereza la Tarime pamoja na matatizo mengi ambayo yametokana na kutokulipa madeni ya wazabuni na kuweza kutoa vifaa hivi unakuta mpaka Askari Magereza anachukua nguo zake anavisha mfungwa kama anavyotoka nje.

Ni lini sasa Serikali itaondoa hii fedheha ihakikishe kwamba wafungwa ambao wanastahili kuvaa nguo waweze kupewa zile nguo ambazo wataweza kujihifadhi? Na wajue kabisa kwamba waliopo Serikalini leo magereza ni yao kesho. *(Kicheko)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Engineer Masauni tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimsahihishe siyo sahihi kwamba Serikali haitoi kipaumbele kwenye huduma mbalimbali ikiwemo za wafungwa. Nimhakikishie kwamba wafungwa hawa tumekuwa tukiwapatia *uniform* na siyo wote kama ambavyo umetaka ieleweke kwamba hawana *uniform*, lakini changamoto hii itaendelea kupungua hatua kwa hatua. Hata hivyo, sehemu kubwa ya wafungwa tayari wameshaanza kupatiwa nguo kwenye magereza.

SPIKA: Mheshimiwa Goodluck Mlinga nilikuona kule nyuma mwisho kabisa.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, naomba niwakumbushe kuwa tarehe 24 Januari, 2020 Serikali imesaini makubaliano ya kuchukua asilimia 16 kutoka *Barrick Gold Tanzania*, kwa hiyo sasa hivi Serikali ina 16%, maana yake watu wengi hawajaisikia hiyo, kwa hiyo inabidi tuongeze sauti. *(Makofi)*

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Gereza la Ulanga mwaka wa tano sasa hivi mahabusu wanapelekwa mahakamani kwa kutumia bodaboda. Hii ni hatari sana kwa mahabusu kutoroka. Naomba kuuliza swali la nyongeza, je, ni lini Serikali itapeleka gari la mahabusu Gereza la Ulanga? (Makofi/ Kicheko)

SPIKA: Duh hii mpya, mahabusu wanapelekwa mahakamani kwa bodaboda! Mheshimiwa Naibu Waziri mambo haya yapo? Majibu ya swali hilo tafadhali. (Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mlinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mlinga kwa jinsi ambavyo anaweza kujenga hoja zake kwa msisitizo, sisemi kwamba anatia chumvi, lakini anajenga hoja kwa msisitizo na anatumkumbusha mambo muhimu kama ambavyo ametukumbusha hili suala la mafanikio kwenye sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mlinga kwamba najua anapozungumza bodaboda alitaka tu kiongeza uzito wa hoja yake, lakini tunatambua juu ya changamoto ya usafiri katika baadhi ya magereza yetu nchini na nimhakikishie pale ambapo gari mpya zitakapopatikana, tutampeleka katika gereza hilo la Jimboni kwa Mheshimiwa Mlinga ili kukabiliana na changamoto hiyo ya usafiri.

SPIKA: Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji uliza swali lako.

Na. 5

Hitaji la Benki Wilayani Rufiji

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA aliuliza:-

Wilaya ya Rufiji ni moja ya Wilaya kongwe nchini na inakadiriwa kuwa na watu takribani 350,000; eneo la Wilaya ni kubwa na huwalazimu wananchi kusafiri umbali wa kilometa 100 kufuata huduma za kibenki.

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma za kibenki katika Wilaya ya Rufiji?

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mchengerwa, watu wa Rufiji duniani ni pamoja na watu wanaoishi katika Kisiwa cha Fiji.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Kabisa.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango tafadhali majibu ya swali hilo la Warufiji wote, Dkt. Ashatu Kijaji.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa upatikanaji wa huduma za kifedha na hasa karibu na maeneo ya wananchi ili kuwawezesha kuendesha shughuli zao za kiuchumi. Aidha, kufuatia mabadiliko ya sekta ya fedha nchini ya mwaka 1991 Serikali ilitoa uhuru kwa mabanki kufanya tathimini na utafiti ili kuamua kuhusu maeneo ya kupeleka huduma za kibenki

kulingana na taarifa za utafiti uliofanywa pamoja na vigezo vya benki husika. Kwa kuwa benki zinajiendesha kibiashara maamuzi ya kufungua tawi sehemu yoyote hapa nchini huzingatia vigezo hivyo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Wilaya ya Rufiji wanapata huduma za kifedha kupitia kituo cha makusanyo ya fedha cha NMB yaani *cash collection point* kilichopo Kata ya Utete pamoja na mawakala wa benki hususan Benki ya NMB na CRDB waliopo katika Wilaya ya Rufiji.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge wa Rufiji aendelee kuwahimiza wananchi wake kutumia fursa zilizopo za kupata huduma za kifedha kupitia kituo hicho cha makusanyo ya fedha cha NMB, mawakala wa benki na simu za mkononi wakati Serikali ikiendelea kufanya jitihada za kuboresha miundombinu muhimu pamoja na kufanya majadiliano na kuyashawishi baadhi ya mabanki ili kuona jinsi ya kupunguza baadhi ya vikwazo vinavyoweza kusababisha gharama za uendeshaji wa shughuli za kibanki katika Wilaya ya Rufiji kuwa juu.

SPIKA: Mheshimiwa Mchengerwa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rufiji ni Wilaya kongwe sana iliyozaa zaidi ya Wilaya tano lakini pia imezaa Taifa la Fiji kama ambavyo wewe mwenyewe unafahamu. Lakini pia eneo la Rufiji, Kibiti na Kilwa hakuna benki yoyote ya biashara na Serikali sasa inapeleka zaidi ya trilioni saba za ujenzi wa uzalishaji wa umeme katika Bwala la Mto Rufiji ambapo tunategemea kuwepo kwa watumishi, wafanyakazi zaidi ya 6,000 mpaka 7,000.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa kwamba tawi la benki katika Wilaya yetu ya Rufiji haliepukiki? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, eneo la Rufiji lina ukubwa wa zaidi ya hekari 500,000 ambao lipo ndani ya Bonde la Mto Rufiji, lakini pia kwa kuwa Serikali inatekeleza Mradi wa Umeme wa Rufiji, Serikali pamoja na Wilaya ya Rufiji imetenga zaidi ya hekari 150,000 kwa ajili ya kwenye kilimo cha kisasa cha umwagiliaji.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa kwamba Benki ya Maendeleo ya Kilimo ni muhimu sasa kuwepo Rufiji ili kuweza kuwasaidia wananchi wa Rufiji kuchangamkia fursa za maendeleo, fursa za kilimo, fursa za biashara katika Mradi wetu wa Umeme wa Rufiji? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza kuhusu kwamba Serikali haioni kwamba haiepukiki sasa kufungua tawi Rufiji, kama nilivyosema benki nyingi zinaandeshwa kibiashara na benki nyingi huwa zinaangalia *commercial viability* ya eneo husika kabla hawajaweza kupeleka tawi la benki husika kwenye eneo husika. Kwa hiyo, kama ambavyo nimesema kwenye jibu la msingi, mabanki yetu yanafanya utafiti huo na tathmini kujiridhisha na nini kinatakiwa kufanyika kwenye maeneo husika. Hata hivyo, nimwambie Mheshimiwa Mchengerwa kwamba baada ya swali lake hili kama Serikali tumeanza kuifanyia kazi na tumeongea na Mkurugenzi wa TPB PLC na Mkurugenzi ameomba yafanyike yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza anaomba apate maombi mahsusi ili kuweza sasa kutuma timu yake kwenda kufanya kufanya *feasibility study* na kujiridhisha na *commercial viability* ya eneo la Rufiji ili kwenda kufungua tawi la Benki ya TPB kutokana na *potentials* zote kama zilivyoelezwa na Mheshimiwa Mchengerwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili kuhusu Benki ya Kilimo, kama alivyosema yeye mwenyewe Benki ya Kilimo ni benki ya maendeleo, hivyo lazima kila inapokwenda kufunguliwa ielewe kabisa wanakwenda kuhudumia aina gani ya wananchi ambao wako kwenye miradi mikubwa ya kimaendeleo. Pia Rufiji hawako mbali sana na Dar es Salaam ambako Benki yetu ya Kilimo ya Maendeleo ndipo Makao Makuu yake yalipo ambapo inahudumia maeneo yote ya Pwani, maeneo ya Morogoro. Kwa hiyo, niwaombe sana wakulima wetu wakubwa ambao wanahitaji mikopo ya maendeleo wafike Dar es Salaam na watahudumia na Benki yetu ya Kilimo ya Maendeleo. (Makofi)

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Dkt. Kafumu, swali fupi la nyongeza.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Wilaya ya Igunga kwa kupindi cha miaka mitano sasa shughuli zake za uchumi zimeongezeka sana, watu wanalima, watu wanafuga na kuna fedha nyingi mzunguko ni mkubwa, lakini tatizo ni kwamba tuna benki moja tu Benki ya NMB. Benki ya CRDB walikuja wakafanya *evaluation* wakaona *economic viability* pale ni nzuri na wakaja wakatembea, lakini mpaka sasa hivi hawajaanzisha benki. Naomba Serikali, ni wakati sasa kama wanaweza kutusaidia kuiambia Benki ya CRDB wafungue tawi pale Igunga. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha kwa kufupi, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Peter Dalaly Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimepokea taarifa yake ya kwamba Benki ya CRDB ilifika na kufanya *economic analysis* na *commercial viability* ya Wilaya yetu ya Igunga, na mimi nimepokea maombi yake, nitawasiliana na Mkurugenzi Mkuu wa CRDB kuhusu kujua utafiti huo umefika wapi na nini maamuzi yao, kama inaonekana kuna *commercial viability* nina uhakika mkubwa kwa sababu CRDB ni moja ya benki inayowafikia wananchi, watafika Igunga.

SPIKA: Mheshimiwa Rhoda, nimekuona.

MHE. RHODA E. KUMCHELA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na changamoto za kukosa huduma za kibenki katika Mkoa wa Katavi, Wilaya ya Mlele pamoja na Wilaya ya Tanganyika ni moja ya Wilaya ambazo zinakosa huduma za kibenki na ukizingatia asilimia 80 ya wakulima walioko kule wanafanya biashara kubwa na wana pesa nyingi wanasafirisha kwa njia ya magari. Sasa usalama wa fedha zao kutoka katika Wilaya hizi wanatembea zaidi ya kilometa 60 mpaka katika Wilaya ya Mpanda.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha tunapata matawi ya kibenki ili wakulima hawa waweze kusafirisha fedha zao katika mazingira yaliyo salama? (Makofi)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Rhoda Kunchela, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, inashangaza kidogo kusema wananchi bado wanasafirisha pesa kwa magari wakati Serikali imefungua na imeongeza mawanda mapana kabisa ya huduma za kibenki hapa nchini. Hakuna eneo lolote utakapofika hapa nchini ukakosa huduma za kifedha za mawakala wa benki zetu mbalimbali na huduma za *simu banking* katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ndio maana Tanzania inaongoza kwa Afrika kwa huduma za fedha jumuishi. Kwa hiyo, niwaombe sana wananchi wetu Wilaya ya Mlele, Wilaya ya Katavi waweze kuzitumia fursa hizi zilizopo baada ya Serikali yao kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara nchini. Mawakala wengi wa huduma za fedha wapo kwenye maeneo yote nchini na sasa kila mwananchi ana simu yake, tumeweza kusajili simu kwa hiyo sasa hivi ni rahisi sana kufanya *transactions*.

Sasa hivi unapofanya *transaction* niwaambie wananchi wa Tanzania huna wasiwasi wa kutuma pesa yako kwa simu kwa sababu mfumo umeunganishwa na Benki Kuu ya Tanzania, kwa hiyo, unajua kabisa kabla hujatuma kuliko kukaa na kuanza kufikiri fedha yangu imepotelea njiani, sasa unaulizwa kabisa unamtumia fulani bin fulani, una uhakika kwa hiyo hakuna wasiwasi wowote. Niwaombe Watanzania watumie fursa hii ya huduma za fedha jumuishi kwa maendeleo yao na maendeleo ya Taifa letu.

SPIKA: Mheshimiwa Khadija Aboud.

Na. 7

Idara ya Uratibu wa NGOs Kujitegemea

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD aliuliza:-

Idara ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (*NGO's*) inafanya kazi zake kwa weledi na uadilifu mkubwa lakini haina mamlaka ya kujitegemea kama zilivyo *BRELA* na *RITA*.

Je, ni lini Serikali itaipa Mamlaka Idara hiyo kuwa Taasisi inayojitegemea?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017 Ofisi ya Waziri Mkuu iliandaa kikosi cha kupitia, kuchambua na kushauri juu ya namna bora ya uratibu wa mashirika yasiyo ya Serikali. Moja ya mapendekezo yaliyotolewa ni kuifanya Idara ya Mashirika Yasiyo ya Serikali kuwa Taasisi inayojitegemea. Hata hivyo, suala hilo ni la kimuundo na linahitaji maandalizi ya kutosha. Serikali inatoa rasilimali fedha na rasilimali watu wa kutosha pamoja na vitendea kazi muhimu ili kumwezesha Msajili kufanya kazi yake na umadhubuti chini ya usimamizi wa Bodi ya Uratibu wa

Mashirika Yasiyo ya Serikali. Serikali inayafanyia kazi pasipo kuingiliwa na pia ina wawakilishi wa Serikali na NGO's.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Serikali. Serikali imefanya marekebisha ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Serikali, Sheria Na. 3 ya mwaka 2019 na kuweka masharti yote ya kusajili chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Serikali na hivyo kumpa mamlaka mbalimbali Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Serikali ikiwemo kusimamia Shirika husika, kufanya kazi pale linapopatikana na makosa wakati ikisubiri uamuzi wa Bodi. Aidha, mashirika yametakiwa kuwasilisha kwa Msajili taarifa ya utekelezaji ya robo mwaka, taarifa za ukaguzi wa fedha za mwaka na mikataba ya fedha ambayo mashirika yanaingia na wafadhili na kuweka bayana kwa umma taarifa za mapato na matumizi ili kongeza uwazi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, nyenzo hizo ni muhimu katika kumfanya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Serikali kufuatilia utendaji wa mashirika hayo na hivyo kuchukua hatua stahiki. Hivyo kwa sasa Serikali haina mpango wa kuifanya Idara ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Serikali kuwa Taasisi inayojitegemea.

SPIKA: Mheshimiwa Khadija Aboud, swali la nyongeza.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu haya ya Serikali, pia nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali inazochukua katika kusaidia mashirika haya ya Kiserikali na kuyawekea utaratibu mzuri. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Taasisi Zisizo za Kiserikali, Ofisi za Mrajisi wa Mashirika hayo kati ya Zanzibar na Tanzania Bara wana ushirikiano mzuri na ushirikiano wa pamoja, lakini kuna changamoto moja. Taasisi zisizo za Kiserikali zinapotaka kufungua upande mmoja wa Muungano aidha Bara au Zanzibar taasisi hizo zinalipishwa sawasawa na taasisi za kigeni zinapotaka kufungua Mashirika ya Kiserikali hapa Zanzibar.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto hiyo ili mashirika yetu ya kiserikali ya Zanzibar na Bara yasiwe yanalipishwa sawasawa na taasisi ambazo zinatoka nje ya nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, Taasisi Zisizo za Kiserikali zimekuwa zikitoa mchango mkubwa sana katika kuinua mchango wa nchi na uchumi wa wananchi, zimekuwa zikisaidia sana kutatua baadhi ya changamoto mbalimbali za kusaidia jamii na huduma mbalimbali za kijamii. Je, Serikali inatambua vipi mchango huo wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya maswali haya Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wa karibu sana wa utendaji wa Wizara yetu ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na hususan masuala haya ya NGOs. Niseme tu kwamba kwa mujibu wa sheria tuliyokuwa nayo sasa hivi ambayo inasimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni sheria ambayo si ya Muungano, kwa maana kwamba Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Serikali Tanzania Bara ni tofauti na yule ambaye yuko kule Zanzibar. Hata hivyo, tunatambua kwamba kuna NGOs nyingi hapa nchini ambazo zinafanya kazi Tanzania Bara na vilevile Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Spika, changamoto ambayo ameeleza Mheshimiwa Mbunge tunakiri kwamba tunayo, lakini sisi kama Serikali tulishaanza kuchukua hatua, Msajili wa Mashirika Yasiyo Serikali Tanzania Bara pamoja na kule Zanzibar wamekuwa wakifanya vikao. Kikao cha kwanza walikifanya mwezi Septemba na Disemba mwaka jana wamekaa tena na kuweza kuweka utaratibu mzuri ambapo Taasisi ama NGOs ambazo zinafanya kazi Tanzania Bara zinaweza zikapata unafuu wa kuweza kufanya kazi Zanzibar na zile za Zanzibar zinaweza zikafanya kazi Tanzania Bara wakati marekebisho ya sheria yakiendelea ili kuweza kuweka utaratibu mzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili ameuliza kuhusiana na mchango wa NGOs. Tulipofanya marekebisho ya Sheria ile ya NGO's, lengo na mahususi lilikuwa ni hilo, kwa sababu kwanza kulikuwa kuna mkanganyiko mkubwa sana wa usajili wa NGOs, kulikuwa kuna NGOs ambazo zilikuwa zinasajiliwa chini ya Msajili wa NGOs na kulikuwa kuna NGOs ambazo zilikuwa zinasajiliwa BRELA, kulikuwa kuna NGOs ambazo zilikuwa zinasajiliwa kwa Msajili wa Societies. Usimamizi na mchango ilikuwa ni mgumu sana kuuratibu, lakini kwa utaratibu huu mpya sasa hivi ambao umeuhisha usajili wa NGOs, sasa hivi tutaweza kujua mchango wa NGOs zote takribani 10,000 ndani ya nchi na sisi kama Serikali tutakuwa tunautambua na kuuthamini mchango huo katika taarifa zetu mbalimbali za Serikali.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria sasa swali la Mheshimiwa Dkt. Suleimani Ally Yussuf, Mbunge wa Mgogoni, kwa niaba yake Mheshimiwa Ally Saleh.

Na. 6

Kesi Anazopangiwa Jaji na Hakimu kwa Mwaka

MHE. ALLY SALEH ALLY (K.n.y. MHE. DKT. SULEIMANI ALLY YUSSUF) aliuliza:-

Kutokana na maendeleo ya kiuchumi na kijamii kumekuwa na ongezeko kubwa la makosa katika jamii jambo ambalo linasababisha mfumo wa utoaji haki pamoja na Mahakama kuelemea.

(a) Je, kila Jaji au Hakimu anapangiwa kesi ngapi kwa mwaka ili kupunguza mlundikano wa kesi?

(b) Je, ni mambo gani kimsingi yanayosababisha mashauri kuchukua muda mrefu?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, tafadhali.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Suleimani Ally Yussuf, Mbunge wa Mgogoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania imejiwekea utaratibu ili kuhakikisha mashauri yote yanayofunguliwa Mahakamani yanamalizika kwa wakati. Utaratibu huu ni pamoja na kujiwekea malengo ya idadi ya mashauri yatakayoamuliwa na Jaji na Hakimu kwa mwaka.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, malengo ni kuhakikisha tunapunguza mlundikano wa mashauri Mahakamani ambapo kwa mwaka kila Jaji anatakiwa kumaliza mashauri 220; Mahakimu katika Mahakama za Hakimu Mkazi wa Wilaya kumaliza mashauri 250 na katika Mahakama za Mwanzo 260.

Mheshimiwa Spika, pia Mahakama imejiwekea ukomo wa muda wa mashauri kukaa Mahakamani. Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu ni miaka mwili; Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya mwaka mmoja na Mahakama za Mwanzo ni miezi sita. Mikakati hii imesaidia kupunguza mlundikano wa mashauri kwa kiasi kikubwa hususan kwa Mahakama za Mwanzo ambapo kwa sasa mlundikano wa mashauri ni asilimia sifuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo bado Mahakama zetu zimekuwa zinakabiliwa na changamoto za mlundikano wa mashauri na baadhi ya mashauri kuchukua muda mrefu zaidi. Changamoto hizi zimetokana na idadi ndogo ya Majaji na Mahakimu ikilinganishwa na idadi ya mashauri yanayofunguliwa katika Mahakama zote nchini. Vilevile upelelezi katika Mahakama na mashauri kuchukua muda mrefu na mashahidi kutotoa ushahidi wao kwa wakati katika baadhi ya mashauri yanayofunguliwa katika Mahakama zetu nchini ni miongonzi mwa sababu na baadhi ya mashauri kuchukua muda mrefu Mahakamani. Hata hivyo ninamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa kuteuwa Majaji 11 wa Mahakama ya Rufaa na Majaji 39 wa Mahakama Kuu katika Awamu ya Tano, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri; Mheshimiwa Ally Saleh swali la nyongeza.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kabla ya swali la nyongeza kwanza nilitaka kusema kitu juu ya mfumo wetu huu wa Bunge Mtandao, pengine hili linafaa kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, muuliza swali yupo nje ya Bunge na swali limekuja hakuna access aliyopewa muuliza swali kuweza kulipata swali *in advance*. Kwa hiyo, nimesikiliza swali moja kwa moja bila ya kuwa na taarifa kwa sababu mwenye swali hakuwa na njia ya ku-access.

SPIKA: Mheshimiwa Ally Saleh, hilo lilikuwa tulifanye kwa utaratibu mwingine ni kwamba tu mfumo mtandao unakupiga chenga, lakini hayo mambo yako *covered* kabisa. Kwamba mwenye swali Mbunge yeyote kama hayuko Bungeni analitaarifu Bunge na anataarifu ni nani amuulizie swali lake na huyo anayemuulizia swali lake anatumiwa majibu yote na kila kitu anatumiwa; kwa hiyo, hayo yote yako *covered*, mfumo mtandao yaani uko kisawasawa, uliza swali lako Mheshimiwa Ally Saleh. (*Makofi*)

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, lakini mwenye swali ndio kaniambia kwamba hakuna taarifa yoyote aliyotoa. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Ally Saleh, Spika akishakujulisha unamuamini Spika au unamuamini mwenye swali ambaye wala Bungeni hayupo? (*Kicheko*)

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Spika, nashukuru; dhana ya swali hili ni kwenye haki jamii na kwamba, *issue* kubwa ni kupunguza idadi ya msongamano. Mheshimiwa Waziri hapa amesema kwamba kuna tatizo la idadi ya Majaji au Mahakimu, sasa je, anafikiri katika muda gani Wizara inajipa muda gani kuhakikisha kwamba hali itakuwa inatosha kiwango cha Mahakimu, Majaji na kulingana na kasi ya matendo ya jinai?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, amezungumza habari ya moja katika tatizo ni suala la ushahidi. Je, Mheshimiwa Waziri hafikiri kwamba kuna haja sasa ya kukazia kwenye suala la kukusanya ushahidi kujaribu kutumia mbinu mpya na za kisasa zaidi ili ushahidi ukamilike na ufikishwe Mahakamani kwa wakati, ili raia waweze kupata haki?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, tafadhali.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, katika Awamu hii ya Tano tumejitahidi sana, Serikali sio tu katika kuteuwa Majaji na Mahakimu, lakini pia katika kufungua Mahakama mpya kwenye Wilaya mbalimbali. Kwa kufuata utaratibu huu inaonekana kwamba katika kipindi cha maendeleo cha miaka mitano hii mafanikio ukilinganisha kipindi cha nyuma imekuwa ni asilimia 33.5.

Mheshimiwa Spika, kwa kutazama mwelekeo huu ninadhani tutaweza kufikia hatua nzuri tukimaliza mpango huu wa maendeleo ambao tunaona unamalizika mwaka huu na tukifuata utaratibu tuliokuwa katika mpango uliopita tunaweza kufikia zaidi ya asilimia 50 kwa kuweza kukamilisha mwelekeo wa ujenzi na uteuzi katika miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, katika suala la upelelezi na mashahidi, mfumo mzima wa Mahakama sasa hivi ni kufanya kazi kwa karibu na mtambuka na vyombo vyote vinavyofanya kazi pamoja na haki, hasa Wizara ya Mambo ya Ndani, lakini pia tumeanzisha utaratibu wa *electronic* ambapo tunaweza kusajili, tunaweza kupata ushahidi kwa kutumia *electronic* katika mikoa mitatu sasa hivi na nia yetu ni kuhakikisha kwamba mfumo huu wa *electronic* unaenezwa kwenye mikoa mingine. Na kwa kweli, umesaidia sana katika kuharakisha mfumo mzima wa kutoa haki ikiwa ni pamoja na kutoa ushahidi. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na maswali ya Wizara ya Afya, swali la Mheshimiwa Sikudhani Yasin Chikambo, uliza swali lako Mheshimiwa Chikambo tafadhali.

Na. 8

Watoto wa Mitaani Wanaoishi Mazingira Magumu

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO aliuliza:-

Kumekuwa na wimbi kubwa la watoto wa mitaani ambao wanaishi katika mazingira magumu.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia watoto hao?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, Dkt. Ndugulile tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Yassin Chikambo, Mbunge Viti Maalum kutoka Mkoa wa Ruvuma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na wimbi kubwa la watoto wa mitaani ambao wanaishi katika mazingira magumu. Katika kipindi cha Januari hadi Disemba, 2019 jumla ya watoto 36,548 wakiwemo watoto wa kiume 17,894 na wa kike 18,654 walitambuliwa. Kati ya hao

jumla ya watoto 1,178 walipatiwa huduma mbalimbali ikiwemo huduma za afya, msaada wa kisaikolojia na jamii, msaada wa kisheria, kuunganishwa na familia zao na kuwapatia elimu ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mpango wa kuwaunganisha watoto na familia na kuwatafutia malezi mbadala wale wasio na familia katika Mkoa wa Mwanza. Programu hii imeanza kutekelezwa mwezi Novemba, 2019 na inatarajiwa kufika mikoa yote ambayo ina wimbi kubwa la watoto wanaoishi mitaani.

Mheshimiwa Spika, mwisho nichukue nafasi hii kuikumbusha jamii kuwa jukumu la matunzo, malezi, ulinzi na usalama wa mtoto ni la familia na jamii kwa ujumla. Vilevile Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinapaswa kusimamia Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 ili kuwawajibisha wazazi wanaotelekeza majukumu yao na badala yake wanawaacha watoto kuzurura mitaani.

SPIKA: Mheshimiwa Sikudhani, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza napenda nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo amekiri kwamba watoto wa mitaani wapo.

Mheshimiwa Spika, zipo sababu nyingi zinazosababisha uwepo wa wimbi kubwa la watoto wa mitaani ikiwemo na wazazi na hasa akinababa kutelekeza familia zao.

Je, Serikali inachukua hatua gani pindi inapowabaini wazazi wa aina hiyo, inawachukulia hatua gani katika kuhakikisha wanarudi katika familia zao na familia zinaimarika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali inatekeleza programu ya kuwaunganisha watoto na familia na kuwapa malezi mbadala na Waziri ameeleza kwamba programu hii inatekelezwa katika Mkoa wa Mwanza, tunayo mikoa 26; ni nini sasa mkakati wa Serikali wa kuhakikisha programu hii inafika katika mikoa mingine ikiwemo Mkoa wa Ruvuma ili wazazi na watoto waliopo katika maeneo yale wafaidike na programu hii? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Afya, Mheshimiwa Dkt. Engelbert Ndugulile, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya, lakini kwa ufuatiliaji wa karibu sana kuhusiana na masuala ambayo yanahusiana na haki na ustawi wa watoto Tanzania. Nakupongeza sana Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumekuwa tumeona ongezeko la watoto ambao wanaishi na kuzurura mitaani na moja ya kisababishi ni hiyo sababu ambayo Mheshimiwa Mbunge ameisema, wazazi kutelekeza majukumu yao ya msingi ya kuwasimamia watoto hawa. Na ni kweli kwamba tuna Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 ambayo imetoa haki za msingi kwa mtoto. Na sisi Serikali kupitia Ustawi wa Jamii tumeendelea kuyashughulikia mashauri mbalimbali ya wazazi na hususan akinababa kutelekeza watoto na kuyapeleka Mahakamani kukazia hukumu.

Mheshimiwa Spika, tunatambua bado ipo changamoto ya wigo wa Maafisa Ustawi wa Jamii katika maeneo mbalimbali na sisi kama Serikali tunajaribu sana kuhakikisha kwamba tunaongeza idadi ya Maafisa Ustawi wa Jamii katika maeneo mbalimbali. Lakini vilevile tunaendelea kutafakari kuhusiana na hizi adhabu ambazo tumeziweka, hususan pale ambapo mzazi kuna hukumu ya Mahakama, lakini wazazi wanaendelea kukaidi. Tunaangalia njia bora zaidi ya kuhakikisha kwamba zile adhabu zinawekewa msisitizo.

Mheshimiwa Spika, lakini katika swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge ameuliza kuna hii programu ambayo tumeianza ya kuwaunganisha watoto na walezi ama walezi mbadala ama wazazi mbadala. Hii tumeianza katika ngazi ya majaribio tutakapoona mafanikio na matunda ya programu hii, hapo sasa ndio tutakapoanza kwenda katika maeneo mengine ya nchi hususan majiji ambayo tuna changamoto kubwa ya watoto wanaozurura mitaani.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Ritta Mwamoto Kabati, swali la nyongeza.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze Serikali kwa kuweka mpango mzuri kabisa wa elimu kwa watoto wetu kwamba watoto wote wanahakikisha wanapata elimu, lakini bado kuna wazazi ambao kwa mfano pale Dar es Salaam wanakaa pale barabarani wanawatuma watoto kwenda kuomba kwenye magari, sasa wale watoto wanakosa haki kabisa ya msingi ya kusoma.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba watoto wetu wale wanasoma na wale wazazi wanachukuliwa hatua?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Afya, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya nyongeza kwa Mheshimiwa Chikambo, watoto, labda kwa faida ya Bunge lako tukufu, Tanzania tumeridhia Mkataba wa Kimataifa na sisi tukaanzisha Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ambayo inatoa haki kwa watoto. Mtoto ana haki ya kutunzwa, mtoto ana haki ya kuendelezwa, mtoto ana haki ya kushirikishwa katika maamuzi yanayomhusu na mtoto ana haki ya kutokutumikishwa kazi nzito.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukiangalia katika sheria hii utaona hapa tunagusa katika maeneo makubwa mawili; kwanza haki ya mtoto ya kuendelezwa, lakini haki ya mtoto kutotumikishwa kazi nzito. Serikali tumeendelea kuchukua hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nitumie fursa hii sasa kuongea na kuziagiza Halmashauri za manispaa na majiji kuhakikisha kwamba, wanasimamia kikamilifu sheria hii ya mtoto na ili watoto wale waweze kupata haki yao ya msingi ya kuendelezwa kwa maana ya kusoma, lakini pili kutokutumikishwa kazi na badala yake wale watoto waweze kukaa shuleni na kupata elimu. *(Makofi)*

SPIKA: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo. Mheshimiwa Tunza tafadhali.

Na. 9

Hitaji la X-Ray Hospitali ya Ligula – Mtwara

MHE. TUNZA I. MALAPO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka *x-ray machine* mpya katika Hospitali ya Rufaa ya Mtwara – Ligula?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Afya. Bado tuko Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mtwara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Hospitali ya Ligula inakabiliwa na uchakavu wa mashine ya *x-ray* ambayo uharibika mara kwa mara. Katika ziara yangu ambayo niliifanya katika hospitali hii mnamo tarehe 4 Disemba, 2018 nilijionea uchakavu wa mashine na hivyo tulitoa ahadi ya Serikali ya kuipatia hospitali hii mashine mpya ya *digital x-ray*.

Mheshimiwa Spika, mashine tano mpya za *x-ray* za kidijitali (*digital x-ray*) zimeshaingia nchini kupitia utaratibu wa *managing equipment services* tarehe 14 Januari, 2020. Taratibu za ugomboaji zikikamilika zitapelekwa na kusimikwa katika Hospitali za Rufaa za Njombe, Iringa, Tabora, Temeke pamoja na Mkoa huu wa Mtwara katika Hospitali ya Ligula.

SPIKA: Mheshimiwa Tunza.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Spika, sijui mchakato utakamilika lini, lakini kuna mambo mawili; kunakuwepo mashine na kunakuwepo msomaji. Katika Hospitali hii ya Mkoa wa Mtwara kuna tatizo pia la msomaji wa *x-ray*, mtu amevunjika mkono sehemu ya nyuma, inaonekana amevunjika mkono sehemu ya mbele. Sasa nataka kujua Serikali imejipanga vipi inapopeleka hiyo mashine tena ya *digital* na kumpata mtu ambaye ataendana na hiyo mashine katika usomaji wake?

Mheshimiwa Spika, lakini swali langu la pili, katika Hospitali ile ya Mkoa wa Mtwara kumekuwa na tatizo kubwa la madaktari hasa upande wa wanawake. Nataka kujua Serikali imejipanga vipi na ni lini itapeleka madaktari hao ili kutoa kero hii ambayo iko kwa muda mrefu? Nakushukuru.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Tunza Malapo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri na ufuatiliaji ambao anaufanya katika sekta hii ya afya na hususan katika Mkoa huu wa Mtwara. Labda niseme ni hivi kwamba katika hili eneo ambalo ameligusia kuna mambo mawili kuna suala la mpiga picha ambaye ni *radiographer*, yeye kazi yake ni kupiga picha, lakini tuna *radiologist* ambaye yeye ni msomaji wa picha. *Digital x-ray* tutafunga na ni kama nilivyosema

katika jibu langu la msingi, mashine ziko bandarini tunafanya utaratibu wa ugomboaji na tutaenda kuifunga pale Ligula, *radiographer* tunao.

Mheshimiwa Spika, suala la msomaji tunakuja na utaratibu mpya kwa sababu hii ni *digital x-ray* sisi kama Serikali na sisi tunaingia katika mfumo unaitwa *telemedicine* na tutakuja na kitu kinaitwa *tele-radiology*, kwamba hizi *digital x-ray* zote ambazo tunazifunga kwa kutumia Mkongo wa Taifa pale Muhimbili na pale MOI sasa hivi tumetengeneza kitu kinaitwa *hub*. Tutakuwa na *centre* moja ambayo kutakuwa na *screen* ambayo imeunganishwa na mtandao, picha zitakazopigwa Tanzania kote iwe ni Mbinga, iwe ni Ligula, iwe katika eneo lolote Tanzania hii zitakuwa zinatumiwa, wataalam/madaktari wetu bingwa pale Muhimbili wataisoma ndani ya dakika 15 na lile jibu linarudi tena kulekule ambako linatoka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikutoe mashaka sisi kama Serikali tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba matumizi ya hizi *digital x-rays* zinaweza zikatumiwa na wananchi wa Tanzania wananufaika na utaratibu mpya ambao tumeanza nao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili la Madaktari Bingwa; ni kweli Hospitali ya Mkoa ya Ligula ina changamoto ya Madaktari Bingwa na sasa hivi sisi kama Serikali tunawekeza katika kuhakikisha kwamba hospitali za rufaa za mikoa ikiwa ni pamoja na Ligula tunakuwa na madaktari bingwa wa magonjwa ya wanawake, madaktari bingwa wa magonjwa ya ndani, madaktari bingwa wa magonjwa ya watoto, madaktari bingwa wa magonjwa ya mifupa, madaktari bingwa wa magonjwa ya dharura, pamoja na mengine mengi.

Kwa hiyo, sasa hivi wapo Madaktari wapo katika mfumo wa mafunzo na tumesomesha zaidi ya madaktari 100 kwa mwaka pale watakapokamilisha masomo yao tutawapangia katika hospitali zetu ya Ligula na hospitali zingine za RRH. Lengo na kusudio la Serikali wakati tunaboresha vituo vya afya, hospitali za wilaya, tunataka sasa hospitali za rufaa za mikoa zitoe huduma za kibingwa kama ilivyokusudiwa.

SPIKA: Swali la nyongeza Mheshimiwa Salma Kikwete, tafadhali, nilikuona

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kwanza kabisa kwa masikitiko makubwa naomba nitoe pole zangu za dhati kwa wananchi waliopatwa na kadhia ya mvua na hasa katika Mkoa wetu wa Lindi kule Kilwa, Liwale pamoja na Lindi Vijijini na hasa katika eneo la Mchinga ambao watu wamepoteza makazi yao, mazao yao na vitu vingi mbalimbali, tunawapa pole sana kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nataka niulize swali langu la nyongeza kutokana na swali la msingi namba tisa kuhusu suala la *x-ray*, nitauliza suala la mashine ya *dialysis*. Tunajua na tunatambua kwamba ugonjwa wa kisukari unaongezeka siku hadi siku na kutokana na kuongezeka kwa ugonjwa wa kisukari unapelekea matatizo ya figo na matatizo ya figo yanapelekea watu kufanya *dialysis*. *Dialysis* hizi ziko katika maeneo machache hapa nchini kwetu Tanzania. Je, ni lini mashine za *dialysis* zitapelekwa katika mikoa mbalimbali hapa nchini? Ahsante. (Makofi)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mama Salma Kikwete hasa kwa kutoa pole za kipekee kwa wananchi wa Mchinga. Sasa majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salma Kikwete, Mbunge wa Viti Maalum/Mbunge wa Taifa lakini anawakilisha Mkoa wa Lindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunaona ongezeko kubwa sana la wagonjwa wa figo ambao wanahitaji huduma za kusafisha damu na ni kweli huduma hizi zimekuwa katika hospitali ngazi ya kanda na katika mikoa mingi huduma hii ilikuwa inakosekana hali ambayo ilikuwa inapelekea watu wengi kusafiri muda mrefu kwenda kupata huduma hii. Aina ya huduma hii inahitaji mtu apate *dialysis* mara tatu au nne kwa wiki ili aweze kuendelea na maisha yake. Serikali tumeliona hilo na sasa hivi tumepata *dialysis machines* takribani 45, tunazisambaza katika mikoa nane na mkoa ambao tutaanza nao ni pamoja na Mkoa wa Mtwara, Lindi hatujaiweka katika utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, kusudio letu ni kwamba kadri tunavyojenga uwezo na upatikanaji wa hizi mashine kwa sababu naomba niseme *dialysis machine* si kila mtu ambaye anaweza akaifanya, inahitaji utaalum, inahitaji miundombinu tofauti kabisa, inahitaji maji maalum, inahitaji manesi maalum, kwa hiyo tunaendelea kujenga na kwa kuanzia tunaanza na mikoa nane ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Mtwara, tunaamini kwamba huduma hii sasa tutakuwa tumeisogeza karibu zaidi na wananchi wa Mkoa wa Lindi wakati tunaendelea kujenga uwezo na baada ya hapo tutafika mikoa yote ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Lindi. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana kwa majibu mazuri. Tunaendele na Wizara ya Viwanda na Biashara, swali la Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum, Mbunge wa Welezo, uliza swali lako tafadhali

Na. 10

Vikwazo kwa Bidhaa za Zanzibar Katika Soko la Tanzania Bara

MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM aliuliza:-

Je, ni nini kinasababisha baadhi ya bidhaa zinazozalishwa Zanzibar kupata vikwazo kuingia katika soko la Tanzania Bara?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, *Engineer Stella Manyanya*, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saada Salum Mkuya, Mbunge wa Welezo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu ni moja hatutegemei kuwepo kwa vikwazo vya kibiashara kutoka upande mmoja wa Muungano kwenda upande mwingine. Kinachojitokeza ni changamoto chache za kisheria, kanuni na taratibu ambazo hata hivyo zimewekewa utaratibu mahsusi wa kushughulikia. Utaratibu wa kushughulikia changamoto hizo hufanyika kwa njia ya vikao vya ushirikiano wa kisékta ambapo Ofisi ya Makamu wa Rais imetoa mwongozo wa sekta za pande mbili za Muungano kujadili changamoto kupitia vikao kuanzia ngazi za wataalam, Makatibu Wakuu na Mawaziri na kushauri mamlaka za maamuzi.

Mheshimiwa Spika, chini ya utaratibu huo, sekta ya viwanda na biashara kwa nyakati tofauti imekuwa ikipokea kujadili na kutafutia ufumbuzi changamoto za biashara zilizoibuliwa

kutoka pande zote mbili za Muungano, baadhi ya bidhaa zilizowahi kushughulikiwa chini ya utaratibu huo ni pamoja na kuku, maziwa na bidhaa nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kuwasiliana na kushirikiana katika kushughulikia kwa pamoja changamoto ambazo huenda zikajitokeza ili kuimarisha Muungano wetu na kukuza biashara kwa maslahi mapana ya wananchi wetu kupitia biashara.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya, swali la nyongeza.

MHE. DKT. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza na nashukuru sana majibu ya Serikali kwa swali langu hilo.

Mheshimiwa Spika, biashara ni nyenzo muhimu sana katika uchumi wa mtu binafsi, lakini vilevile uchumi wa Taifa kwa ujumla. Sasa ucheleweshaji wa kutatua changamoto kama hizi ambazo zinapitia katika mfumo ambapo kama Waziri alivyoeleza wa vikao na taratibu, unaathiri moja kwa moja maisha ya watu na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Je, ni lini Serikali itaangalia utaratibu mahsus wa kutatua changamoto hizi za kibiashara hususan kwa biashara ambazo zinatoka Zanzibar zinakuja katika soko la Tanzania Bara kwa sababu hiyo ndio changamoto kubwa ambayo inajitokeza na sio *otherwise?* (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali la pili Zanzibar kwa sasa kuna Taasisi ya Viwango (*Zanzibar Bureau of Standards - ZBS*), lakini mara nyingi bidhaa ambazo zinapimwa na ZBS zikiingia katika soko la Tanzania Bara, wafanyabiashara wanalazimika biashara zile kupimwa tena na TBS.

Je, mfumo wa uthibitishaji wa bidhaa wa ZBS hauaminiki au hauko sambamba na mfumo huu wa TBS mpaka inafanya bidhaa ambazo zinakuja zilizopimwa na ZBS zinapimwa tena na TBS?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mbunge wa Welezo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana ni lini kutakuwa na utaratibu au mfumo maalum. Kwanza niseme tu kwamba kama ambavyo nilieleza hapo awali mfumo upo kulingana na ngazi zetu za kimashirikiano na hasa kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo inashughulikia pia masuala ya Muungano. Kwa bahati mbaya katika maswali yake hajasema hasa bidhaa zipi, amesema kwa ujumla wake, ingekuwa ni bidhaa ipi pengine ingenisaidia zaidi kujua ni kitu gani hasa kishughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba kama ambavyo hata juzi tumeshuhudia ni kwamba changamoto muhimu au jambo muhimu linalotakiwa wakati tunapohitaji kujadili juu ya changamoto zinazowakabili wafanyabiashara hao, ni vyema kuwa na umakini, lakini pia kuwa na maelezo ya kina yanayozungumzia hilo suala baada ya kulifanyia utafiti na tafakari ya kutosha. Kwa mfano katika kipindi cha nyuma nimejibu zaidi ya maswali manne yakizungumzia suala la sukari kuingia Tanzania Bara, lakini hivi karibuni tumeshuhudia kuona kwamba kumbe

sukari hata inayozalishwa katika Kiwanda cha Mahonda ilikuwa hata haitoshelezi kwa upande wa Zanzibar endapo hakuna sukari nyingine itakayoagizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni mambo ambayo wote inabidi tuyaangalie kwa pamoja. Vilevile Mheshimiwa Makamu wa Rais juzi amesisitiza juu ya umuhimu wa sisi kufanya kazi kwa pamoja kwa mashirikiano na bila kubaguana na hiyo ndio iwe *spirit* yetu katika kujenga umoja wetu na mashirikiano.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili TBS na ZBS, niseme tu kwamba kupitia hii *blueprint* katika mambo ambayo yataangaliwa ni pamoja na taasisi ambazo zimekuwa zikifanya kazi kwa pamoja za Kimuungano na hata za Kimataifa ili kuwapunguzia vikwazo wafanyabiashara wetu.

Kwa hiyo, naamini na hilo pia litashughulikiwa kuweza kuona ni jinsi gani mamlaka zetu zote mbili zinajengewa uwezo na kuwa na uelewa wa pamoja ili bidhaa ikikaguliwa upande mmoja isiwe lazima kukaguliwa upande wa pili.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Maji, swali linaulizwa na Mheshimiwa Joseph Roman Selasini.

Na. 11

Tatizo la Maji - Jimbo la Rombo

MHE. JOSEPH R. SELASINI aliuliza:-

Jimbo la Rombo hususan ukanda wa chini wenye takribani vijiji 41 lina shida ya maji; na Halmashauri imeanzisha mradi wa kupanua bomba kubwa la maji linalotoka Marangu. Aidha, Halmashauri ilipendekeza vyanzo vingine ikiwemo matumizi ya maji na Ziwa Chala, uchimbaji wa visima na mabwawa yatokanayo na mito ya msimu.

(a) Je, Serikali imekubali mpango wa kuanza kutumia maji ya Ziwa Chala?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kutosha ili mradi huo uweze kuanza?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, tafadhali, Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Jimbo la Rombo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali tayari ina mpango wa kutumia Ziwa Chala kama chanzo cha maji kwa wananchi wa Rombo. Uamuzi huo ulitokana na upembuzi yakinifu na usanifu uliofanyika kuanzia mwezi Machi, 2019 na kukamilika mwezi Julai, 2019. Upembuzi huo ulibainisha vyanzo vinne vya maji ambavyo ni chanzo cha maji cha Ziwa Chala kitakachohudumia vijiji 21 na vyanzo vingine vitatu vya maji vya mtiririko Mto Njoro, Mto Yona na Marangu na Uswai Wambushi.

Mheshimiwa Spika, makisio ya awali ya mradi huo ni shilingi bilioni 40 ambapo ujenzi wake uliamuliwa ufanyike kwa awamu. Awamu ya kwanza itahusu ujenzi wa chanzo cha maji cha Njoro ambacho kitahudumia Mji wa Tarakea na vijiji jirani na katika mwaka wa fedha

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

2019/2020 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mradi huo Serikali itaendelea kutenga fedha kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya kukamilisha awamu ya kwanza na kuanza awamu nyingine.

Mheshimiwa Spika, baada ya awamu zote kukamilika mradi huu unatarajia kuhudumia vijiji vya Kikelelwa, Mbomai, Kibaoni, Nayeme, Nasae, Msanjai, Urauri, Ushiri, Ikuini, Mrao, Kiruakeni, Kisale, Marangu, Mamsera, Mahida, Holili, Mengwe na Ngoyoni vyenye jumla ya watu 157,000.

SPIKA: Swali la nyongeza kwa muuliza swali, Mheshimiwa Selasini, tafadhali

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Matumizi ya maji ya Ziwa Chala yaliombwa hapa Bungeni na Wabunge wote walionitangulia; Mheshimiwa Alphonse Maskini, Mheshimiwa Aloyce Ngalai, Mheshimiwa Justine Sarakana, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba na Awamu zote Tano za utawala wa nchi hii. Naomba nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano na kuishukuru kwa uamuzi wake wa kuamua kutumia maji haya kwa ajili ya wananchi wa Rombo na nina hakika kama mradi huu utatekelezwa shida ya maji katika Jimbo la Rombo itakuwa ni historia. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa kuuliza mradi huu unategemewa kuanza na kumalizika lini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, hivi sasa kuna visima viwili ambavyo vimeshakamilika vinatusumbua sana pale Rombo, Kisima cha Leto na Kisima cha Shimbi Mashariki. Namshukuru Naibu Waziri, wiki iliyopita alikuwa Rombo na alitoa maagizo ili haya maji yapate kutumika kwa wananchi.

Sasa swali langu maagizo yamekuwa yanatolewa lakini hayatekelezwi, je, sasa Serikali iko tayari kuwashughulikia maafisa na watendaji ambao wanazuia maji haya yasitumike na kusababisha mateso kwa wananchi?

SPIKA: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji tafadhali

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kiukweli uungwana ni vitendo Mheshimiwa Mbunge ni muungwana. Kutokana na uungwana huo wa kushukuru sisi kama Serikali nataka nimhakikishie tutatekeleza Mradi ule wa Ziwa Chala katika kuhakikisha tunaondoa kabisa tatizo la maji na mpaka hivi tunavyozungumza tulishatoa agizo kwa maana ya wataalam wetu waweze kufanya makisio na tutawatumia shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya uanzaji wa mradi ule ili wananchi wake waweze kupata huduma ya maji. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Spika, la pili nikiri kabisa tuna Mradi wa Leto pamoja na Shimbi Mashariki, nimetoka juzi, moja ya changamoto ulikuwa ni uzembe wa mkandarasi ilihali fedha tumempa. Kwa hiyo tumemwagiza na tumemshughulikia ipasavyo, ndani ya wiki hii maji yale yatafunguliwa na wananchi wako wataweza kupata huduma ya maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Baada ya swali zuri sana kwa siku ya leo lililoulizwa na Mheshimiwa Selasini nadhani hakuna haja ya kuendelea na kipindi cha maswali tena, maswali mawili yaliyobaki yatafunguliwa wakati mwingine. Kwa hiyo tuendeele na shughuli nyingine. *(Makofi)*

Katibu shughuli inayofuata.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

SPIKA: Miswada ya Sheria ya Serikali, Katibu tena!

NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya marekebisho katika Sheria ya Usuluhishi kwa lengo la kuweka masharti ya utatuzi wa migogoro kirafiki nje ya mfumo wa mahakama pamoja na kuwezesha makubaliano ya kiusuluhishi yaani *A Bill to an Act to Amend the Arbitration Act for the purpose of facilitating amicable settlement of disputes outside the court system as well as enforceability of Arbitration Agreement.*

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

SPIKA: Ahsante Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba muda mrefu mmekuwa hamko pamoja lakini basi tupunguze sauti tafadhali. Mheshimiwa Waitara nakuona, nitaanza kutaja sasa wanaosimama na kupiga soga humu, naomba tutulie.

Kwa hiyo, Muswada huo umeshasomwa kwa mara ya kwanza *The Arbitration Bill, 2020*, tuendelee na maandalizi na nimeupeleka kwenye Kamati ya Sheria Ndogo ya Mheshimiwa Chenge kwa ajili ya uchambuzi.

Katibu tunaendelea na shughuli inayofuata.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

HOJA YA KUTENGUA KANUNI

SPIKA: Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye pia ni *Chief Whip* atusomee.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kutoa maelezo ya hoja ya kutengua kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya 153(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeanzisha utaratibu wa kukabidhi majoho ya Uspika kwa Maspika Wastaafu wa Bunge kama moja ya njia ya kuenzi kazi zao na kuwawezesha nao kuwa na kumbukumbu ya kazi iliyotukuka waliyoifanya kwa Bunge hili na Taifa kwa ujumla, ambapo shughuli ya kukabidhi majoho kwa Maspika Wastaafu watatu imepangwa kufanyika ndani ya ukumbi wa Bunge letu tukufu leo tarehe 28 Januari, 2020;

Na kwa kuwa kanuni za Bunge zimeweka utaratibu wa wageni kuingia ndani ya ukumbi wa Bunge na kukaa katika sehemu mahsusi zilizotengwa kwa ajili yao;

Na kwa kuwa ili Waheshimiwa Maspika Wastaafu waweze kuingia ndani ya ukumbi wa Bunge italazimu Kanuni za Kudumu za Bunge zitenguliwe ili waruhusiwe kuingia na kukaa ndani ya Ukumbi wa Bunge;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba Kanuni ya 139(1) na Kanuni ya 143(a) ambazo kwa ujumla wake zinaelekeza kwamba wageni Bungeni watakaa kwenye majukwaa maalum ya kukaa wageni zitenguliwe ili Mheshimiwa Pius Chipanda Msekwa na Mheshimiwa Anne Semamba Makinda waweze kuingia ndani ya ukumbi wa Bunge na kukaa kwenye sehemu mahsusi iliyoandaliwa kwa ajili yao katika shughuli ya kukabidhi majoho kwa Maspika hao wastaafu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

SPIKA: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, baada ya Azimio hili, naomba sasa uagize ili Waheshimiwa Maspika Wastaafu waingie ndani kwa utaratibu ambao umepangwa.

SPIKA: Sasa Waheshimiwa Wabunge tujiandae kuwapokea wazee wetu hawa. *Sergeant-At-Arms* naomba uwalete Maspika wastaafu pamoja na Mheshimiwa mama Margaret Sitta. Msafara utaanza na mama Makinda aliyekuwa Spika wa mwisho. *(Makofi)*

(Hapa Spika Mstaafu Mhe. Anne S. Makinda aliingia ukumbini na kukaa katika eneo maalum lililoandaliwa kwa ajili yake)

SPIKA: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kwa mapokezi ya heshima kwa mama yetu Mama Makinda. *(Makofi/Vigelegele)*

Sasa naomba kwa niaba ya Marehemu Spika Samuel John Sitta sasa Mke wa Marehemu Mheshimiwa Margaret na yeye aweze kuingizwa ukumbini. *(Makofi/Vigelegele)*

(Hapa Mhe. Margaret S. Sitta, Mke wa Spika Mstaafu (Marehemu Samuel J. Sitta) aliingia ukumbini na kukaa katika eneo maalum lililoandaliwa kwa ajili yake)

SPIKA: Karibu sana mama yetu Mama Margaret Sitta, Mbunge mwenzetu, karibu sana.

Sasa *Sergeant-At-Arms* umlete Spika Mstaafu Mzee Pius Chipanda Msekwa. *(Makofi)*

(Hapa Spika Mstaafu Pius Chipanda Msekwa aliingia ukumbini na kukaa katika eneo maalum lililoandaliwa kwa ajili yake)

SPIKA: Karibu sana Mheshimiwa Spika Mstaafu, Mheshimiwa Pius Msekwa, karibu ukae. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, ni heshima kubwa sana kwetu kupata fursa hii ya kuwakaribisha wazee wetu hawa na viongozi wetu miongoni mwetu. Kama tunavyojua

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mchango wao umekuwa mkubwa sana katika kujenga demokrasia ya Kibunge katika nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, uongozi wa Bunge, Tume ya Bunge, Kamati ya Uongozi na Wabunge wote wameridhia kabisa leo tuwaite muwe pamoja nasi kwa muda huu mfupi basi tuweze kupata nafasi ya kuwakabidhi majoho mliyoyatumia mlipokuwepo hapa iwe ni sehemu ya kumbukumbu zenu katika utumishi wa Bunge hili na ni heshima kubwa sana kwetu kwamba mmekubali wito wetu. Mmesafiri kutoka mbali na kufika kuwa pamoja nasi, tumefarijika sana na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Lakini kabla hatujaendelea naomba nitumie fursa hii kutambulisha wageni waliokuja ili pamoja nanyi muweze kuona jinsi ambavyo tumepata wageni wengi waliposikia jambo hili la ninyi kuja hapa basi wamekuja wawe pamoja nasi.

Kwanza niwatambulishie Mawaziri Wakuu Wastaafu, Mheshimiwa Edward Lowassa yuko pamoja nasi. Ahsante sana, mzee wetu Mheshimiwa Edward Lowassa akiwa Waziri Mkuu, yeye alifanya kazi na Spika Marehemu Samuel Sitta. *(Makofi/Vigelegele)*

Lakini pia tunae Waziri Mkuu Mstaafu, Makamu wa Kwanza na Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa John Samwel Malecela, yeye alifanya kazi na Mheshimiwa Pius Msekwa akiwa Spika. *(Makofi/Vigelegele)*

Tunaye Mheshimiwa Frederick Sumaye ambaye alifanya kazi katika kipindi chake chote cha Uwaziri Mkuu na Mheshimiwa Spika Pius Msekwa. *(Makofi)*

Tunao viongozi waandamizi wa Chama cha Mapinduzi akiwepo Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Dkt. Bashiru Ally. *(Makofi/Vigelegele)*

(Hapa Wabunge wa CCM walishangilia CCM, CCM, CCM)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Baadhi ya Wabunge wananiambia hawajakuona Katibu Mkuu bado. Tunaomba usimame tena. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Baba lao! Baba lao huyo.

MBUNGE FULANI: CCM baba lao! Katibu Mkuu baba lao!

SPIKA: Mheshimiwa Katibu Mkuu hii inaashiria kwamba bado Bunge moja tu lijalo tuingie kwenye kilinge cha Uchaguzi Mkuu. *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Bashiru baba lao! Bashiru baba lao!

MBUNGE FULANI: Wote tunarudi!

SPIKA: Ahsante sana. Lakini pia Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima kubwa kabisa, naomba niwatambulishie Mheshimiwa Spika Mstaafu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mheshimiwa Pandu Ameir Kificho ambaye pia amesafiri kuja kuwa pamoja nasi. Ahsante sana Mzee Kificho. *(Makofi/Vigelegele)*

Mzee Kificho amefanya kazi kwa muda mrefu akiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi na amefanya kazi kwa karibu sana na Maspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Lakini kama mnavyokumbuka alikuwa Mwenyekiti wa muda wa Bunge la Katiba kwenye ukumbi huu na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

alifanya kazi nzuri sana. Tunakushukuru sana kusafiri kutoka Zanzibar na kuweza kuja kwa ajili ya jambo hili muhimu. Ahsante sana Mzee Kificho. *(Makofi)*

Lakini tunao wake wa viongozi Mama Regina Lowassa yuko hapa Mke wa Mheshimiwa Edward Lowassa. Ahsante mama. Ahsante sana na kama mnavyoona amependeza kweli kweli. *(Makofi)*

Lakini yuko Mama Anna Abdallah, Mke wa Mheshimiwa Pius Msekwa. Bado ana nguvu kabisa Mama Anna Abdallah, leo ni furaha kweli kuwaona wazee wetu hawa. Karibu sana Mama Anna Abdallah. *(Makofi)*

Lakini pia tunao Makatibu wa Bunge wastaafu waliofanya kazi na baadhi ya Maspika hawa. Tunae Ndugu George Francis Mlawa alifanya kazi na Spika Pius Msekwa, karibu sana. *(Makofi)*

Baadaye tutasomewa wasifu, sikumbuki vizuri historia lakini Katibu wa kwanza mzalendo wa Bunge la Tanzania ni Mzee Pius Msekwa mwenyewe. *(Makofi)*

Lakini baada ya George Mlawa alifuata Jaji Kipenka Musa ambaye alifanya kazi na Spika Pius Msekwa. Tunashukuru sana Mheshimiwa Jaji kuweza kusafiri na kuwa pamoja nasi, karibu sana. *(Makofi)*

Baada ya Jaji Kipenka Musa alifuata Damian Foka ambaye alifanya kazi na Spika Samuel Sitta. Karibu sana Ndugu Damian Foka. *(Makofi)*

Baada yake akafuata Dkt. Thomas Kashillillah... *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Oyooo! *(Makofi/Vigelegele)*

SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Nashukuru sana. Basi Dkt. KashiLillah naomba usimame tena ndugu yangu maana yake... *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Katibu wetu huyo alifanya kazi na Mheshimiwa Spika Samuel Sitta, Spika Anne Makinda na alifanya kazi na mimi pia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa haraka haraka tunao wageni wengine. Tunaye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Binilith Mahenge yuko pamoja nasi. Ahsante sana Mkuu wa Mkoa kwa kufika. *(Makofi)*

Tunaye Jaji Mfawidhi Kanda ya Dodoma Mheshimiwa Siane Mohammed, ahsante sana Mheshimiwa Jaji. *(Makofi)*

Tunaye Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma Ndugu Maduka Kessy, karibu sana Katibu Tawala. *(Makofi)*

Tunaye Naibu Meya wa Jiji la Dodoma Ndugu Emmanuel Chibango. *(Makofi)*

Tunaye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mheshimiwa Patrobas Katambi. *(Makofi)*

Lakini pia tumewaalika Watumishi Waandamizi wa Bunge ambao ni wastaafu, Ndugu Japhet Sagasii, karibu. *(Makofi)*

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ndugu Eliakim Mrema, Ndugu John Joel, Ndugu Goodchance Kombe, huyu alikuwa Mweka Hazina. Lakini pia alikuwepo Msaidizi wa Mzee Samuel Sitta na Mzee Msekwa, Ndugu Christopher Ndal. Karibu sana Mzee Ndal. *(Makofi)*

Wapo watoto wa Mheshimiwa Marehemu Samuel Sitta, Ndugu John Sitta, Ndugu Edward Sitta, Ndugu Samuel Sitta *Junior* na Ndugu Benjamin Sitta, naomba msimame kwa pamoja. *(Makofi)*

Wakuu wa Vyuo Vikuu vilivyoko Dodoma, Kaimu Makamu wa Chuo cha *UDOM*, Profesa Donald Mpanduji, karibu sana. Yuko Makamu Mkuu wa Chuo cha St. John Profesa Yohana Msanjila. Ahsante na karibu sana. *(Makofi)*

Viongozi wa Taasisi zinazoongozwa na Maspika Wastaafu, yuko Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Profesa Bernadetha Killian, karibu sana. Yuko Meneja wa Kitengo kinachoangalia uhai na uendelevu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*) Ndugu Baraka Maduhu. *(Makofi)*

Wapo viongozi wa dini, Askofu Mkuu kanisa la Anglikana hapa Dodoma, yuko Askofu wa *KKKT* Dodoma, yuko Askofu Mkuu wa Jimbo Katoliki Dodoma, yuko Sheikh wa Mkoa *BAKWATA* Dodoma, yuko Askofu Mkuu wa kanisa ya Pentekoste Dodoma na yuko Kiongozi Mkuu wa Hindu Mabohora hapa Dodoma. Kwa hiyo tunao viongozi wa dini. *(Makofi)*

Wako wazee wa Mkoa wa Dodoma, Mzee Job Lusinde, ahsante na Mzee Mohammed Makubeli. *(Makofi)*

Wageni wangu wengine ni kutoka *Tanzania Chamber of Commerce Industry and Agriculture*, Rais wa *TCCIA* - Ndugu Paul Koi, Makamu wa Rais - Ndugu Julius Kaijage, Mjumbe wa Bodi - Ndugu Swala Swala, Mjumbe wa Bodi - Ndugu Meshack Kulwa, Mkurugenzi Mtendaji - Ndugu George Lengeju na Msaidizi wa Rais wa *TCCIA* Janeth Kambona. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ambao tuliwaalika ni Mheshimiwa Makongoro Nyerere ambaye amefuatana na Ndugu Deus Wambura ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana kule Butiama. Lakini pia tunaye pia Mwenyekiti wa *CCM* Mkoa wa Tabora, karibu sana. *(Makofi)*

Kwa jinsi shughuli za leo zilivyo, naomba wageni wa Waheshimiwa Wabunge tuahirishe, tutawataja wakati mwingine.

Basi kwa hatua hii Waheshimiwa Wabunge sasa naomba nitumie fursa hii kwanza kuwakaribisha sana hapa Bungeni viongozi wetu hawa wastaafu. Hii ni nafasi adimu sana kutokea na pengine haijawahi kutokea huko nyuma kwa Maspika Wastaafu kuja kukaa ndani ya Bunge kama jinsi ambavyo tumefanya leo. Tunawashukuru sana kwa kukubali wito wetu wa kuja hapa Dodoma na kuungana nasi, ni heshima kubwa. *(Makofi)*

Kama njia mojawapo ya kuenzi kazi zao Maspika hawa kwa Bunge hili, lakini pia kuwawezesha nao kuwa na kumbukumbu muhimu ya kazi iliyotukuka waliyofanya kwa Bunge hili na Taifa letu kwa ujumla, tumeamua kuanzisha utaratibu huu ambapo kuanzia sasa Maspika Wastaafu watakuwa wanakabidhiwa majoho waliyoyatumia wakati wa vipindi vyao vya uongozi, lakini viongozi wengine pia wakiwemo Makatibu na kadhalika ambao walivaa majoho, wao tutakuwa tunawakabidhi kwa utaratibu mwingine nje ya ukumbi kadri tutakavyopanga

hapo baadaye. Utaratibu huu umekuwa ukifanyika katika Mabunge mengine duniani na sisi tumeona ni vizuri tukafanya hivyo. *(Makofi)*

Kuanzia nchi yetu ilivyopata uhuru mwaka 1961, tumewahi kuwa na Maspika wa Bunge sasa takribani saba ambao wa kwanza alikuwa ni Abdulkareem Yusuf Ali Alibhai Karimjee, akafuatiwa na Chifu Adam Sapi Mkwawa, akafuatiwa na Chifu Erasto Andrew Mang'anya, akafuatiwa na Pius Chipanda Msekwa, akaja Samuel John Sitta, akaja Anne Semamba Makinda na sasa ni mimi. *(Makofi)*

Wakati wa kipindi cha Maspika watatu wa mwazo, utaratibu wa mavazi ya Spika bado ulikuwa ni tofauti kidogo. Kumbukumbu zinaonesha kwamba Spika wa kwanza kuvaa joho hili ambalo nimelivaa mimi hapa alikuwa ni Mheshimiwa Pius Msekwa ambaye kwa kweli ndiye aliyebuni hata liweje na nakshi nakshi zake zilivyo hizi ni kazi yake yeye. *(Makofi)*

Kabla yake alikuwa Spika Chifu Adam Sapi Mkwawa na alikuwa akivaa mavazi ya Chifu wa kabila la Wahehe, ndiyo alikuwa akiyatumia akiwa anaongoza hapa na kilemba kile cha Chifu wa Kihehe. Ikatolewa hoja, nilikuwa najaribu kuangalia kwenye kumbukumbu na *Hansard* sijaipata vizuri, wakati huo Bunge likikutana pale ambapo ipo Benki ya NMB leo, kwenye Jengo la CCM wakati ule wa chama kimoja, nadhani ni kama Mzee Sitta ndio alitoa hoja wakati huo Chifu mwenyewe akiwa kwenye kiti kwamba ikitokea Chifu hayupo, hivi Spika anayefuata nani atamsaidia kufunga kile kilemba cha Kihehe asubuhi kabla hajaingia hapa Bungeni, ikaonekana itakuwa mtihani mkubwa.

Kwa hiyo, ndio likatolewa azimio la kwamba patafutwe joho na joho hilo wa kwanza kulivaa ni Mzee Msekwa, kama nimekosea hii historia nitakaa na Mzee Msekwa siku moja ataiweka sawasawa. Kwa hiyo, tunashukuru kwamba jambo hili likaweza kufanyika wakati huo. *(Makofi)*

Yafaa niwajulishe pia kuwa hivi karibuni nilishiriki katika Mkutano wa Maspika wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola kule Ottawa, Canada na desturi ya mkutano huu siku ya kwanza Maspika wote wanaohudhuria huwa wanavaa majoho yao katika maandamano maalum mnapoingia kwenye ukumbi wa mkutano. Kwa kweli niseme mnaona kwenye luninga baadhi ya Maspika niliokuwa nao kule, joho letu ni joho la kipekee na lilitia fora katika Maspika wote waliohudhuria, mnaona la kwetu lilikuwa tofauti na linapendeza kweli kweli. Kwa hiyo, hongera sana Mzee Msekwa kwa kubuni joho hili. *(Makofi)*

(Hapa luninga za ukumbini zilionyesha picha ya baadhi ya Maspika wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola wakiwa wamevaa majoho yao)

SPIKA: Sasa baada ya kusema hayo, tunaanza shughuli yetu rasmi sasa, tutaanza kwa kusoma wasifu wa kila mmojawapo na wasoma wasifu watausoma palepale walipo. Tuanze na wasifu wa Mheshimiwa Mama Anne Semamba Makinda aliyekuwa wa mwisho katika Uspika na wasifu huo utasomwa na *Chief Whip* wetu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, hapo hapo ulipo tafadhali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi sasa mbele ya Bunge lako tukufu niweze kusoma wasifu wa Spika Mstaafu mwanamke wa kwanza Tanzania, Mheshimiwa Mama Anne Semamba Makinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaanza na kuzaliwa kwake na elimu yake; Mheshimiwa Anne Semamba Makinda alizaliwa tarehe 26 Julai, 1949 Wilaya ya Njombe, Mkoa wa Iringa kwa

wakati huo. Alisoma shule ya Msingi Uwemba na Peramiho shule ya kati (*middle school*) kuanzia mwaka 1957 hadi mwaka 1964. Alijiunga na masomo ya sekondari katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Masasi, Mtwara kuanzia mwaka 1965 hadi mwaka 1968 na kisha *Kilakala High School*, Morogoro kuanzia mwaka 1969 hadi mwaka 1970. Mama Makinda oyeeee. (Makofi)

WABUNGE FULANI: Oyeeee. (Makofi)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Makinda alipata elimu ya juu katika Chuo cha Uongozi Mzumbe (*IDM*) kuanzia mwaka 1971 hadi mwaka 1975 ambapo alisomea fani ya uhasibu. Aidha, alijiunga na masomo katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha (*IFM*), Dar es Salaam kuanzia mwaka 1975 hadi mwaka 1976 kwa ajili ya maandalizi ya kufanya mtihani wa *CPA (Certified Public Accountancy Examinations)*.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nisome uzoefu katika utumishi wake wa umma; Mheshimiwa Makinda aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu mwaka 1983 mpaka mwaka 1990 akishughulikia Bunge, Habari na Maafa. Akiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Makinda kwa nyakati tofauti alifanya kazi na Mawaziri Wakuu wanne ambao ni Marehemu Edward Moringe Sokoine, Mheshimiwa Dkt. Salim Ahmed Salim, Mheshimiwa Cleopa David Msuya na kisha Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba. Aidha, aliteuliwa kuwa Waziri wa kwanza wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto mwaka 1990 hadi mwaka 1995. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika medani za kimataifa Mheshimiwa Makinda alikuwa Rais na mwanamke wa kwanza wa Kamati ya Utendaji ya Shirika la Umoja wa Mataifa (*UNICEF*) kati ya mwaka 1993 hadi mwaka 1994. Kati ya mwaka 1984 hadi 1986 alikuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Utendaji ya Shirika la Habari la Afrika (*Pan Africa News Agency*) lililokuwa na Makao yake Makuu huko Senegal. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Makinda aliteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma mwaka 1995 hadi mwaka 2000. Aidha, kwa nyakati tofauti Mheshimiwa Makinda aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi mbalimbali kama ifuatavyo; Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya *MKURABITA (Tanzania Property and Business Formalization Program)* toka mwaka 2010 hadi 2015. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Makinda pia alikuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) toka mwaka 2001 hadi mwaka 2006. Mheshimiwa Makinda amewahi pia kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Chai kuanzia mwaka 2010 hadi 2015, Mheshimiwa Makinda oyeeee.

WABUNGE FULANI: Oyeeee. (Makofi)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Makinda kwa nyakati tofauti amewahi kuwa Mjumbe wa Bodi za Wakurugenzi katika mashirika mbalimbali kuanzia mwaka 1975 hadi 1983 kama ifuatavyo; Shirika la Umeme Tanzania, Benki ya Taifa ya Biashara, Shirika la Reli Tanzania, *Tanganyika Railways Corporation*, Shirika la Elimu Tanzania na *Tanzania Textile Company*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Makinda ni Mwenyekiti ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuanzia mwaka 2016 wadhifa anaoendelea nao hadi sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nilete uzoefu wa Mheshimiwa Makinda katika masuala ya Kibunge; Mheshimiwa Makinda alichaguliwa kuwa Mbunge kuanzia mwaka 1975 hadi 1995 akiwakilisha vijana. Aidha, alichaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Njombe Kusini kuanzia mwaka 1995 hadi mwaka 2015. Mheshimiwa Makinda ni miongoni mwa Wabunge waliokaa Bungeni kwa miaka mingi yaani miaka 40. *(Makofi/Vigelegele)*

WABUNGE FULANI: Rudia hapo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, nirudie kidogo eeh?

WABUNGE FULANI: Eeh.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, aidha, Mheshimiwa Mama Makinda ni miongoni mwa Wabunge na naweza kusema Wabunge wachache waliokaa Bungeni kwa miaka mingi, amekaa Bungeni miaka 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani kwa uwepo wake hapa leo naomba niseme mwingine aliyevunja rekodi ya kukaa miaka 40 Bungeni na ambaye tunae hapa ndani leo na kwa namna ya pekee ni mwanamke pia ni Mheshimiwa Mama Anne Magreth Abdallah ambaye ni mke wa Mheshimiwa Pius Chipanda Msekwa. *(Makofi/Vigelegele)*

SPIKA: Mheshimiwa *Chief Whip* kwa taarifa tu ya Waheshimiwa Wabunge, Bunge hili la Kumi na Moja lina Wabunge 78 ambao wapo chini ya miaka 40; yaani umri wao wenyewe ni chini ya miaka 40. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri unaweza kuendelea. *(Kicheko)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa taarifa hiyo kwa sababu inatusaidia kuona ni namna gani viongozi wetu wamelitumikia Bunge kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Makinda alikuwa Mnadhimu wa Serikali aliyefanya kazi na Mawaziri Wakuu wengi kuliko mnadhimu mwingine yeyote mpaka sasa. Akiwa Bungeni, Mheshimiwa Makinda amekuwa mmoja wa waasisi na Mwenyekiti wa kwanza wa Chama cha Wabunge Wanawake (TWPG) na Mwenyekiti wa Bunge kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2010. Vilevile Mheshimiwa Makinda alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira, Utalii na Maliasili kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Mama Makinda akiwa Mwenyekiti wewe mwenyewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai ulikuwa Makamu wake kwenye Kamati hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Makinda amekuwa Mjumbe wa Jukwaa la Kibunge la SADC-PF toka mwaka 2000 hadi 2010. Vilevile alikuwa Makamu Mwenyekiti wa SADC-PF kuanzia mwaka 2008 hadi 2010. Mheshimiwa Makinda amekuwa pia Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 2005 hadi 2010. Mheshimiwa Makinda amekuwa Spika wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 2010 hadi 2015. Wadhifa huu ulimfanya Mheshimiwa Makinda kuwa mwanamke wa kwanza nchini Tanzania kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Akiwa Spika amekuwa pia Rais wa

SADC-PF mwaka 2014 hadi mwaka 2015 na Mwenyekiti wa CPA Kanda ya Afrika mwaka 2014. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nitachomekea hapo kidogo kabla ya maneno ya kuhitimisha, Mama Makinda na wanawake wengine wa namna hiyo wametengeneza mfano mzuri wa wanawake wengi kujiunga na medani za kisiasa hapa nchini Tanzania. Kwa hiyo, wanawake wa Tanzania tunamshukuru sana Mama Makinda kwa kazi hiyo nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya wasifu huo, kwa ridhaa yako naomba sasa Mheshimiwa Anne Semamba Makinda asogee mbele ili umkabidhi joho lake na kumvalisha kama heshima kwake katika Mkutano wako huu wa leo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

SPIKA: Ahsante, Mama Makinda nakuomba hapa mbele.

Hapa Spika Mstaafu (Mheshimiwa Anne S. Makinda) Alivalishwa Joho

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuombe Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwakyembe, atusomee wasifu wa Mheshimiwa Spika Mstaafu, Marehemu Samuel John Sitta. Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe tafadhali.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba sasa nisome wasifu wa Marehemu Mheshimiwa Samuel John Sitta, Spika wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, kuzaliwa na elimu; Marehemu Mheshimiwa Samuel John Sitta alizaliwa tarehe 18 Disemba, 1942 Urambo, Mkoani Tabora. Mwaka 1950 hadi 1953 Mheshimiwa Samuel Sitta alisoma Shule ya Msingi ya Urambo. Mwaka 1954 mpaka 1957 alijiunga na masomo ya *Middle School* Sikonge ambapo alifaulu vizuri na kujiunga na Shule ya Sekondari ya Wavulana Tabora kuanzia mwaka 1958 mpaka 1963 ambapo alisoma kidato cha kwanza hadi cha sita.

Aidha, mwaka 1964 Mheshimiwa Sitta alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo baadaye alihitimu Shahada ya Sheria mwaka 1971. Mwaka 1976 Mheshimiwa Sitta alihitimu *diploma* katika masuala ya utawala nchini Uswisi na mwaka 2014 alipata cheti cha mafunzo ya uongozi kutoka Chuo Kikuu cha Harvard nchini Marekani.

Mheshimiwa Spika, utumishi wa umma; mwaka 1967 Mheshimiwa Samuel Sitta aliajiriwa na Kampuni *Caltex Oil* kama Meneja wa Kampuni. Miaka miwili baadaye yaani mwaka 1969 aliajiriwa na Shrika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) kama Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi na Mkurugenzi wa Utawala hadi mwaka 1975. Kati ya mwaka 1975 na 1995, Mheshimiwa Sitta alishika nafasi mbalimbali za uongozi zikiwemo Ubunge wa Urambo, Naibu Waziri wa Mawasiliano, Waziri mwenye dhamana ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma, Waziri wa Sheria, Waziri wa Ujenzi, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro na Mkuu wa Mkoa wa Iringa na kila alikopita aliacha alama zisizofutika kwa urahisi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mathalani, mwaka 1980 akiwa Waziri wa Ujenzi ndipo daraja maarufu la *Salander Bridge* la Dar es Salaam lilipojengwa chini ya uongozi wake. Vilevile ni wakati wa uongozi wake akiwa Waziri wa Ujenzi, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam ulipojengwa. (Makofi)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, mwaka 1996 Mheshimiwa Sitta aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji (*Tanzania Investment Centre*) ambapo alihudumu hadi mwaka 2005. Katika kipindi cha uongozi wake kituo hiki kilichaguliwa kuwa kituo bora cha uwekezaji Barani Afrika kutokana na uongozi wa kasi na viwango wa Marehemu Mheshimiwa Samuel John Sitta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika utumishi wake uliotukuka Mheshimiwa Sitta aliwahi kuwa Wakili wa Mahakama Kuu na akiwa anamiliki Kampuni yake ya Uwakili iitwayo *Ethical Law Chambers*.

Mheshimiwa Spika, utumishi katika siasa; akiwa mwanachama wa TANU na baadaye Chama cha Mapinduzi (CCM) mwaka 1977 Mheshimiwa Sitta alishikilia nafasi mbalimbali za uongozi zikiwemo:-

(i) Katibu Mtendaji wa CCM Mkoa wa Iringa mwaka 1987 hadi 1988;

(ii) Katibu Mtendaji wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro mwaka 1990 mpaka 1993;

(iii) Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM mwaka 2005 hadi 2010;

(iv) Mbunge wa Jimbo la Urambo na baadaye Urambo Mashariki kuanzia mwaka 1975 hadi 2015;

(v) Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi hadi alipofariki dunia tarehe 07 Novemba, 2016;

(vi) Spika wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 2005 hadi 2010 akijulikana kama Spika wa kasi na viwango (*speed and standards*) na hakika, kuta hizi za Bunge hili tukufu ni mashahidi wa kudumu; na

(vii) Waziri wa Afrika Mashariki na Waziri wa Uchukuzi mwaka 2015. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Mheshimiwa Sitta aliwahi kushika nafasi za uongozi katika Vyama vya Kibunge duniani ikiwemo:-

(i) Mjumbe wa Kamati Tendaji ya Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola (CPA); na

(ii) Makamu wa Rais na baadaye Rais wa Dunia wa Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola (CPA) mwaka 2008 hadi 2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Samuel Sitta alifariki dunia tarehe 07 Novemba, 2016 nchini Ujerumani na siku nne baadaye yaani tarehe 11, Novemba, 2016, mwili wake uliagwa rasmi ndani ya ukumbi huu wa Bunge ikiwa ni heshima ya juu kabisa kwa kiongozi huyo wa mfano na wa kuigwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya wasifu huo kwa ridhaa yako, namuomba Mke wa Marehemu Mheshimiwa Samuel John Sitta, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, asogee mbele ili umkabidhi joho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa namuomba Mheshimiwa Mama Sitta asogee mbele tuweze kumkabidhi joho kwa niaba ya Spika Mstaafu, Marehemu Mheshimiwa Samuel John Sitta. (*Makofi*)

Hapa (Mhe. Margaret S. Sitta) alipokea joho kwa niaba ya Spika Mstaafu, Marehemu Mhe. Samuel J. Sitta)

SPIKA: Sasa nimuombe Mheshimiwa Andrew Chenge - Mtemi, asome wasifu wa Spika Mstaafu, Mheshimiwa Pius Msekwa.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa heshima uliyonipatia ili niweze kusoma wasifu wa Mheshimiwa Pius Chipanda Msekwa na kabla sijasoma wasifu huo, napenda niseme kwamba nilibahatika kufanya kazi na Mheshimiwa Msekwa akiwa Naibu Spika mwaka 1993 nilipoteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na baadaye tumefanya naye kazi alipokuwa Spika kamili baada ya afya ya Mheshimiwa Mtwana Adam Mkwawa kudhoofu na baadaye kutangulia mbele ya haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nilibahatika katika uongozi wa Awamu ya Tatu, kwa wadhifa huo wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya naye kwa kipindi chote kuanzia mwaka 1995 mpaka 2005. Kwa hiyo, najisikia vizuri sana kwa nafasi hii uliyonipatia, lakini nikijumuisha kwa miaka iliyofuata kwa Spika, Marehemu kaka yangu Samuel John Sitta na baadaye Spika Anne Semamba Makinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo mtaelewa kwa nini nimekuja na gear hiyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nianze na kuzaliwa na elimu ya Mheshimiwa Pius Chipanda Msekwa; Mheshimiwa Pius Chipanda Msekwa alizaliwa katika Kijiji cha Ugombe, Wilaya ya Ukerewe tarehe 9 Juni, 1935. Alipata elimu ya msingi katika Shule ya Msingi ya Kagunguli, Ukerewe kuanzia darasa la kwanza hadi darasa la nne na baadaye Shule ya *St. Mary Seminary Nyegezi*, Mwanza ambapo Mheshimiwa Msekwa alifanya mtihani wa kitaifa uliokuwa unaitwa *territorial standard ten examination* na kufaulu vizuri, hivyo, alichaguliwa kuendelea na masomo ya darasa la 11 na 12 katika Shule ya *St. Francis College Pugu*, Dar es Salaam ambayo kwa sasa inaitwa Pugu Sekondari.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa darasa la 12 ndiyo ulikuwa mwisho wa elimu ya sekondari kwa wakati huo, baada ya hapo kulikuwa na mtihani ulioitwa *Cambridge School Certificate Examination*, Mheshimiwa Msekwa alifaulu mtihani huo na kuchaguliwa kujiunga Chuo Kikuu Kishiriki cha Makerere, Uganda ambapo alifaulu na kutunukiwa *Bachelor of Arts (Honors)* na kuhitimu masomo yake mnamo Machi, 1960.

Mheshimiwa Msekwa, muumini wa kauli ya usemi wa wahenga kwamba elimu haina mwisho, kwani baada ya kuteuliwa kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1970 akiwa na shahada moja tu ya *Bachelor of Arts*, alijiunga na chuo hicho kusomea Shahada ya Uzamili (*Master of Arts*) katika fani ya *Political Science* na *Public Administration* na kufaulu vizuri mwaka 1973.

Uzoefu wa Mheshimiwa Msekwa katika utumishi wa umma; mara baada ya kuhitimu masomo yake, Mheshimiwa Msekwa aliteuliwa kushika wadhifa wa Katibu Msaidizi wa Bunge mwaka 1960 na kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge wa kwanza Mtanzania, tarehe 9 Disemba, 1962 na wote mnaofahamu historia ya Tanzania, ndiyo ilikuwa siku ya Tanganyika kuwa Jamhuri kamili. Wadhifa huo ulimfanya pia kuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi. Katika mfumo wetu wa wakati huo Katibu wa Bunge alikuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi na Spika wa Bunge alikuwa ndio Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Aidha, Julai, 1970, Mheshimiwa Msekwa aliteuliwa kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*Vice Chancellor*) wa kwanza ambaye alifanya kazi hiyo kwa miaka saba mfululizo hadi mwaka 1977.

Miongoni mwa shughuli nyingine alizowahi kuzifanya ni pamoja na zifuatazo:-

Mheshimiwa Msekwa aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Taratibu za Utoaji Haki Nchini (*The Judicial System Review Commission*) iliyojulikana kama Tume ya Msekwa mwaka 1974. Aliwahi pia kuwa Mwenyekiti wa kwanza wa Baraza la Mitihani la Taifa. Vilevile Mheshimiwa Msekwa aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume ya Nyalali iliyopendekeza Mfumo wa Vyama Vingi nchini mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Msekwa aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi mwaka 1975 na kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Tume hiyo hadi mwaka 1980. Aidha, Mheshimiwa Msekwa aliteuliwa kuongoza Mashirika ya Umma mbalimbali kama Mwenyekiti wa Bodi zake. Mashirika hayo ni yafuatayo; Chuo cha Ushirika Moshi, Chuo cha Wanyamapori (*College of African Wildlife Management*) - Mweka, Moshi; Chuo cha Mipango, Dodoma; Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Arusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uzoefu katika Serikali; Mheshimiwa Msekwa aliteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mikoa ya Tabora na baadaye Kilimanjaro kuanzia mwaka 1980 hadi 1984. Baada ya hapo aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu hadi mwaka 1989 alipoteuliwa kuwa Kamishna wa Tume ya Mipango ambayo ilikuwa chini ya Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uzoefu katika chama; Mheshimiwa Msekwa alijiunga na Chama cha Mapinduzi tarehe 01 Aprili, 1977, kadi namba 000003, Tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Wilaya ya Kinondoni, Mkoani Dar es Salaam. Aidha, baada ya kutangazwa Azimio la Arusha aliteuliwa kuwa Katibu Mtendaji Mkuu wa TANU kuanzia mwaka 1967 hadi mwaka 1970. Vilevile aliteuliwa kuwa Katibu Mtendaji Mkuu wa CCM wa kwanza kuanzia mwaka 1977 hadi mwaka 1980.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya hapo Mheshimiwa Msekwa aliteuliwa kuwa Katibu wa Tume ya watu 20 ya kuandaa Katiba ya Chama kipya cha CCM mwaka 1977 na amewahi kuwa Makamu Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi Bara mwaka 2007 hadi 2012. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uzoefu katika masuala ya Kibunge; kama nilivyogusia awali, Mheshimiwa Msekwa amewahi kufanya kazi kama Katibu wa Bunge Msaidizi kuanzia mwaka 1960 na Katibu wa Bunge kuanzia mwaka 1962 hadi mwaka 1970. Aidha, Mheshimiwa Msekwa aliteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mikoa ya Tabora na Kilimanjaro wadhifa ambao ulimpa fursa ya kuwa Mbunge kuanzia mwaka 1980 kwa kuwa wakati huo Wakuu wa Mikoa walikuwa Wabunge kutokana na wadhifa wao huo. Akiwa Mbunge Mheshimiwa Msekwa alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Wabunge ya Kurekebisha Kanuni za Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Pius Msekwa alikuwa Naibu Spika wa Bunge akitokana na Jimbo la Ukerewe kuanzia mwaka 1990 hadi mwaka 1994. Aidha, amekuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha miaka 11 mfululizo kuanzia Aprili, 1994 hadi Disemba, 2005. Vilevile akiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa Mjumbe

wa Kamati ya Utendaji ya Umoja wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Parliamentary Association*) tangu mwaka 1996 hadi mwaka 1999 ambapo alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu. Aidha, Mheshimiwa Msekwa amekuwa mwandishi nguli wa vitabu na majarida mbalimbali kuhusiana na masuala ya Bunge, siasa na jamii kwa ujumla kwa muda mrefu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baadhi ya vitabu vilivyoandikwa na Mheshimiwa Pius Msekwa kwa kutaja vichache tu ni hivi vifuatavyo:-

The Transition to Multi-Partism in Tanzania; Reflections on the First Multi-Party Parliament 1995 – 2000; Bunge la Kwanza katika Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa Tanzania 1995 – 2000; Reflections on the First Decade of Multi-party Politics in Tanzania; Uongozi na Utawala wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere; Nafasi ya Kamati za Bunge katika Uendeshaji wa Shughuli za Bunge; Mpango wa Elimu kwa Umma kuhusu Bunge; Mahusiano baina ya Bunge na Wananchi, Serikali na Mahakama, kwa mujibu wa Katiba ya Nchi; Maadili na Uwajibikaji wa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilichotoka mwaka 1995; Nafasi ya Bunge katika Uongozi wa Nchi; A Handbook ambayo tunaitumia Wabunge, A Handbook for New Members of Parliament, 2003; Ten Years after the Transition to Multipartism 2005; Parliament Privileges in Tanzania cha mwaka 1995; na vingine vingi, orodha ni ndefu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, huyo ndiyo, Pius Chipanda Msekwa na wote mnaofuatilia shughuli zake kwenye *Daily News* kila siku ya Alhamisi kuna mambo makubwa kusaidia jamii yetu ya Tanzania. Ningeweza kusema mengi, lakini dibaji yangu ilikuwa imebeba yote ambayo nilikusudia kuyasema na pia niweke akiba. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Mheshimiwa Spika ni Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na anaishi Ukerewe Mkoani Mwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya wasifu huo na kwa ridhaa yako, namwomba Mheshimiwa Pius Chipanda Msekwa ajongee mbele ili umkabidhi joho lake na kumvalisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Chenge. Nakuomba Mheshimiwa Msekwa sasa sogege hapo mbele. (Makofi/Vigelegele)

Hapa Spika Mstaafu (Mheshimiwa Pius Chipanda Msekwa) Alivalishwa Joho

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, baada ya zoezi hili natumai mna hamu kabisa ya kuwasikia wazee wetu hawa wakitupa salamu zao, kwa sababu ya muda tumewapangia dakika 15 kila mmoja, karibuni sasa, nadhani tuanze na Mama Makinda, halafu anafuata Mama Margaret Sitta na atamalizia Mzee Pius Msekwa. Mheshimiwa Mama Makinda karibu sana kwenye *microphone*, karibu uongee nasi, karibu sana. (Makofi/Vigelegele)

MHE. ANNE S. MAKINDA - SPIKA MSTAAFU: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa wageni wote waalikwa na Mheshimiwa Spika Mstaafu Mzee Pius Msekwa na ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa kitendo cha kutualika sisi na kututaka tuweze kupewa heshima hii ya kuwa na mavazi ambayo tuliyavaa tukiwa ndani ya jengo hili ni cha kipekee sana, ni cha kipekee na Bunge letu nadhani ni la kihistoria, jambo ambalo sisi wenyewe mimi binafsi siwezi hata kulieleza ukuu wake. (Makofi)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru sana kwa ubunifu huu wewe mwenyewe pamoja na Kamati yako ambapo umeweka sisi wastaafu tuwe karibu na mahali ambapo wengine wetu tulifanya kazi maisha yetu yote. Kwa sababu hiyo, mimi nilipoingia Bungeni mwaka 1975 nilikuwa kijana peke yangu humu ndani, kijana kweli maana yake nilikuwa tu nimemaliza Mzumbe, hata kazi yenyewe mimi niliyosomea sikufanya, nilifanya kazi ya humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hata namna nilivyoingia nilijiona sistahili, nilijiona kabisa sistahili maana wote walikuwa watu wazima hata sijui nilikuwa nivae nini, hata nifanye nini, lakini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nilipewa busara kwamba kwa sababu mimi ni mdogo, kazi ya kwanza nijifunze hawa watu humu ndani wanafanya vitu gani, huwezi kuamini hata Ofisi ya Bunge yenyewe nilikuwa sijui, nilikuja kuijua wakati nagombea. *(Makofi)*

Kwa hiyo kazi ya kwanza nilipochaguliwa na tuligombania na watu wazima sana na watu wakawa wananiambia wewe bwana hata usipopata leo si bado wewe kijana na mimi nikasema ndiyo, lakini mimi nikawa-*surprise* nikapita uchaguzi, hata nguo ya kuvaa ili kuapishwa mle Bungeni nilikuwa sina, mimi nilikuwa navaa suruali. Kwa hiyo nikaamka kuna *classmate* wangu mle nikamfuata usiku ule kwamba wewe nitengenezee nguo kesho nataka kuvaa, naapishwa kesho Mheshimiwa mimi. Kwa hiyo, nilivyofika humu miezi sita nilikaa kwenye kiti sikuuliza swali, sikuonesha kidole, nilikuwa najifunza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilipitia vitabu vyote ninavyovijua Bungeni kwamba hiki kinasema nini, wanafanya nini kila kitu, kweli miezi sita sikusimama, lakini nilikuwa Mjumbe wa Kamati *Public Accounts Committee*, sasa ni *auditor* nilikuwa pale. Kwa hiyo, tulifanya kazi sana kwa lengo la kubadilisha mazingira ya nchi yetu, wakati ule ndiyo baada ya muda *decentralization* ndiyo ilikuwa imefanyika. Kwa hiyo, waliopelekwa kuwa *accountants* huko mikoani, wengi walikuwa hawakwenda shule. Kwa hiyo, ilibidi tutengeneze utaratibu ambao unawawezesha wale waweze kuandika vitabu vikiwa vizuri bila kuwa wana *qualification* zinazohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *point* ambayo najaribu kusema ni kwamba Bunge kama hili la kwetu asilimia kubwa ni vijana tena vijana kweli, sasa ukisema yanayotokea mengine kwa sababu vijana nakataa kwa sababu mimi nilishakuwa kijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kubwa ambalo nafikiri ni muhimu sana kwa wale mlioko vijana na wanaokuja kujifunza kwa walioanza, watu wazima inakufanya wewe uwe bora zaidi na makini zaidi kwa sababu utachukua vya wale wazee, lakini wewe ni kijana utakwenda hatua nyingi zaidi na kuwa bora zaidi kuliko hata wale wazee. *(Makofi)*

Sasa hili nilifikiri ni somo ambalo Waheshimiwa Wabunge vijana bado Taifa linawaangalia, linawategemea, lakini mtafanikiwa sana mkijifunza kwa hawa wazee, halafu mkatengeneza na ya kwenu ya sasa, kwa hiyo, mkichanganya hiyo *combination*, lazima mtakuwa Wabunge bora sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya kwamba tunazungumza wakati saa 12 zimeshafika, lakini hiyo siyo hoja, maana yake wote mtarudi na mkirudi, naamini wote mtarudi na mtaweza kilitumikia Taifa letu kwa werevu ambao mmeupata sasa na mtakaoupata katika maeneo yenu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sifa moja ya Mbunge yeyote, awe Mbunge yeyote yule, hakuna mtu mnyenyekevu sana sana kwa wananchi kama Mbunge na ninyi mnajua hilo na hiyo inatupa uhuru wa wananchi kuku-*approach* wewe Mbunge, Mbunge yeyote ambaye siyo mnyenyekevu kwa wananchi wake huyu ni Mbunge wa mashaka, lakini hilo naamini

mnalifahamu na sababu ya unyenyekevu ni kusudi wawe huru na wewe, waweze kukwambia mambo yao na wewe uweze kuyafikisha hapa mahali ambapo mnatunga sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Waheshimiwa sisi, tulifanya kazi, mimi nilifanya kazi na Mzee Msekwa alipokuwa Naibu Spika mimi nilikuwemo humu ndani, alipokuwa Spika mimi Mwenyekiti wa Bunge mpaka nikawa Naibu Spika pale nilikuwa tena kwa Mheshimiwa Marehemu Samuel Sitta baadaye na mimi mwenyewe nikawa Spika. Kwa hiyo, kikubwa ninachopenda kusema na sipendi nizungumze zaidi kwa sababu kuna *dictionary* hapa na *encyclopedia* iko hapa dakika zangu nataka achukue yeye, kwamba tujifunze, kujifunza hakuna mwisho. (Makofi)

Wabunge wote duniani kote hata mkiona wanapigana ndani ya Bunge lakini uzalendo kwa nchi yao ni mkubwa sana, yaani hiyo wewe nenda mahali popote, Mbunge yoyote utakayekutana msemee vibaya nchini kwake, mtapigana huko huku. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo suala la uzalendo linaloombwa kila siku, jamani siyo hiyari, kama wewe ni Mtanzania uzalendo unakuwa ni *number one* kwa sababu ni nchi yako, ni nyumbani kwako, utakaa wewe, watakaa kizazi kinachokuja na nchi yako. Kwa hiyo, uzalendo katika nchi yako ukiwa Mbunge uwe mfano na watu wengine waweze kuona kwamba huyu ni kitu cha maana. Huwezi kama Mbunge kukaa mahali pengine ukaanza kuzungumza nchi yako vibaya kwa mtu mwingine, hata wanaokusikiliza hawakusifu bali wanakudharau. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, angalieni nchi kubwa kama Marekani, huwezi kukuta Mmarekani anazungumza nchi yake hovyoyote, hata akiwa Mmarekani mweusi, hata akiwa Mmarekani mzungu, hawazungumzi nchi zao hovyoyote mahali popote, mliowahi kufanya kazi na Mmarekani mtakuwa mnajua hiyo sifa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo na sisi kama tukitaka kujenga nchi hii uzalendo lazima uwe kitu cha kwanza kwa sababu nchi hii ni ya kwetu sisi wote, tofauti zetu za kiitikadi zisitugawe, sisi ni Watanzania, hata kuwa na vyama vingi kama anavyosema ilianzishwa na Bunge hili ni sheria, siyo kwamba ni hiari ni sheria kuwa na vyama vingi, ni sheria tuliyopitisha wenyewe hapa. Tena kuna kitu kimoja *Chief Chenge* hakusema, mara ya kwanza Bunge linaanza hapa na Vyama Vingi tulijiwekea kwenye kanuni zetu *threshold* iwe asilimia 26, ndiyo vyama vitambulike kama ni rasmi. Tulipoingia hapa hawakufika ile *threshold*, ni wakati wa kipindi cha Mzee Msekwa ndipo tulibadili ile kanuni humu humu ndani *threshold* ndiyo ikawa kumi na mbili na nusu (12.5) ndiyo ikawa *threshold* angalau kuwa-*accommodate* wale walioweza kuingia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuwa na vyama vingi jamani ni mfumo tu wa kuweza kuendesha nchi, siyo kwamba ni uhasama au ni kitu chochote, ni lazima wote tupendane huku na huku na ndivyo tutakavyoweza kujenga nchi yetu. Nataka muda wangu mwingi nimuachie mzee wangu Msekwa mimi nimekaa naye miaka yote ni *mentor* wa kwangu na mtu ambaye nilikuwa nam-*admire* sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka nitumie muda huu kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuweza kutusikiliza, kutusindikiza, kutupa heshima kwa kweli tunashukuru sana, tunachoweza kufanya ni kuwatakieni kheri mnakokwenda kila mmoja wenu Mwenyezi Mungu amuone kila alichochangia katika kipindi hiki amrudishie kile kinachostahili. Nawatakieni kheri. Ahsanteni sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ahsante. (Makofi/Vigelele)

SPIKA: Tunakushukuru sana Mama Makinda, umetukumbusha kwamba kwa kweli ni muhimu sana Katibu wa Bunge u-take note wakati wa *orientation* ya Bunge jipya hilo la Kumi na Mbili ipo haja ya kuwaita wazee wetu hawa kuzungumza na Wabunge wapya. (Makofi)

Mama amegusa kwamba ni muhimu sana kwa Wabunge kujifunza bila kuchoka, kwa mfano nilivyotajiwa vitabu vya mzee Msekwa vingi sana hapa ishirini na kitu, vyote viko Maktaba pale, ni wangapi tumewahi kuvipitia, ukipitia vitabu vile unakuwa Mbunge mahiri kabisa.

Pia mama amegusia eneo la unyeyekevu, jambo ambalo tumepambana nalo kwa miaka mitano hii. Mbunge usipokuwa mnyenyekevu wewe siyo Mbunge, baadhi yetu walifikiri ukiingia hapa ni ubabe na maneno ya ajabu na nini, tulikuwa tukiambiana hapa jamani ndiyo hili mama anatuambia, usipokuwa mnyenyekevu kwa wananchi hivi wakupigie kura wewe nani? Kwa sababu ipi hasa? Ndiyo maana watu wamekaa miaka 40, siri ndiyo hiyo, unyenyekavu na kama wewe mnyenyekevu kwa wananchi, utakuwa mkorofi kwa Spika au watu wengine, haiwezekani! Ukishaweza kunyenyekea walio wadogo basi utanyenyekea kila aliyebaki.

Pia ametuambia suala la uzalendo, kwa nchi yetu tusemane humu humu ndani, piga sana ndani ya Bunge si Katiba inakuruhusu lakini tukivuka tu mpaka wa Nchi lazima sote kwa pampja tuiseme vizuri Tanzania. (Makofi)

Maana huwezi kuwa nchini hapa unaimba Tanzania, Tanzania, nchi yangu ni nzuri sana, ukivuka mpaka unasema tofauti, haiwezekani. Kwa hiyo, uzalendo ni muhimu sana sana na mengine yote ambayo ametuambia na ametukumbusha kwamba *threshold* ya upinzani hapa Bungeni ili kuunda Kambi ya Upinzani ni asilimia 12.5 sasa hii mwaka 2020 huenda *threshold* hiyo haitapatikana sijui itakuaje. Hiyo nimechomekea tu. Itabidi tutengeneze Kanuni ambazo hazina Kambi ya Upinzani. Hiyo nimechomekea mimi. (Kicheko)

Tunakushukuru sana Mama Makinda, *actually* kwenye Mabunge ya wenzetu na hasa kule ilikoanzia kule huko, walikuwa wanapewa siyo joho tu, walikuwa wanapewa na Kiti chake alichokuwa anakitumia kama Spika anakwenda nacho nyumbani kama kumbukumbu yake ndiyo ilivyokuwa hasa. Lakini sisi tumeanza na hi kwa sababu tumesita kidogo, lakini Kiti cha Mzee Msekwa kipo, Kiti cha Marehemu Sitta kipo, Kiti cha Mama Makinda kipo na hiki mnachokiona hiki, hiki changu hawakukalia hawa wazee, kiko tofauti. Kwa hiyo, mkija kuona baadae niende nacho Kongwa nitashukuru kweli. Ahsante. (Kicheko/Makofi)

Kwa hatua hiyo sasa nimuite Mheshimiwa Mbunge mwenzetu, Margaret Sitta azungumze kwa niaba ya Mzee wetu Samuel Sitta. Mama Sitta karibu sana. (Makofi)

MHE. MARGARET S. SITTA - K.n.y. SPIKA MSTAAFU MAREHEMU SAMUEL J. SITTA: Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba kwa heshima na taadhima, kabla sijasoma yale niliyoandika kama neno la shukrani, kwa heshima uniruhusu kwa kuwa jambo hili ni zuri, la heshima, lakini pia linagusa hisia, wako wenzetu waliotusindikiza sisi kama familia, kwa ruhusa yako naomba nitambue uwepo wa watu wa Tabora na Urambo ambao wamejumuika nasi siku ya leo ambao wako hapa, kwa heshima na taadhima naomba uwaruhusu wasimame. (Makofi)

SPIKA: Naomba msimame wale mliotoka Tabora na Urambo tuwaone. Karibuni sana sana, karibu sana, sana, sana, karibuni sana, karibuni.

MHE. MARGARET S. SITTA - K.n.y. SPIKA MSTAAFU MAREHEMU SAMUEL J. SITTA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nakushukuru ulitambua kiongozi wa msafara ambae ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Hassan Mwakasule. Ahsante sana.

Mheshimiwa Job Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Maspika Wastaafu, Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge, Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri mliopo, Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Waheshimiwa wageni waalikwa wote mliopo akiwepo pia Kiongozi wetu wa Chama Cha Mapinduzi, Waheshimiwa wageni waalikwa wote Mabibi na Mabwana, *Asalaam Aleykum!*

WABUNGE FULANI: *Waaleykum Salaam.*

MHE. MARGARET S. SITTA - K.n.y. SPIKA MSTAAFU MAREHEMU SAMUEL J. SITTA: Bwana Yesu asifiwe.

WABUNGE FULANI: Amen.

MHE. MARGARET S. SITTA - K.n.y. SPIKA MSTAAFU MAREHEMU SAMUEL J. SITTA: Mheshimiwa Spika, Rais wa zamani wa Marekani, Abraham Lincoln aliwahi kusema kuwa "kila mwanadamu anayo fursa ya kuacha historia ya kutukuka iwe kwenye ngazi ya familia, iwe kwenye ngazi ya taasisi hata ngazi ya Taifa kwa ujumla ilimradi aongozwe na maono, ujasiri na imani ya kile anachokisimamia." Mwisho wa nukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo cha asubuhi hii ya leo cha Bunge lako tukufu kukabidhi majoho kwa Maspika Wastaafu siyo tu ni cha kihistoria ndani na nje ya Bunge hili bali ni ushahidi wa dhati wa dhamira yako ya kusimamia na kutekeleza kwa vitendo yale unayoyaamini. Kwa niaba ya familia ya Marehemu Mheshimiwa Samuel John Sitta na Spika Mstaafu tuna kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa kutufikisha siku ya leo tukiwa wenye nguvu na afya kushuhudia tendo hili kubwa la kihistoria kwa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kupokea Joho la Uspika kama ishara ya kuwaenzi viongozi walioshika nafasi ya Uspika waliohai na waliotangulia mbele za haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee jambo hili la kuanzisha utaratibu huu tunakushukuru sana na tunaomba upokee shukrani zetu za dhati na Mwenyezi Mungu akubariki pamoja na wale wote viongozi na watendaji mlioshirikiana nao katika kuanzisha na kufanikisha tukio hili la kihistoria. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile chini ya uongizi wako, Bunge letu hili lenye Wabunge hawa tunaowaona siku ya leo lilichukua uamuzi wa kihistoria wa kuingiza Bungeni mwili wa marehemu Mheshimiwa Samuel John Sitta na Spika Mstaafu jambo ambalo familia na wananchi wa Urambo na Mkoa wa Tabora kwa ujumla hawatalisahau. Hakika mlitupa heshima kubwa na kwa hiyo tunaomba tena upokee shukrani zetu za dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuishukuru sana Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa jinsi ilivyoshirikiana na Bunge kwa kufanikisha matibabu, kwa kuendeleza matibabu na hatimae mazishi ya kihistoria ya Marehemu Mheshimiwa Samuel John Sitta yaliyofanyika Wilayani Urambo sehemu ambayo wananchi kwa upendo wao walimchangua kuwa Mbunge na kumuwezesha kuwa Spika wa Bunge na katika tukio hili kama nilivyosema hapo awali tunao wawakilishi wa Wananchi wa Urambo na Mkoa wa

Tabora kwa ujumla. Nichukue nafasi hii pia kukishukuru Chama cha Mapinduzi ambacho ndicho kilimpa nafasi ya kugombea Ubunge na hatimae kuwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Marehemu Samuel John Sitta, Mbunge na Spika Mstaafu ambaye joho lake kwa heshima kubwa nimelipokea asubuhi hii kwa niaba ya familia alitumia muda wake mwingi wa utumishi wa umma kwenye siasa. Aidha, alifikia kilele cha utumishi wake kwenye siasa alipochaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Novemba, 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alipokuwa Spika, Mheshimiwa Samuel Sitta marehemu aliongoza Taasisi hii kwa falsafa ya viwango na kasi yaani *speed and standards* kwa kuzingatia misingi ya uwajibikaji, uhuru na haki. Falsafa hii ndiyo iliyokuwa dira na mwongozo wake katika utekelezaji wa majukumu na kazi zake na alipata nafasi ya kushika nafasi mbalimbali akiwa mtumishi wa Serikali na hatimaye kama nilivyotaja kuwa kiongozi wa kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru wafanyakazi wote aliofanya nao kazi katika Taasisi mbalimbali, Wizara, Mikoa wakiwepo pia wafanyakazi wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo Joho hili ambalo tumekabidhiwa leo daima litaendelea kuwa ni ukumbusho wa misingi ambayo aliisimamia marehemu ambayo ni pamoja na uadilifu, kusema ukweli, kuzingatia haki, ujasiri na kufanya kazi kwa viwango na kasi yaani *speed and standards* na kuwa na ngozi ngumu hasa katika masuala ya kisiasa. Haya kwetu sisi ndiyo mambo ya msingi ambayo tutaendelea kuyaenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia; kwa niaba ya familia ya Marehemu Mheshimiwa Samuel John Sitta naomba tena kukushukuru kwa tukio hili la heshima. Aidha, tunawashukuru wote walioshiriki katika kufanikisha tukio hili la kihistoria na kwa wale waliotusindikiza tunasema tena ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu Samuel John Sitta mahali pema peponi, Amen. *(Makofi)*

Mungu libariki Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mungu ibariki Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mungu ibariki nchi yetu ya Tanzania, ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mama Sitta, ahsante sana tunakushukuru sana, ahsante sana kwa hotuba yako ambayo pia ni hotuba ya familia. Sasa nimkaribishe Spika Mstaafu Mheshimiwa Pius Msekwa aweze kuongea nasi. Mheshimiwa Msekwa karibu sana, karibu uongee nasi, karibu Mzee wetu, karibu sana. *(Makofi)*

MHE. PIUS C. MSEKWA - SPIKA MSTAAFU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ahsante sana Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri na kama walivyotangulia kusema wenzangu na mimi pia natambua heshima kubwa tuliyopewa siku ya leo ya kuruhusiwa kusimama mbele yako na mbele yenu Waheshimiwa Wabunge tukiwa ndani ya ukumbi wenyewe kwa sababu tunajua kwamba ni marufuku kwa mtu yoyote kuingia humu ndani kama hajaapishwa kuwa Mbunge au kama siyo mtumishi wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakushukuru na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kutupatia kibali siku ya leo kwa azimio mlilolipitisha mapema na kutengua Kanuni na

kutuwezesha na sisi kuingia humu ndani ili tuweze kuwasalimia tukiwa hapa ndani, tunashukuru sana. (Makofi)

Naomba pia nitoe shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai pamoja na afya njema ya mwili na akili iliyoniwezesha kuhudhuria na kushiriki katika tukio hili maalum la kukabidhiwa na la kihistoria. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na waliokusaidia lakini kwa hakika tukio hili ni ubunifu binafsi wako. Sisi wenzako tuliokutangulia hatukuwahi kufikiria jambo zuri kama hili ndiyo sababu leo linafanyika kwa mara ya kwanza kabisa katika historia ya Bunge letu na historia ya nchi yetu. Kwa hiyo, natoa shukrani maalum kwako pamoja na pongezi nyingi kwa jinsi ulivyosimamia, siyo tu ulivyolibuni wazo lenyewe, lakini vilevile ulivyosimamia utekelezaji wake wewe mwenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo nashukuru pia kwa ukarimu wako uliotuwezesha mimi pamoja na Mke wangu Mama Anna Abdallah kuhudhuria na kushiriki ipasavyo katika tukio hili la kihistoria. Naendelea kusema ahsante sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini umegusia jambo kwamba mimi ndiyo wa kwanza kulivaa joho la namna ambalo linatumika sasa Bungeni. Ni kweli kabisa, kumbukumbu zako ni kweli kabisa kwamba Spika mzalendo wa kwanza wa Bunge letu, Chifu Adam Sapi Mkwawa alikuwa yeye havai joho la namna tunayoiona leo, yeye alikuwa anatumia mavazoi rasmi ya Chifu wa Wahehe kwa sababu yeye mwenyewe alikuwa ni Chifu wa Wahehe, sasa sisi wengine tusiokuwa Machifu wa Wahehe tusingeweza kuvaa mavazi hayo so ilibidi utumike utaratibu wa kutafuta Joho Rasmi la Spika kwa kuzingatia kama Mabunge mengine mengi duniani hata la kwetu wakati wa ukoloni kulikuwa na Joho la Spika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulichotakiwa kufanya ni kubuni joho linalolingana na mazingira ya Tanganyika huru wakati ule na baadaye Tanzania ili tuondokane na majoho yenye mazingira ya kikoloni ndiyo tukabuni. Kilichotokea ni kwamba iliundwa Kamati Maalum ambayo kiongozi wake alikuwa ni Mheshimiwa Marehemu Samuel Sitta na kwa kushirikiana na Spika niliyekuwepo wakati ule ndiyo waliobuni joho hili tukafikiria tuweke mazao makuu ya Tanzania, tuko katika ile jeuri ya kutaka tuwe na joho la Kitanzania tukaweka korosho na mengine kama unavyoyajua, lakini ni sahihi kabisa kumbukumbu zako kwamba historia ya joho hili imeanza na mimi na naendelea kutoa shukrani kwamba joho ulilonikabidhi leo ndiyo *original*, lenyewe. Nitalitunza kwa heshima kama ulivyokusudia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa hiyo imenipa furaha sana kwamba historia imeanza na mimi na sasa nawasilimia Waheshimiwa Wabunge nikiwa nimevaa joho *original* na ndiyo lenyewe limeli-check nimeona hali yake. Kwa hiyo, ili ku-share furaha hiyo pamoja na wasikilizaji wangu waliopo ndani na nje ya Bunge naomba sasa nitamke basi, nitoe kauli ya kulipokea. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, sasa natamka rasmi tena kwa furaha na bashasha kwamba naipokea zawadi hii kwa heshima kubwa, zawadi ya joho *original* la Spika ambalo nilibahatika kulivaa kwa kipindi kirefu cha zaidi kidogo ya miaka 10 nilipokuwa katika wadhifa huo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya tamko hilo sasa niendeleo kutoa shukrani zangu kama ilivyo ada ninapopewa fursa kubwa kama hii. Naishukuru Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kunitunza vizuri katika maisha yangu ya ustaafu kwa njia ya malipo pensheni stahiki, nono pamoja na mafao mengine kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ya Pensheni kwa Viongozi Wastaafu wa Kitaifa. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, baada ya shukrani hizo naomba sasa nijitambulisha zaidi, namshukuru Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge kwa kuchambuaachambua uongozi wangu wa siku za nyuma, historia ya maisha yangu katika uongozi wa nchi hii na kama alivyoeleza hivi punde.

Mheshimiwa Spika, nyongeza ndogo tu, ni kama alivyoosema kwamba baada ya kustaafu nyadhifa zote za uongozi na ya mwisho kabisa ilikuwa ni Makamu Mwenyekiti wa ngazi ya Taifa wa Chama cha Mapinduzi, basi nilihamisha makazi ya familia yangu kwenda kwetu Ukerewe, kulingana na msemo maarufu wa Kiswahili kwamba mtu kwao, si hilo tu na vilevile kwa kufuata nyayo za Kiongozi Mkuu wa nchi hii, Mwalimu Julius Nyerere, aliamua kuhamia kwao Butiama baada ya kustaafu wadhifa wa Rais wa nchi hii kwa miaka mingi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, basi nikiwa huko Ukerewe shughuli zangu kama alivyoeleza Mheshimiwa Mtemi Chenge, shughuli yangu kubwa sasa hivi ni uandishi wa vitabu na amevitaja, lakini cha hivi karibuni kabisa ambacho nadhani hakijaingia kwenye orodha ya vitabu vilivyopo katika *library* yako kinaitwa Ni Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Kimechapishwa mwishoni tu mwa mwaka jana na kuingia sokoni, kimechapishwa na *Tanzania Education of Publishers* wako Bukoba hawa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile naendelea kuandika na makala alizozitaja Mheshimiwa Chenge zinazotoka katika Gazeti la *Daily News* kila Alhamisi, lakini kwa kufuatiwa wito uliotolewa na Mheshimiwa Rais Magufuli mwishoni mwa mwaka jana alipokuwa anazindua kitabu cha Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa alitoa wito kwa viongozi wote waliopo madarakani hivi sasa na waliokwisha kustaafu kwamba wajitahidi kuiga mfano wa Rais Mstaafu Mheshimiwa Mkapa kwa kuandika vitabu vya historia za maisha yao katika uongozi na mimi tayari nimeshaitika wito huo na tayari nimekwishaanza kuandika kitabu cha historia yangu katika uongozi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, natarajia kwamba uongozi wangu katika Bunge hili utachukua sehemu kubwa zaidi katika kitabu hicho kwa sababu ninazo kumbukumbu nyingi sana kwa kipindi hicho nilichokuwa Spika wa Bunge hili ambavyo baadhi yake tayari nilikwishakuziandika katika kitabu kilichotangulia kinaitwa *The Story of the Tanzania Parliament* kilichapishwa mwaka wa 2012. (Makofi)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge natambua kwamba muda niliopangiwa ni dakika zisizozidi 15 za kuwasalimieni, kwa hiyo basi, nikiwa katika hali hiyo ya furaha na bashasha kutokana na zawadi kubwa hii niliyokabidhiwa na pia kwa lengo la kuwashirikisha furaha hiyo wenzangu, pamoja na kuchangamsha kidogo kwa mazingira ya tukio hili naomba nitumie fursa ya salamu zangu hizi kwa kutoa simulizi chache nyepesi nyepesi, lakini zinahusu mambo ya Bunge. Inawezekana kwamba baadhi ya wasikilizaji wangu watakuwa wanazisikia habari hizi kwa mara ya kwanza na kwa hiyo, zitakuwa habari mpya kwao, lakini zinazoeleza mambo ambayo labda walikuwa hawayafahamu vizuri itakuwa ni jambo jema likitokea hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, habari nyepesi nyepesi ya kwanza, ni simulizi kuhusu chanzo cha Kanuni ya Bunge letu inayokutaka wewe Spika na Spika yeyote mwingine kila anapompa Mbunge nafasi ya kuchangia Bungeni au kuuliza swali, kila Spika anapofanya hivyo analazimika kumtaja Mheshimiwa huyo kwa majina yake au kama Mbunge ni Waziri basi kwa wadhifa wake wa Uwaziri, tunayo Kanuni hiyo chanzo chake ni nini, hadithi njoo. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, chanzo chake si kingine bali ni ulemavu wa Spika mmojawapo wa zamani wa Uingereza la *House of Commons*. Kilichotokea ni kwamba wakati fulani wa zamani

kulikuwa na Spika mmoja huko Bunge la Uingereza aliyekuwa na tatizo na uhafifu wa kuona, Wakerewe wangesema alikuwa na malienge, sijui na Kiswahili ni malienge vilevile. Basi siku moja wakati wa kikao cha Bunge kinaendelea kama kawaida na kama ilivyokuwa imezoeleka katika Bunge siku za nyuma alielekeza macho yake kwa Mheshimiwa Mbunge aliyetaka kumpa nafasi ya kusema, sasa kwa mshangao wake na wengine wengi waliokuwepo wakasimama Waheshimiwa Wabunge wawili kwa pamoja wote wakidai kwamba jicho la Spika liliwaona. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, sasa basi kutokana na tafrani hiyo ndipo ikatengenezwa Kanuni inayomlazimisha Spika amuite kwa majina yake yule Mbunge anayempa nafasi ya kusema au kuuliza swali, hiyo moja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, habari nyingine nyepesi nyepesi...

SPIKA: Kabla Mzee hajaendelea na habari ya pili nyepesi, hii ikitokea Mbunge ana malienge akafikiri Spika anamuangalia yeye kumbe sio yeye. Mheshimiwa Spika endelea. (Kicheko)

MHE. PIUS C. MSEKWA - SPIKA MSTAAFU: Mheshimiwa Spika, nyingine ni simulizi ya kutaka kutoa ufafanuzi tu kwa nini kila Mkutano wa Bunge letu unaanza siku ya Jumanne na Bunge hili Mkutano huu umeanza leo Jumanne, sasa kwa nini maelezo yake ni kwamba kila Bunge duniani kote linazo mila zake na desturi zake, sasa miongoni mwa mila na desturi za Bunge la Tanzania ni mila hiyo ya kuanza mikutano yetu yote ya Bunge ikiwa siku ya Jumanne, ndio sababu Mheshimiwa Kiongozi wa Shughuli za Bunge anaposimama kutoa hoja ya kuahirisha Mkutano wa Bunge lolote lile anataja tarehe ya Mkutano utakaofuata ambayo inaangukia siku ya Jumanne.

Mheshimiwa Spika, jambo halipo kwenye Kanuni wala haliko kwenye sheria yoyote ya Bunge, ni mila tu na desturi ambayo tumeamua kuiendeleza tangu ilipoanzishwa katika Bunge letu hata kabla ya uhuru, hata Bunge la wakati wa ukoloni ile lilikuwa linaitwa LEGCO nalo lilikuwa linaanza siku za Jumanne, basi ni utekelezaji tu kwamba tunaendelea kufanya hivyo, si sheria, si Kanuni ni utekelezaji tu wa mila na desturi za Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niende kwenye habari nyepesi nyingine zinazomhusu Mheshimiwa Spika, sio Spika wewe, lakini Spika yeyote yule wa Bunge. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, habari hizo ni kwamba huyu kiongozi wa Bunge anayelitwa Spika huwa anakabiliwa na mizigo mizito isiyoonkana machoni pa watu ambayo kwa lugha ya Kiingereza inaitwa *Speaker's Burdens* kwa Kiswahili ni mizigo mizito inayomwelelea Spika au kiongozi yoyote Naibu Spika au Mwenyekiti anapokaa kwenye kiti hicho akiongoza shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa muonekano wa kawaida Waheshimiwa, Mheshimiwa Spika mwenyewe akiwa yupo pale au hata kiongozi mwingine yupo huwa wanaonekana kuwa wametulia vilivyo na hawana wasiwasi, lakini kumbe kwa ndani huwa kuna kitu kinachowatesa ambacho ndio hiyo mizigo inayowaelelea wakati huo. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishagusia hivi punde, mimi mwenyewe nilibahatika kukalia kiti hicho kwa miaka zaidi ya 10, kwa kweli ni miaka 15 tukijumlisha pamoja na ile miaka ya nilipokuwa Naibu Spika, lakini nilikuwa nakitalia kwa muda mrefu kwa sababu Spika

mwenyewe hali yake ya afya ilikuwa hairuhusu kukaa kwa muda mrefu, kwa hiyo unapata kama jumla ya miaka 15 hivi. Kwa hiyo, ninazo kumbukumbu nzuri za mizigo hiyo kwani imenikuta mimi mwenyewe, nafahamu uzito wake.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kifupi mizigo yenyewe tunaweza kuiita ni pacha, yaani ni miwili kwa pamoja, sasa kulwa wa mapacha wetu ni wajibu wa Spika wa kulinda heshima ya kiti cha Spika na doto ni wajibu wake wa kulinda heshima ya taasisi nzima ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuanze na ile na kulwa kulinda wajibu wa Spika wa kulinda heshima ya kiti cha Bunge. Uzito wa mzigo huu unatokana na kuzingatia kwamba Spika au Kiongozi yeyote mwingine anayekaa kwenye kiti hicho ili aweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi analazimika kusikiliza kila neno linalosemwa na kila Mbunge hapa Bungeni wakati Waheshimiwa Wabunge wanapotoa michango yao, lazima asikilize kila neno na hiyo peke yake inahitaji umakini mkubwa kwa upande wake. Kwa nini analazimika kufanya hivyo? Ni kwa sababu kama mnavyojua vizuri Waheshimiwa Wabunge wakati Mbunge mmoja anapokuwa anasema maneno yake, anapokuwa anachangia maneno yake hapa Bungeni, Mbunge mwingine yoyote na wakati wowote anaweza akasimama ghafla kwenye kiti chake kwa kutumia ile Kanuni ya Kuhusu Utaratibu akahoji na kutoa dukuduku lake na chini ya Kanuni hiyo ikitokea hivyo ni lazima Spika ampe nafasi huyo Mbunge aliyesimama kuhusu utaratibu atoe dukuduku lake hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa basi hebu fikiria ikitokea kwamba Mbunge huyo anayesimama akidai kwamba Mbunge anayeendelea kusema ametumia maneno yasiyokuwa ya Kibunge *(unparliamentarily language)* ikitokea akadai hivyo, sasa na Spika lazima atoe uamuzi wake hapo hapo ili kusudi shughuli ziweze kuendelea. Hebu fikiria sasa kwamba Spika kwa kuwa hakuwa makini, kwa kuwa hakisikia maneno hayo atauliza, hivi alisemaje, akifanya hivyo atakuwa amejivunja heshima yake na atakuwa amevunja vilevile heshima ya kiti chake kwa sababu atakuwa amethibitisha na kudhiririsha wazi kwamba hakuwa makini, alikuwa amelala usingizi. Ni mzigo mkubwa, ni lazima awe makini wakati wote kusikiliza kila neno linalosemwa ili Mbunge akitoa hoja aweze kuliitolea uamuzi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa tuangalie upande wa kulinda heshima ya Kiti cha Spika, hiyo ni kwamba Spika au Kiongozi yeyote anayekaa pale inamlazimu wakati wote awe mwangalifu sana katika kutoa maamuzi yake, kwa nini? Kwani ikitokea kwamba ametoa maamuzi yasiyokubalika na maamuzi hayo yakabatilishwa na Bunge lenyewe atajikuta katika hali mbaya sana. Hii si nadharia, kwa kweli imewahi kutokea mahali pengine, sio hapa kwetu hapana. Kwa mfano kuna mkasa wa aina hiyo ambao ulimpata Spika wa zamani wa Bunge la Australia, kilitokea nini? Alijaribu kumuadhibu Waziri mmojawapo wa Serikali ya Australia, kwa nini alijaribu kumuadhibu.

Mheshimiwa Spika, alimuadhibu kwa kutumia ile Kanuni nyingine ya kumtaja Mbunge, Waheshimiwa Wabunge mnaifahamu ya kumtaja Mbunge kwamba amedharau Madaraka ya Spika anamtaja. Sasa Waheshimiwa Wabunge mnajua hiyo Kanuni Mbunge mmoja akishahoji hivyo kwamba aliyekuwa anasema ikitokea kwamba Spika kamtaja Mbunge, lazima Mbunge asimame papo hapo na kutoa hoja kwamba huyo aliyetajwa asimamishwe kushiriki shughuli za Bunge kwa kipindi atakachoitaja katika hoja yake hii.

Mheshimiwa Spika, sasa basi kilichotokea katika Bunge la Australia ni kwamba Waziri mhusika alisimama, walikuwa wanajadili hoja ya Wizara yake wakati wa Bajeti. Waziri huyo alipokuwa anatoa majibu sasa, anapohitimisha hoja yake, anatoa majibu akasema Mbunge akamtaja Mbunge wa Upinzani kwamba alisema uongo na mnajua kusema uongo haikubaliki

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Bungeni. Waziri akasema Mbunge huyo amesema uongo tena kwa maneno ya Kiingereza alisema; *a monstrous lie* yaani ni uongo wa kutisha, uongo mkubwa wakati alipokuwa anachangia hoja ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, sasa kama Kanuni inavyotaka baada ya Waziri kusema hivyo Mbunge mwingine wa Upinzani kasimama akatoa hoja ya kumwomba Spika amsimamishe Waziri huyo kushiriki katika shughuli za Bunge kwa sababu ametajwa yaani alitoa hoja *monstrous lie* si neno la Kibunge kwanza, kwa hiyo, Waziri asimamishwe kushiriki shughuli za Bunge na akatajwa, kumbe Spika ameridhika na hoja hiyo. Akamwamuru Waziri afute maneno yake. Kama ilivyo utaratibu watu, Waziri akakataa katakata kufuta maneno yake, basi akamtaja kwa Kanuni hiyo.

Sasa Mbunge mwingine wa Upinzani akasimama mara moja kutaka Waziri asimamishwe kushiriki katika shughuli za Bunge na akataja muda gani asimamishwe. Mpaka hapo mambo yamekwenda vizuri kwa mujibu wa taratibu za Bunge hoja imetolewa na Spika ameridhika nayo, ametoa amri, Waziri amekataa, akamtaja na hoja nyingine ikatolewa ya kumsimamisha, yote yamekwenda kwa mujibu wa Kanuni.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo ndio mambo yakamharibikia huyo Spika, yaliharibikaje, kwa sababu Spika alipowahoji sasa Wabunge waiamue hiyo hoja Wabunge wote wa upande wa Serikali wakasema *no*, yaani wakaikataa hiyo hoja na kwa kuwa katika Mabunge yote ya vyama vingi wa upande wa Serikali ndio wengi, basi Bunge likawa limekataa hoja ya kumsimamisha Waziri asishiriki shughuli za Bunge. Hiyo ilimsononesha sana Spika na kwa kuwa alikuwa mstaarabu basi akatangaza kujiuzuru kwamba mandhari Bunge halina imani yake basi anajiuzuru na kweli akatoka uone tu uzito wa mzigo huo wa maamuzi ya Spika. Hivyo ni lazima awe mwangalifu katika maamuzi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nahisi muda ulionipangia sasa unakaribia kumalizika niachane na hadithi, kwa kuwa nazifahamu taratibu za Bunge nisingependa kupigiwa kengele ya nidhamu. *(Kicheko)*

Sasa naomba nimalizie salamu zangu hizi kama nilivyoanzia tu kama wenzangu walivyosema kwa furaha tuliyopewa sisi leo Maspika wastaafu wawili ambao bado tuko hai ya kuruhusiwa kuwasalimieni Waheshimiwa Wabunge tukiwa humu ndani kabisa ya Bunge hili, ni fursa nadra sana, ni fursa ya pekee na pia ni fursa adimu sana na sisi tunatambua hivyo na tutaendelea kutambua hivyo na kuenzi heshima kubwa hiyo mliyotupa leo Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo namalizia kwa kurudia kutoa shukrani zangu kwako Mheshimiwa Spika na Wabunge kwa mema yote mliyotutendea siku hii ya leo na kwa kuwa huu ni mwaka wa uchaguzi Mkuu katika nchi yetu wa Rais, Wabunge na Madiwani naomba nimalizie kwa kuwatakia kila la heri Waheshimiwa Wabunge wote na pia kwa kumuomba Mwenyezi Mungu awashushie baraka zake na neema zake nyingi ziwalettee mafanikio makubwa kila mmoja kulingana na malengo yake binafsi aliyojiwekea katika mwaka huu wa uchaguzi. Na zaidi ya yote naomba Mwenyezi Mungu aendeleo kutujalia huu uwe ni mwaka wa amani na utulivu katika nchi yetu na uwe na amani miongoni mwa wananchi wetu wote, Amina. *(Makofi)*

Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Libariki Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mzee wetu Spika Mstaafu Mheshimiwa Pius Msekwa tunakushukuru mno na kwa pamoja tunawashukuruni mno, mmeifanya siku yetu kuwa ya kipekee sana, *you have made our day. (Makofi)*

Mzee Msekwa ametukumbusha mambo mengi mazuri, muhimu ya kihistoria na kwa kweli yeye ni *encyclopedia* ya masuala ya Kibunge, kabisa na ametuachia kimaandishi kama tulivyosema, maktaba yetu imesheheni kazi zake.

Waheshimiwa Wabunge wote na hasa vijana tuendeleo kuwa tunapitia kule tuchote zile hekima na nikupongeze kwa kuanza kuandika *biography* yako, tunaisubiri kwa hamu, tunasubiri ya Mama Makinda kwa hamu, kitabu hicho tunakisubiri pia, vinasaidia sana, Mama Anna Abdallah tunasubiri kitabu chako kwa sababu Mama Anna Abdallah ni katika wamama wa mwanzo waliochangia sana katika haki ya mwanamke katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mzee Kificho tunasubiri kitabu chako na wengine wengi kama ambavyo Mheshimiwa Rais alitoa wito wakati ule wa kuzindua kitabu cha Mheshimiwa Rais Mstaafu, Benjamin Mkapu. *(Makofi)*

Sasa matangazo machache ndio tuanze kutoka; kwanza kati ya kipindi cha Bunge lililopita na sasa CHADEMA walifanya uchaguzi wao na akachaguliwa Mheshimiwa Freeman Mbowe kuwa Mwenyekiti tena wa chama hicho. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Mwambe! Mwambe!

SPIKA: Kwa hiyo, tunakupongeza sana na nilikuwa naongea na Mheshimiwa Bashiru anasema mkaribishe kwenye ulingo wa Oktoba mwaka huu, eeh! Kwa hiyo, karibu Mheshimiwa Mbowe, karibu sana kwa awamu nyingine. *(Makofi)*

Pia Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Mnyika John Mnyika na yeye amechaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho. *(Makofi)*

Sasa pia Mheshimiwa Freeman Mbowe ameniandikia kunijulisha kwamba Mnadhimu Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni atakuwa ni Mheshimiwa Esther Bulaya. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Wapi Selasini!

SPIKA: Karibu sana Mheshimiwa Esther ufanye kazi karibu na Mheshimiwa Jenista pale, ili mambo yetu yaweze kwenda. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Makofi haya mbona siyo mengi?

SPIKA: Tangazo ljingine ni kutoka kwa Mheshimiwa Anna Lupembe, Mwenyekiti wa Ibada kwenye *chapel* yetu. Anawataarifu Wabunge kwamba, leo baadae hapa baada ya kuahirisha mambo kutakuwa na ibada kwenye *chapel* ya kawaida ya Bunge.

Pia Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mwenyekiti wa Tawi la Simba Bungeni, anawatangazia kwamba baada ya kukamilika zoezi la kujaza fomu ili kupata kadi za mashabiki wa Simba kupitia Benki ya *Equity* mnaombwa kwenda kusaini kwenye hizo kadi zenu leo mchana tayari kwa zoezi la kufungua Ofisi mpya ya Simba Mjengoni litakalofanyika kesho saa 07.00 mchana. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Wamechelewa.

SPIKA: Katika zoezi hilo la kesho saa 07.00 mchana Mheshimiwa Shangazi anawakaribisha kipekee Mdamini wa Yanga, Mheshimiwa George Mkuchika awepo, Mheshimiwa Freeman Mbowe anakaribishwa rasmi awepo, Mheshimiwa Anthony Mavunde kama Mbunge mwenyeji wa Dodoma hapa anatakiwa awepo na Katibu wa Bunge Mheshimiwa Stephen Kagaigai anaombwa awepo kesho hiyo mchana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapa, Mheshimiwa Waziri Mkuu ndio mwenyewe anatakiwa awepo kabisa na ameshapata mwaliko tayari. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya hapa tutafuatana kwenda hapo nje ambapo tutapata picha za pamoja pamoja na Wastaafu wetu na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Mawaziri Wakuu Wastaafu na viongozi wote waalikwa kwenye gallery tukusanyike pale nje kwa ajili ya picha ya pamoja na kwaya pia tuwepo pale kwa ajili ya picha maalum ya kumbukumbu kwa ajili ya kwamba leo ndio tumeanza, kwa hiyo, tuje pale pia. Pia kutakuwa na picha ya Tume, Kamati ya Uongozi, Mawaziri Wakuu Wastaafu, Waheshimiwa Mawaziri mliopo, Makatibu wa Bunge Wastaafu, kutakuwa na picha mbalimbali pale. *(Makofi)*

Mwisho nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kabisa na za wapiga kura wangu wa Kongwa kwa Serikali kwa ujumla kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kunipelekea ahsante kwa Mheshimiwa Rais alipofanya ziara hapa Dodoma alitangaza, mimi sikuwepo pale kwamba Soko jipya la Dodoma litaitwa kwa jina la Job Ndugai. Nashukuru sana kwa heshima hiyo ni heshima kubwa sana kwangu, nawiwa kweli kweli kusema kwamba jambo hili lilinigusa sana. *(Makofi)*

Niliwahi kuwambia hapa nimekuwa Mbunge kwa miaka 20, lakini ukitafuta kule jimboni kwangu hata choo cha shule chenye jina la kwamba mimi niliwahi kuzindua hakuna. *(Kicheko)*

Na Wabunge wengine wengi nafikiri ni hivyo, labda wale mliolazimisha niwekwe mimi jina langu, lakini hapajawahi kuwa na kumbukumbu ya namna hiyo kwa hiyo, kunikumbuka kwa hilo kwa kweli namshukuru sana nasema ahsante sana. *(Makofi)*

Basi baada ya zoezi hili sasa naomba Mpambe wa Bunge ajiandae kuja kuwachukua Wastaafu wetu kwanza mmoja baada ya mwingine kuwatoa nje na baadaye itakuwa ni zamu yetu sisi wengine wote. Atanza Mheshimiwa Spika Mstaafu Pius Msekwa, atafuata Mama Margaret Sitta, wataondoka mmoja-mmoja. *(Makofi)*

(Hapa Spika Mstaafu Mhe. Pius C. Msekwa Aliondoka Ukumbini)

SPIKA: Ahsante sana, sasa anafuata Mama Margaret Sitta. Naomba Mpambe wa Bunge uje umchukue muweze kumtoa nje kwa utaratibu huo huo.

(Hapa Mhe. Margaret S. Sitta Aliondoka Ukumbini)

SPIKA: Na sasa nimuombe Mpambe wa Bunge aje amchukue Mama yetu, Spika Mstaafu Mheshimiwa Mama Anne Semamba Makinda, pia aweze kutoka sasa kwenye Ukumbi wa Bunge. *(Makofi)*

- (f) oversee the implementation of the Society’s strategic initiatives and its functioning within the agreed framework, in accordance with relevant statutory and regulatory structures;
- (g) ensure the adequacy of financial, operational systems and internal controls;
- (h) ensure the implementation of corporate ethics and the Code of Conduct;
- (i) convene Annual General

Meetings; and

(j) perform any other duty in relation to the affairs of the Society subject to this Act or regulations made hereunder.”.

Addition of section 17A

54. The principal Act is amended by adding immediately after section 17 the following-
“Chapters of Society

17A.-(1) There shall be Chapters of the Society in designated regions as the Council may consider necessary.

(2) There shall be chapter zones established by the Council for proper governance and management of the affairs of the chapters.

(3) The Council may make rules to govern the conduct and operations of Chapters and Chapter zones.”.

Amendment of Part V

55. The principal Act is amended by deleting the title to Part V and substituting for it the following:

PART V
SECRETARIAT

Repeal and replacement of section 19

56. The principal Act is amended by repealing section 19 and replacing for it the following-
“Secretariat of Society

19.-(1) There shall be a Secretariat of the Society which shall be responsible for the day to day management and administration of the affairs of the Society.

(2) The functions of the Secretariat shall be to-

(a) implement decisions of the Council;

(b) assist the Council in the preparation of reports and any other information for the members or stakeholders;

(c) support the committees, chapters, zones and other bodies of the Society to discharge their functions;

(d) organise conferences of the

Society;

(e) raise funds and manage the financial affairs of the Society within the limits of its approved budget;

(f) keep proper books and records of all financial affairs of the Society;

(g) keep proper minutes and activity reports of the Society;

(h) keep up to date records and database of members of the Society;

(i) develop and implement projects aimed at realizing the objects of the Society and its strategic plans; and

(j) perform any other activities in the attainment of the Society's objectives.

(3) The Council shall employ a person from amongst members or officers of the Society to be the Executive Director of the Secretariat.

(4) The Executive Director shall be employed by the Council through a transparent and competitive recruitment process.

(5) The Executive Director shall be the chief executive officer and the accounting officer of the Society and shall, in particular-

(a) be responsible for the recruitment of staff of the Secretariat;

(b) be responsible for the preparation of periodic strategic plans, annual action plans and budget;

(c) be responsible for the supervision and monitoring of the day to day implementation of objectives and functions of the society;

(d) be responsible for raising

funds of the Society;

(e) be the Secretary to the Council;

(f) be accountable to the Council; and

(g) perform any other duties for the proper management and administration of the affairs of the Society.

(6) A person shall not be eligible to be employed as the Executive Director of the Society unless that person-

(a) is an advocate of the High Court of Tanzania and the courts subordinate thereto, with at least ten years of practice;

(b) is of good moral standing in the society; and

(c) has demonstrated experience in management of the same position or its equivalent.

(7) A person employed as Executive Director shall hold office for a term of five years and may be eligible to serve for one further term subject to good standing performance.

(8) The Executive Director may be removed from office by the Council by votes of at least two thirds of the members on any of the following grounds-

(a) inability to perform functions of the office due to mental or physical infirmity;

(b) gross misconduct;

(c) incompetence;

(d) has been adjudged bankrupt;

(e) desertion of office or duty;

or

(f) has been convicted of a criminal offence punishable by imprisonment for a period of not less than two years.

(9) The Council shall, before

removing the Executive Director-

(a) notify the Executive Director, in writing, of the reasons for the intended removal; and

(b) afford the Executive Director an opportunity to be heard in defence of allegations brought against him.”.

Repeal
replacement
section 21

and
of

57. The principal Act is amended by repealing section 21 and replacing for it the following:

“Annual General Meeting

21.-(1) The Council shall, in at least the second week of April of each calendar year, convene an Annual General Meeting of the Society.

(2) The Council may, where circumstances so permit, convene other general meetings of the Society.

(3) The Annual General Meeting shall be convened by way of representation.

(4) The Annual General Meeting shall be duly constituted where it is composed of:

(a) members of the Council;

(b) members of all Standing Committees;

(c) all Chapter leaders including members of their standing committees;

(d) four members from each Chapter comprising of representatives of young lawyers, female lawyers, senior lawyers and persons with disability, all elected annually by chapter members in the chapter general meetings;

(e) members of the Zonal Executive Committees;

(f) two members from the Chapter zones elected from the zone members during zonal annual general meeting; and

(g) any other person, as the Council may consider necessary to invite.

(5) Annual General Meetings

shall be conducted as prescribed by Council.”.

Amendment
section 22 of

58. The principal Act is amended in section 22, by deleting subsection (1) and substituting for it the following-

“(1) Notwithstanding section 21, the Council may convene a general meeting of the Society whereat least one third of members of good standing consisting of equal percentage representation from each Chapter, at any time requisition a general meeting by written notice in that behalf signed by them, specifying the object of the proposed meeting, and deposit with the Executive Director.”.

Amendment
section 28 of

59. The principal Act is amended in section 28, by-

(a) designating the contents of section 28 as contents of subsection (1);

(b) adding immediately after subsection (1) as designated the following:

“(2) The Council shall submit to the Minister minutes of the Annual General Meeting or general meeting as the case may be within two months after the minutes have been confirmed by the Annual General Meeting or general meeting respectively.”.

Repeal
replacement
section 29 and
of

60. The principal Act is amended by repealing section 29 and replacing for it the following-

“Accounts of Society

29.-(1) The Council shall cause proper accounts of all funds, property and assets of the Society to be kept, and to be audited, by an auditor approved by the Annual General Meeting from amongst auditors approved by the Minister responsible for finance.

(2) The Council shall present the audited accounts, together with the auditor’s report to the Annual General Meeting convened at a time and manner prescribed in accordance with section 21.

(3) The Council shall serve a copy of the audited accounts together with the auditor’s report to the Minister and the Minister

responsible for finance within six weeks after the report is presented at the Annual General Meeting.”.

Repeal
replacement
section 30

and
of

61. The principal Act is amended by repealing section 30 and replacing for it the following-
“Reports and accounts

30.-(1) The Council shall, in the Annual General Meeting, present to the Society an annual report of the activities of the Society.

(2) The Council shall deliver a copy of the annual report to the Minister within six weeks after being presented at the Annual General Meeting.”.

PART XV

AMENDMENT OF THE TRUSTEES’ INCORPORATION ACT, (CAP. 318)

Construction
Cap.318

62. This Part shall be read as one with the Trustees’ Incorporation Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Amendment
section 2

of

63. The principal Act is amended in section 2, by adding immediately after subsection (3) the following:

“(4) The Administrator-General may, before a trust is incorporated or at any later stage after incorporation, require disclosure of the names of settlors and beneficiaries of the trust.”.

Amendment
section 8

of

64. The principal Act is amended in section 8(1), by adding the words “finance, shares, monies” after the word “land,” wherever it appears in paragraph (c).

OBJECTS AND REASONS

This Bill proposes to amend Fourteen laws namely: the Civil Procedure Code, (Cap. 33), the Criminal Procedure Act, (Cap. 20), the Dairy Industry Act, (Cap. 262), the Executive Agencies Act, (Cap. 245), the Fisheries Act (Cap. 279), the Government Proceedings Act, (Cap. 5), the Law of the Child Act, (Cap. 13), the Local Government (Districts Authorities) Authorities Act, (Cap. 287), the Local Government (Urban Authorities) Act, (Cap. 288), the Meat Industry Act, (Cap. 421), the Penal Code, (Cap. 16), the Probate and Administration of Estates Act, (Cap. 352) and the Tanganyika Law Society Act, (Cap. 307), and the Trustees' Incorporation Act, (Cap.318).

The proposed amendments intend to keep updated the respective laws with changes so far observed in their implementation.

This Bill is divided into Fifteen Parts.

Part I deals with preliminary provisions which include the title of the Bill and the manner in which the laws proposed to be amended, are amended in their respective Parts.

Part II of the Bill proposes to amend the Civil Procedure Code, Cap. 33 by adding a new section 64A with a view to including in the Act provisions relating to conciliation, negotiation and mediation. The objective of the amendments is to facilitate settling of disputes out of court through a recognized forum.

Part III of the Bill proposes to amend the Criminal Procedure Act, Cap. 20. The amendments expound on the meaning of "substance of evidence". The objective of the amendment is to enhance clarity of the definition in order accommodate other specified forms of evidence obtained during committal proceedings.

Part IV of the Bill proposes to amend the Dairy Industry Act, Cap. 262. The proposed amendments intend to improve composition of the Annual Council so as to make the Council more effective, manageable and to enhance improved cooperation between the Council and the Dairy Board.

The Bill is amended to improve composition of Board members of the Tanzania Dairy Board by empowering the Minister to appoint competent members who are resourceful to the dairy industry; and to reduce number of Board members in order to improve efficiency of the Board. These amendments make provisions for dairy stakeholders to be registered by the Board for the purpose of better control of the industry.

The Bill further proposes to empower the Minister to establish a Dairy Laboratory with a view to enhancing capacity of the Tanzania Dairy Board (TDB) to carry out tests and analysis for compliance and research. A provision on compounding of offences is also introduced in this Part in order to facilitate compliance and reduction of time and cost of litigation. The Act is amended to provide for delegation of powers to local government authorities for the purpose of widening TDB outreach services.

Part V of the Bill proposes to amend the Executive Agencies Act, Cap. 245. The Act is amended to make requirements for executive agencies to notify the Attorney General and the Solicitor General of all proceedings by or against the Executive Agency. This proposal is a result of the changes effected through the Written Laws Miscellaneous Amendment (No. 7) Act, 2018 which amended the Attorney General (Discharge of Duties), Act, Cap. 268 following the restructuring of the Office of the Attorney General.

Part VI of the Bill proposes to amend the Fisheries Act, Cap. 279. The amendments intend to enhance efficiency in the management and control of fisheries resources. The Act is further amended to impose obligations on local government authorities to perform their role of management, protection, conservation and development of fisheries resources in their respective jurisdiction to ensure sustainability of fisheries resources.

The Act is further amended to increase penalties prescribed. The objective of the amendment is to deter offenders against illegal fishing and trade activities and to foster compliance and sustainable preservation of fisheries resources and aquatic environment.

Part VII of the Bill proposes to amend the Government Proceedings Act, Cap. 5. The proposed amendments intend to make better procedural requirements regarding notices of cases by or against the Government. The Bill is also amended

to vitiate any proceeding for or against the Government where service of notice to the Attorney General and Solicitor General has not been effected. The objective of the amendment is make provisions for better management of cases for and against the Government.

Part VIII proposes to amend the Law of the Child Act, Cap. 13. The Act is amended to confer jurisdiction to all district courts and courts of resident magistrate to handle juvenile cases. The proposed amendments also place the juvenile courts under the management and supervision of the district courts and courts of the resident magistrates' in their respective districts and regions.

Part IX proposes to amend the Local Government (Districts Authorities) Act, Cap. 287. The Act is amended by providing for the requirement of District Executive Director be joined in cases that involve the Village Council, and the issuance of ninety days' notice to the Director and a copy thereof to the Attorney General and the Solicitor General. The objective of the amendment is to make better provisions for the management of cases and safeguarding of Government resources.

Part X proposes to amend the Local Government (Urban Authorities) Act, Cap. 288. The amendments intend to align the provisions of the Act with the requirement of 90 days notice to sue the Attorney General and Solicitor General as provided for under the Government Proceedings Act, Cap. 5.

Part XI proposes to amend the Meat Industry Act, Cap. 421. The proposed amendments intend to provide for a new definition of "meat industry stakeholder" to include business entities involved in the meat industry; to improve the composition of the Board by powering the Minister to appoint competent members who are resourceful to the industry; and to reduce number of Board members in order to increase efficiency of the Board. The Act is further amended by introducing specific penalties for import and export of meat and meat products without permits; and compounding of offences for the purpose of reducing time and cost associated with litigation.

Part XII proposes to amend the Penal Code, Cap. 16. The proposed amendments aim at protecting the male child from sexual abuses other than rape.

Part XIII proposes to amend the Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352. The proposed amendments intend to prohibit non-citizens from owning

land through inheritance. The Act makes a requirement for the Administrator to sell landed property and the proceeds thereto be distributed to the non-citizens, if any.

Part XIV proposes to amend the Tanganyika Law Society Act, Cap. 307. The proposed amendments intend to improve the composition of the Governing Council so as to ensure better management of the Council. The amendments further improve the roles and functions of the Council. It is also proposed to recognize Chapters and zones of the Society, stipulate the roles and functions of the Secretariat and remove the Half Annual General Meeting with the aim of reducing the cost of management and operations and enhancing timely implementation of responsibilities by the Council.

Part XV proposes to amend the Trustees' Incorporation Act, Cap. 318. The proposed amendments intend to recognize settlors and beneficiaries of a particular trust.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza marekebisho katika Sheria Kumi na Nne zifuatazo: Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, (Sura ya 33), Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, (Sura ya 20), Sheria ya Maziwa, (Sura ya 262), Sheria ya Wakala wa Serikali, (Sura ya 245), Sheria ya Uvuvi, (Sura ya 279), Sheria ya Mwenendo wa Mashauri Dhidi ya Serikali, (Sura ya 5), Sheria ya Mtoto, (Sura ya 13), Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), (Sura ya 287), Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), (Sura ya 288), Sheria ya Tasnia ya Nyama, (Sura ya 421), Sheria ya Kanuni za Adhabu, (Sura ya 16), Sheria ya Usimamizi wa Mirathi, (Sura ya 352), Sheria ya Chama cha Mawakili Taganyika, (Sura ya 307) na Sheria ya Usajili wa Wadhamini, (Sura ya 318).

Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuboresha sheria husika ili ziendane na mabadiliko ya wakati na kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wake.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kumi na Tano.

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya Utangulizi na yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho zimerekebishwa katika Sehemu husika ya Muswada.

Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sura ya 33 kwa kuongeza vifungu vipya vya 64A, 64B na 64C ili kujumuisha katika Sheria hiyo masharti yanayohusu kushughulikia madai kwa njia ya usuluhishi, mazungumzo na upatanishi. Kwa mujibu wa mapendekezo haya, Waziri atakuwa na mamlaka ya kuanzisha vituo vya usuluhishi, mazungumzo na upatanishi na kutengeneza kanuni za kuelekeza utaratibu wa kushughulikia migogoro katika vituo hivyo. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha upatanishi, mazungumzo na usuluhishi wa migogoro kufanyika nje ya Mahakama kupitia jukwaa linalotambulika.

Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20. Marekebisho haya yanatoa ufafanuzi wa msamiati “mantiki ya ushahidi” yaliyotumika katika sheria hiyo kwa

lengo la kuongeza wigo wa ushahidi unaopaswa kutolewa mahakamani wakati wa taratibu za kuhamisha shauri kwenda kwenye mahakama yenye mamalaka ya kusikiliza shauri husika.

Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Tasnia ya Maziwa, Sura ya 262. Mapendekezo ya marekebisho yanalenga kuboresha muundo wa Baraza la Mwaka ili kulifanya Baraza hilo liwe na ufanisi zaidi na kuboresha ushirikiano baina ya Baraza hilo na Bodi ya Maziwa.

Sheria inarekebishwa ili kuboresha uwakilishi wa wajumbe wa Bodi ya Maziwa kwa kumpa mamlaka Waziri kuteua wajumbe wenye ujuzi wa kuendeleza tasnia ya maziwa. Sheria inarekebishwa kwa kupunguza idadi ya wajumbe wa Bodi ili kuongeza ufanisi wa Bodi hiyo. Marekebisho haya pia yanaweka masharti ya wadau wa tasnia ya maziwa kusajiliwa na Bodi ili kuwezesha uratibu na udhibiti kwa tasnia ya maziwa.

Sheria inarekebishwa kwa kuweka vifungu vipya vinavyohusu uanzishwaji wa maabara ya maziwa ili kuijengea uwezo Bodi ya Maziwa katika kufanya uchunguzi wa kimaabara kwa ajili ya uhakiki na utafiti. Sheria inarekebishwa kwa kuweka utaratibu wa ufililishaji wa makosa kwa lengo la kuimarisha dhana ya utii wa sheria na kupunguza muda na gharama zitokanazo na uendeshaji wa mashauri mahakamani.

Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura ya 245. Marekebisho haya yanapendekeza kuweka masharti ya kutoa notisi kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wakili Mkuu wa Serikali pale Wakala wa Serikali anaposhtakiwa. Marekebisho haya pia yanaoanisha masharti ya Sheria hiyo ili kuendana na mabadiliko katika Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yaliyofanywa kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 7) ya Mwaka 2018 kufuatia mabadiliko ya muundo wa Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Lengo la marekebisho haya ni kuweka msingi bora wa kulinda mali za Serikali zilizo chini ya Wakala wa Serikali.

Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Uvuvi, Sura ya 279. Marekebisho yanalenga kuongeza ufanisi katika usimamizi na udhibiti wa raslimali za uvuvi. Sheria inarekebishwa pia kwa kuweka wajibu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu ya kusimamia, kulinda, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za uvuvi zilizopo katika maeneo yao.

Pia, marekebisho haya yanalenga kuongeza viwango vya adhabu ili kuthibiti uhalifu dhidi ya uvuvi haramu na kuimarisha utii wa sheria na kuboresha utunzaji wa rasilimali za uvuvi na mazingira ya maji.

Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mwenendo wa Mashauri dhidi ya Serikali, Sura ya 5. Marekebisho haya yanapendekeza kuboresha taratibu za utoaji notisi katika mashauri yanayoihusu Serikali. Sheria inapendekezwa kurekebisha kwa kuweka masharti ya kubatilisha mashauri yote dhidi ya Serikali iwapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali hajaunganishwa kwenye shauri husika. Lengo la marekebisho hayo ni kuweka utaratibu bora wa usimamizi wa mashauri yanayoihusu Serikali.

Sehemu ya Nane inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mtoto, Sura ya 13. Sheria inarekebisha ili kuzipa mamlaka Mahakama za Wilaya na Mahakama za Hakimu Mkazi kusikiliza mashauri ya watoto. Marekebisho katika Sheria yanaiweka Mahakama ya Mtoto chini ya usimamizi na uangalizi wa Mahakama za Wilaya na Mahakama za Hakimu Mkazi katika Wilaya na Mkoa husika.

Sehemu ya Tisa inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287. Sheria hiyo inarekebisha kwa kuweka masharti ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya kujumuishwa katika shauri lolote linalohusu Halmashauri ya Kijiji, na utoaji wa notisi ya siku tisini kwa Mkurugenzi huyo na nakala kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wakili Mkuu wa Serikali. Lengo la marekebisho hayo ni kuweka utaratibu bora wa usimamizi wa mashauri yanayoihusu Serikali.

Sehemu ya Kumi inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288. Sheria hiyo inarekebisha ili kuainisha masharti ya utoaji wa notisi ya siku tisini kabla ya kuishitaki Serikali kwa kumjumuisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wakili Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Mashauri Dhidi ya Serikali, Sura ya 5.

Sehemu ya Kumi na Moja inapendekeza kurekebisha Sheria ya Tasnia ya Nyama, Sura ya 421. Marekebisho hayo yanalenga kutoa tafsiri mpya ya “wadau wa tasnia ya nyama” ili kujumuisha nyanja zote za biashara katika tasnia ya nyama, kuboresha uwakilishi wa wajumbe wa Bodi ya Nyama kwa kumpa Waziri mamlaka kuteua wajumbe wenye ujuzi wa kuendeleza tasnia ya nyama na

kupunguza idadi ya wajumbe wa Bodi ili kuongeza ufanisi wa Bodi. Sheria inarekebishwa kwa kuweka adhabu mahsusi kwa waingizaji na wasafirishaji wa nyama na bidhaa za nyama ndani na nje ya nchi bila vibali. Sheria inarekebishwa kwa kuweka utaratibu wa ufililishaji wa makosa kwa lengo la kuimarisha utii wa sheria na kupunguza muda na gharama zitokanazo na uendeshaji wa mashauri mahakamani.

Sehemu ya Kumi na Mbili inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16. Mapendekezo ya marekebisho yana lengo la kuwalinda watoto wa kiume dhidi ya makosa ya udhalilishaji wa kingono mbali na makosa ya ubakaji.

Sehemu ya Kumi na Tatu inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Mirathi, Sura ya 352. Mapendekezo ya marekebisho yanakusudia kukataza watu wasio raia kumiliki ardhi kupitia mirathi. Aidha, sheria inaweka utaratibu wa watu wasio raia kunufaika na mauzo ya mirathi inayohusiana na ardhi.

Sehemu ya Kumi na Nne inapendekeza kurekebisha Sheria ya Chama cha Mawakili Taganyika, Sura ya 307. Mapendekezo yanakusudia kuboresha uwakilishi wa wajumbe wa Baraza Kuu ili kuweka usimamizi bora wa Baraza. Marekebisho yanapendekezwa ili kutambua Ofisi za kanda, kuondoa Mkutano Mkuu wa nusu mwaka kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji wa Baraza.

Sehemu ya Kumi na Tano inapendekezwa kurekebisha Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura ya 318. Marekebisho haya yanakusudia kuwatambua wasimamizi na wanufaika wa mali zilizo chini ya udhamini.

Dodoma,
21 Oktoba, 2019

ADELARDUS L. KILANGI,
Attorney General

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono nakushukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa wasilisho lako. Tunaendelea tupate maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria au mwakilishi wake, oooh Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Giga karibu una muda usiozidi dakika 20.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya na nikaweza kukutana na nanyi katika mwaka huu mpya wa 2020. Lakini pia naomba nitumiea fursa hii kuwatakia kheri wa Waheshimiwa Wabunge wote heri ya mwaka mpya lakini pia na Watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kusoma taarifa yangu naomba taarifa kamili yote ya Kamati yetu iingezwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 8) ya mwaka 2019 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.8) Bill, 2019*, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilikutana na Serikali katika Ukumbi Namba 9 uliopo Jengo la Utawala katika Ofisi za Bunge Dodoma, mnamo tarehe 15 Januari, 2020 ili kupokea maelezo kuhusu muswada husika. Katika kikao hicho, mtoa hoja alijulisha Kamati kuwa muswada huu unakusudia kufanya marekebisho katika sheria kumi na nne (14) ili kuondoa upungufu ambao umebainika wakati wa utekelezaji wa sheria hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi kwa taasisi zinazosimamia utekelezaji wa sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Serikali yalionesha kuwa, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 8) wa mwaka 2019 unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria kumi na nne (14) kama ilivyoainishwa kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea maelezo hayo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kutoa matangazo ya kuwaalika wadau mbalimbali wafike mbele ya Kamati kwa lengo la kuisaidia katika uchambuzi wa muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa matangazo hayo, wadau walifika na walipewa fursa ya kusikilizwa wakiwasilisha maoni yao. Aidha, baadhi ya wadau waliwasilisha maoni yao kupitia Ofisi ya Katibu wa Bunge na orodha ya taasisi hizo ni kama ifuatavyo; Chama cha Wanasheria Tanganyika *(Tanganyika Law Society)*, TWaweza, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na *Tangible Initiatives for Local Development Tanzania*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati wadau wote kwa ushirikiano wao kwa kuisaidia Kamati kuulewa na kuuchambua muswada huu kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; baada ya kuzungumzia masuala ya awali katika utangulizi wa taarifa hii, napenda kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maoni ya Kamati ambayo yametokana na maelezo ya Serikali pamoja uchambuzi wa Kamati katika Sehemu na Ibara mbalimbali za muswada huu.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya jumla kuhusu uchambuzi wa muswada Kamati ilipitia na kufanya uchambuzi wa sehemu kumi na tano za muswada zenye Ibara 64 na vifungu vyote vya sheria vinavyopendekezwa kurekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi wa Muswada uliofanywa na Kamati, kwa kupitia Ibara zote zinazopendekeza marekebisho katika sheria kuu husika, Kamati inapenda kutoa maoni kuwa, kwa ujumla maudhui ya Muswada huu yana tija kwa taifa na endapo mapendekezo ya marekebisho yatapitishwa na kuwa Sheria yatasaidia kuondoa mapungufu yaliyopo katika Sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati imeridhia marekebisho yanayopendekezwa katika kila sheria inayorekebishwa katika muswada huu, na inaipongeza Serikali kwa kubainisha upungufu katika sheria husika na kuandaa mapendekezo ya kuboresha yaliyowasilishwa katika muswada huu na ambayo yameridhiwa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na Kamati kuridhishwa na maudhui pamoja na mantiki ya marekebisho yanayopendekezwa katika kila sheria husika, ilibaini baadhi ya dosari za kiuandishi katika jumla ya Ibara 13 za baadhi ya sheria ambapo Ibara hizo zenye dosari za kiuandishi ni kama zilivyoinishwa kwenye Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kubaini dosari hizo Kamati ilipendekeza marekebisho yafanyike katika ibara za sheria husika kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho lilioletwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala matatu mahsusi katika muswada; kupitia vikao vya kupokea na kujadili maoni ya wadau pamoja na vikao vya majadiliano na Serikali kuhusu muswada huu, Kamati ilibaini masuala mahsusi ambayo kwa upekee wake naomba niyataje hapa chini.

(i) Waziri kupewa mamlaka ya kuwateua Wenyeviti wa Bodi badala ya Mamlaka hayo kubaki kwa Rais kama ilivyo kwenye sheria nyingine. Suala hilo limebainika katika Ibara ya 13 ya Sheria ya *The Dairy Industry Act, CAP 262* na Ibara ya 38 ya Sheria ya *The Meat Industry Act, CAP 421*;

(ii) Ni mabadiliko ya mfumo wa uwakilishi ndani ya Chama cha Wanasheria wa Tanganyika kwenye vikao vya juu vya maamuzi, ambapo baadhi ya marekebisho yanayopendekezwa katika Ibara 47 ya Sheria ya *The Tanganyika Law Society Act, CAP 307*, yamependekeza dhana ya uwakilishi wa kikanda bila kuweka uwiano wa uwakilishi huo kwa kuzingatia uwiano wa idadi ya wanachama kwa baadhi ya Mikoa na Kanda zenye wanachama wengi;

(iii) Kuwepo kwa hofu ya kuingiliana kwa majukumu ya Muhimili wa Serikali Kuu na Mahakama, ambapo marekebisho katika Ibara ya 59 ya Sheria ya *The Tanganyika Law Society Act, CAP 307*, inampa Waziri ambaye ni sehemu ya Serikali Kuu kuingilia kumbukumbu za vikao vya ndani vya Mkutano Mkuu wa *TLS*.

Pamoja na masuala mengine muhimu yaliyobainika katika Muswada huu, Kamati iliweza kujadili masuala hayo mahsusi kwa kufanya uchambuzi wa kina wa kimantiki kwa kupima malengo ya Serikali sambamba na matamania ya wadau wa sekta ya sheria nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilikwenda mbali kwa kulinganisha hali halisi ya mabadiliko katika sekta ya sheria nchini kutoka mwaka 1954 hadi sasa, na hatimaye kufanya

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maamuzi kwa kupendekeza maboresho katika baadhi ya Ibara pamoja na kuridhia baadhi ya mapendekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifikia hatua hiyo baada ya kupokea na kujadili maelezo ya ziada kutoka Serikalini yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali tarehe 23 Januari, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo; Kamati ilibaini baadhi ya dosari na kupendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika Ibara ya 17 Kamati inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 33A kinachopendekeza kuanzisha Maabara ya Maziwa kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika Ibara ya 45 inayopendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 108 cha Sheria ya *The Probate and Administration of Estates Act, (CAP 352)*, kwa kuongeza kifungu kidogo cha (3) kinachoweka katazo la kugawa ardhi au nyumba kwa mtu ambaye si raia wa Tanzania kwa njia ya mirathi. Kamati inapendekeza kifungu hicho kifutwe ili Serikali ipate muda wa kujiandaa kuleta marekebisho yenye kuzingatia masuala mbalimbali yenye tija kwa Serikali na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho katika Ibara ya 52 inayopendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 15 cha Sheria ya *TLS*, kwa kufuta kifungu kidogo cha kwanza na kukiandika upya ili kuboresha muundo wa Baraza la Uongozi wa *TLS*, Kamati inapendekeza katika kifungu kidogo cha 15(6) kufuta maneno; *“expiration of tenure”* na badala yake kuweka maneno *“swearing in of the new members of the Council”*. Kifungu hicho kisomeke kama hivi ambavyo nitasoma; *“The President, Vice-President, Honorary Treasurer and others members of the members of the council shall assume office immediately after being sworn-in and hold office until the swearing in of new members of the council”*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo hayo yamezingatiwa na Serikali kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 53 inayopewa kufanya marekebisho katika Kifungu cha 16 cha Sheria ya *TLS*, kwa kufuta na kuandika upya maudhui yake kwa lengo la kuboresha madaraka na majukumu ya Baraza, kwa kuongeza aya mpya ya 16(j) inayoweka masharti ya utaratibu wa kutunga kanuni ambacho kinasomeka; *16(j) make regulations for governance and management of the secretariat*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo hayo yamezingatiwa kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 59 inayopendekeza kurekebisha Kifungu cha 28 cha Sheria ya *TLS*, kwa kubadilisha maudhui ya kifungu hicho kuwa maudhui ya kifungu cha 28(1) na kuongeza kifungu kidogo kipya cha 28(2), Kamati inapendekeza maneno *“Kumbukumbu za Mikutano ya Chama”* yafutwe na badala yake kuandikwe maneno *“Taarifa za Mwaka,”* ili kulinda uhuru wa uendeshaji wa shughuli za chama pasipokuingiliwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeridhia mapendekezo ya Kamati kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 59 inayopendekeza kurekebisha kifungu cha 28 cha Sheria ya *The Trustees' Incorporation Act, (CAP. 318)* kwa kubadilisha maudhui ya kifungu hicho kuwa maudhui ya kifungu cha 28(1) na kuongeza kifungu kidogo kipya cha 28(2), Kamati inapendekeza kuongeza maneno mengine kwenye maneno yanayopendekezwa kuingizwa katika kifungu cha 8(1). Maneno yanayopendekezwa kuongezwa ni *securities, stock, or any other property*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo hayo yamezingatiwa na Serikali kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya jumla Kamati ilibaini masuala mbalimbali ya jumla ambayo muhimu yakaboreshwa kwa lengo la kuleta ufanisi wa kutosha kwenye sekta husika kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, Kamati imebainika wazi kuwa, tasnia ya Nyama na Maziwa imeendelea kukua siku hadi siku pia ni moja ya vitega uchumi muhimu na endelevu hapa nchini;

Na kwa kuwa, kukosekana kwa chombo mathubuti chenye mamlaka kamili ya kusimamia na kuratibu tasnia za nyama na maziwa zinazozidi kupanuka kwa kasi kunaweza kuathiri mchango wa tasnia hiyo katika Uchumi endelevu wa Taifa;

Hivyo basi, Kamati inashauri kuwa, Serikali ianze kujipanga kuanza na kukamilisha mchakato wakuunda chombo Kimoja mathubuti zaidi ya Bodi za ushauri, ambacho kitaisaidia Serikali katika kusimamia na kuratibu tasnia ya nyama na maziwa nchini ili tasnia hizo ziwe na tija stahiki katika kuchangia pato la Taifa;

Kwa kuwa, Kamati imebainika kuwa Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika imekuwepo tangu mwaka 1954, wakati wa utawala wa Kikoloni;

Na kwa kuwa, ni ukweli usiopingika kuwa taaluma hiyo imekuwa ikikua na kuimarika kila mwaka kiasi cha kuendelea kuongezeka idadi ya wanataaluma hao;

Na kwa kuwa, ongezeko hilo la wanataaluma sambamba na mabadiliko mbalimbali katika sekta ya sheria haviwezi kuratibiwa na marekebisho madogo ya sheria hayawezi kuleta mabadiliko makubwa yanayotakiwa kwa sasa;

Hivyo basi, Kamati inashauri kuwa, Serikali ijipange vizuri na kuanza mchakato jumuishi wa kuja na Sheria Mpya ya Chama cha Wanasheria Tanganyika, kwa lengo la kukiwezesha chama hicho kujiendesha kwa kuzingatia mahitaji ya nchi na Kimataifa yaliyopo kwa sasa. Kwa ustawi wa taaluma ya Sheria na kwa maendeleo edelevu ya usimamizi na utetezi wa utoaji haki nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimisha kwa kusema kwa mara nyingine naomba nikushukuru wewe mwenyewe, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Spika kwa kutoa kibali ili kamati ya Katiba na Sheria ikaweza kufanya kazi katika muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumtambua na kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Profesa Adelarudus Kilangi, pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati ulioiwezesha Kamati kukamilisha uchambuzi wa muswada huu kwa wakati. Aidha, Kamati inatambua na kumshukuru kila Waziri

na watendaji wake waliofika mbele ya Kamati kwa lengo la kuisaidia Kamati kukamilisha kazi yake kwa ufanisi mkubwa na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa weledi na umahiri wao waliouonesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa Mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususan Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili, Wanasheria Wasaidizi wa Bunge, Ndugu Mossy Lukuvi, Ndugu Hawa Manzurya na Ndugu Thomas Shawa. Pia Makatibu wa Kamati Ndugu Stanslaus Kagisa na Ndugu Angela Henry Shekifu, pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Rahel Masima, waliofanikisha kazi ya uchambuzi na uratibu wa shughuli za Kamati kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NA.8) WA MWAKA 2019(THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.8) BILL, 2019

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, tarehe 14 Novemba, 2019, wakati wa Kikao cha Nane (8) cha Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.8 wa Mwaka 2019 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.8) Bill, 2019] ulisomwa mara ya kwanza Bungeni. Baada ya hapo, Mheshimiwa Spika alizingatia Masharti ya Kanuni ya 84(1) kwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kupeleka Muswada huo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, Kamati iliujadili Muswada huo kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni za Kudumu za Bunge hususan Sehemu ya Nane ya Kanuni za Bunge inayohusu masharti ya Jumla kuhusiana na kutunga Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria Kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.8) Wa Mwaka 2019(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.8) Bill, 2019, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilikutana na Serikali katika **Ukumbi Na.9** uliopo Jengo la Utawala katika Ofisi za Bunge Dodoma, mnamo tarehe 15 Januari, 2020 ili kupokea maelezo kuhusu Muswada husika. Katika kikao hicho, Mtoa Hoja alijulisha Kamati kuwa, Muswada huu unakusudia kufanya marekebisho katika Sheria Kumi na Nne (14) ili kuondoa upungufu ambao umebainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi kwa Taasisi zinazosimamia utekelezaji wa Sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 8) wa Mwaka 2019 unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Kumi na Nne(14) zifuatazo:

- a) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sura ya 33 **[The Civil Procedure Code, Cap 33]**;
- b) Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 **[The Criminal Procedure Act, Cap 20]**;
- c) Sheria ya Tasnia ya Maziwa, Sura ya 262 **(The Dairy Industry Act, Cap 262)**;
- d) Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura ya 245 **(The Executive Agencies Act, Cap, 245)**;
- e) Sheria ya Uvuvi, Sura ya 279 **(The Fisheries Act, Cap 279)**;
- f) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri Dhidi ya Serikali, Sura ya 5 **(The Government Proceedings Act, Cap 5)**;
- g) Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 **(The Law of the Child Act, Cap 13)**;
- h) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 **(The Local Government (Districts Authorities) Act, Cap 287)**;
- i) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288 **(The Local Government (Urban Authorities) Act, Cap 288)**;
- j) Sheria ya Tasnia ya Nyama Sura ya 421 **(The Meat Industry Act, Cap 421)**;
- k) Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 **(The Penal Code, Cap 16)**;
- l) Sheria ya Usimamizi wa Mirathi, Sura ya 352 **(The Probate and Administration of Estate Act, Cap 353)**;
- m) Sheria ya Chama cha Mawakili Tanganyika, Sura ya 307 **(The Tanganyika Law Society Act, Cap 307); na**
- n) Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura ya 318 **(The Trustees' Incorporation Act, Cap. 318).**

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea maelezo hayo, Kamati ilizingatia masharti ya **Kanuni ya 84(2)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kutoa matangazo ya kuwaalika wadau mbalimbali wafike mbele ya Kamati kwa lengo la kuisaidia katika Uchambuzi wa Muswada huu.

Kwa matangazo hayo, Wadau walifika na walipewa fursa ya kusikilizwa wakiwasilisha maoni yao. Aidha, baadhi ya Wadau waliwasilisha maoni yao kupitia Ofisi ya Katibu wa Bunge. Orodha ya Taasisi hizo ni kama ifuatavyo:

- (a) Chama cha Wanasheria Tanganyika (Tanganyika Law Society-TLS),
- (b) TWaweza,
- (c) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC),na
- (d) Tangible Initiatives For Local Development Tanzania-TIFLD.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wadau wote kwa ushirikiano wao kwa kuisaidia Kamati kuulewa na kuuchambua Muswada huu kwa ufanisi mkubwa.

2.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia masuala ya awali katika utangulizi wa Taarifa hii, napenda kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maoni ya Kamati ambayo yametokana na maelezo ya Serikali pamoja uchambuzi wa Kamati katika Sehemu na Ibara mbalimbali za Muswada huu.

2.1 Maelezo ya Jumla kuhusu uchambuzi wa Muswada

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia na kufanya uchambuzi wa Sehemu Kumi na Tano (15) za Muswada zenye Ibara Sitini na Nne (64) na vifungu vyote vya Sheria vinavyopendekezwa kurekebisha .

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi wa Muswada uliofanywa na Kamati, kwa kupitia Ibara zote zinazopendekeza marekebisha katika Sheria kuu husika, Kamati inapenda kutoa maoni kuwa, kwa ujumla maudhui ya Muswada huu yana tija kwa taifa na endapo mapendekezo ya marekebisha yatapitishwa na kuwa Sheria yatasaidia kuondoa mapungufu yaliyopo katika Sheria hizo.

Hivyo, Kamati imeridhia marekebisha yanayopendekezwa kwa kila Sheria inayorekebisha katika Muswada huu, na inaipongeza Serikali kwa kubainisha upungufu katika sheria husika na kuandaa mapendekezo ya kuboresha yaliyowasilishwa katika Muswada huu, na ambayo yameridhiwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na Kamati kuridhishwa na maudhui pamoja na mantiki ya Marekebisha yanayopendekezwa kwakila Sheria husika, ilibaini baadhi ya dosari za kiuandishi katika jumla ya Ibara 13 za baadhi ya Sheria. Ibara hizo zenye dosari za kuandishi ni pamoja na Ibara ya 17, 26, 30, 40, 42, 47, 52, 53, 56,57,58,60 na 64. Baada ya kubaini dosari hizo Kamati ilipendekeza Marekebisha yafanyike katika Ibara za Sheria husika kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisha lililoletwa na Serikali.

2.2 Masuala Matatu Mahsus katika Muswada;

Mheshimiwa Spika, kupitia vikao vya kupokea na kujadili maoni ya Wadau pamoja na vikao vya Majadiliano na Serikali kuhusu Muswada huu, Kamati ilibaini masuala mahsus ambayo kwa upekee wake. Masuala hayo ni:-

a) Waziri kupewa mamlaka ya kuwateua Wenyeviti wa Bodi badala ya Mamlaka hayo kubaki kwa Rais kama ilivyo kwenye sheria nyingine. Suala hilo limebainika katika Ibara ya 13 ya Sheria ya **The Dairy Industry Act, CaP 262** na Ibara ya 38 ya Sheria ya **The Meat Industry Act, CaP 421**.

b) Mabadiliko ya mfumo wa uwakilishi ndani ya Chama cha Wanasheria wa Tanganyika kwenye vikao vya juu vya maamuzi, ambapo baadhi ya marekebisha yanayopendekezwa katika Ibara 47 ya Sheria ya **The Tanganyika Law Society Act, Cap.307**, yamependekeza dhana ya uwakilishi wa kikanda bila kuweka uwiano wa uwakilishi huo kwa kuzingatia uwiano wa Idadi ya Wanachama kwa baadhi ya Mikoa na Kanda zenye Wanachama wengi; na

c) Kuwepo kwa hofu ya kuingiliana kwa majukumu ya Muhimili wa Serikali Kuu na Mahakama, ambapo marekebisha katika Ibara ya 59 ya Sheria ya **The Tanganyika Law Society Act, Cap.307**,

inampa Waziri ambaye ni sehemu ya Serikali Kuu kuingilia kumbukumbu za vikao vya ndani vya Mkutano Mkuu wa TLS.

Mheshimiwa Spika, pamoja na masuala mengine muhimu yaliyobainika katika Muswada huu, Kamati iliweza kujadili masuala hayo mahsusi kwa kufanya uchambuzi wa kina wa kimantiki kwa kupima malengo ya Serikali sambamba na matamano ya Wadau wa Sekta ya Sheria nchini. Aidha, Kamati ilikwenda mbali kwa kulinganisha hali halisi ya mabadiliko katika sekta ya Sheria nchini kutoka Mwaka 1954 hadi sasa, na hatimaye kufanya maamuzi kwa kupendekeza maboresho katika baadhi ya Ibara pamoja na kuridhia baadhi ya mapendekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifikia hatua hiyo baada ya kupokea na kujadili maelezo ya ziada kutoka Serikalini yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tarehe 23 Januari, 2020.

2.3 Maoni na Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini baadhi ya dosari na kupendekeza yafuatayo:-

a) Katika Ibara ya 17 Kamati inapendekeza kuongeza Kifungu kipa cha 33A kinachopendekeza kuanzisha Maabara ya Maziwa kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho.

b) Katika Ibara ya 45 inayopendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 108 cha Sheria ya **The Probate And Administration of Estates Act, (Cap.352)**, kwa kuongeza kifungu kidogo cha (3) kinachoweka katazo la kugawa ardhi au nyumba kwa mtu ambaye si raia wa Tanzania kwa njia ya mirathi, Kamati inapendekeza kifungu hicho kifutwe ili Serikali ipate muda wa kujiandaa kuleta marekebisho yenye kuzingatia masuala mbalimbali yenye tija kwa Serikali na Wananchi kwa ujumla.

c) Katika Ibara ya 52 inayopendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 15 cha Sheria ya TLS, kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) na kukiandika upya ili kuboresha muundo wa Baraza la Uongozi wa TLS, Kamati inapendekeza Katika kifungu kidogo cha 15(6) kufuta maneno "expiration of tenure" na badala yake kuweka maneno "**swearing in of the new members of the Council**".

Hivyo, Kifungu hicho kosomeke:

"The president, vice-president, honorary treasurer and others members of the members of the council shall assume office immediately after being sworn-in and hold office until the swearing in of new members of the council".

Mheshimiwa Spika, mapendekezo hayo yamezingatiwa na Serikali kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho

d) Katika Ibara ya 53 inayopekufanya marekebisho katika Kifungu cha 16 cha Sheria ya TLS, kwa kufuta na kuandika upya maudhui yake kwa lengo la kuboresha madaraka na majukumu ya Baraza, kwa Kuongeza aya mpya ya 16(j) inayoweka masharti ya utaratibu wa kutunga kanuni ambacho kinasomeka: **16(j) make regulations for governance and management of the Sekretariat**.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo hayo yamezingatiwa kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho.

e) Katika Ibara ya 59 inayopendekeza kurekebisha Kifungu cha 28 cha Sheria ya TLS, kwa kubadilisha maudhui ya kifungu hicho kuwa maudhui ya kifungu cha 28(1) na kuongeza kifungu kidogo kipya cha 28(2), Kamati inapendekeza maneno „Kumbukumbu za Mikutano ya Chama yafutwe, na badala yake kuandikwe maneno „taarifa za Mwaka , ili kulinda uhuru wa uendeshaji wa shughuli za chama pasipokuingiliwa na serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeridhia mapendekezo ya Kamati kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho.

f) Katika Ibara ya 64 inayopendekeza kurekebisha Kifungu cha 28 cha Sheria ya **The Trustees' Incorporation Act, (Cap.318)** kwa kubadilisha maudhui ya kifungu hicho kuwa maudhui ya kifungu cha 28(1) na kuongeza kifungu kidogo kipya cha 28(2), Kamati inapendekeza kuongeza maneno mengine kwenye maneno yanayopendekezwa kuingizwa katika Kifungu cha 8(1). Maneno yanayopendekezwa kuongezwa ni: **securities, stock, or any other property.**

Mheshimiwa Spika, mapendekezo hayo yamezingatiwa na Serikali kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho.

2.3.1 Mapendekezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ya jumla ambayo muhimu yakaboreshwa kwa lengo la kuleta ufanisi wa kutosha kwenye sekta husika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika,

a) KWA KUWA, imebainika wazi kuwa, tasnia ya Nyama na Maziwa imeendelea kukua siku hadi siku pia ni moja ya vitega uchumi muhimu na endelevu hapa nchini;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa chombo mathubuti chenye mamlaka kamili ya kusimamia na kuratibu tasnia za Nyama na Maziwa zinazozidi kupanuka kwa kasi kunaweza kuathiri mchango wa tasnia hiyo katika Uchumi endelevu wa Taifa,

HIVYO BASI, Kamati inashauri kuwa, Serikali ianze kujipanga kuanza na kukamilisha mchakato wakuunda chombo Kimoja mathubuti zaidi ya Bodi za ushauri, ambacho kitaisaidia Serikali katika kusimamia na kuratibu tasnia ya Nyama na Maziwa nchini ili tasnia hizo ziwe na tija stahiki katika kuchangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika,

b) KWA KUWA, imebainika kuwa, Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika imekuwepo tangu mwaka 1954, wakati wa utawala wa Kikoloni,

NA KWA KUWA, ni ukweli usiopingika kuwa, taaluma hiyo imekuwa ikikua na kuimarika kila mwaka kiasi cha kuendelea kuongezeka Idadi ya Wanataaluma hao;

NA KWA KUWA, ongezeko hilo la wanataaluma sambamba na mabadiliko mbalimbali katika Sekta ya Sheria haviwezi kuratibiwa na marekebisho madogo ya Sheria hayawezi kuleta mabadiliko makubwa yanayotakiwa kwa sasa,

HIVYO BASI, Kamati inashauri kuwa, Serikali ijipange vizuri na kuanza mchakato Jumuishi wa kuja na Sheria Mpya ya Chama cha Wanasheria Tanganyika, kwa lengo la kukiwezesha Chama hicho kujijendesha kwa kuzingatia mahitaji ya nchi na Kimataifa yaliyopo kwa sasa, kwa ustawi wa taaluma ya Sheria na kwa maendeleo edelevu ya usimamizi na utetezi wa utoaji haki nchini.

3.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali ili kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia kazi Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kumtambua na kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Prof. Adelardus Kilangi, pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati ulioiwezesha Kamati kukamilisha Uchambuzi wa Muswada huu kwa wakati. Aidha, Kamati inatambua na kumshukuru kila Waziri na Watendaji wake waliofika mbele ya Kamati kwa lengo la kuisaidia Kamati kukamilisha kazi yake kwa ufanisi mkubwa na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa weledi na umahiri wao waliouonesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa Mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. **Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu rasmi za Bunge (HANSARD).**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – **Makamu /Mwenyekiti**
3. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb-Mjumbe;
4. Mhe. Makame Mashaka Fom, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Susan Peter Maselle, MB - Mjumbe;-
12. Mhe. Alfredina Apilinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
13. Mhe. Latifah Hassan Chande, Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Ally Abdulla Saleh, Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi, Mb-Mjumbe;
16. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
18. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb - Mjumbe;
21. Mhe. Emmanuel A. Mwakasaka, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Dkt. Susan Alphonse Kolimba, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususan Katibu wa Bunge **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili, Wanasheria Wasaidizi wa Bunge, Ndg. Mossy Lukuvi, Ndg. Hawa Manzurya na Ndg. Thomas Shawa, Makatibu wa Kamati Ndg. Stanslaus Kagisa na Ndg. Angela Henry Shekifu, pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Rahel Masima waliofanikisha kazi ya Uchambuzi na uratibu wa shughuli za Kamati kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA
28 JANUARI, 2020

MWENYEKITI: Ahsante sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Nagma Murtaza Giga umewasilisha vizuri Maoni ya Kamati tunakushuru sana. *(Makofi)*

Tunaendelea tupate maoni ya Kambi ya Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada huu, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani naomuona Mheshimiwa Salome Makamba una dakika zizozidi 20. *(Makofi)*

MHE. SALOME W. MAKAMBA - MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru mbele yako ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 8) wa mwaka 2019 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.8) Act, 2019)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na nguvu kuweza kuingia mwaka huu wa 2020 nikiwa na utimamu wa mwili na akili, pia kuwapa na kuwatakiya heri ya Mwaka mpya Wabunge wenzangu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muendelezo huo nitoe pongezi kwa uongozi mzima wa Chama changu kwa kufanikisha Mkutano Mkuu wa Chama na hatimaye kupatikana kwa uongozi mpya kuanzia ngazi za Mabaraza ya Chama na chama kwa ujumla. Nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, Mbunge wa Jimbo la Hai kwa kuchaguliwa tena na wajumbe wapatao elfu mbili wa Mkutano Mkuu wa CHADEMA kuwa Mwenyekiti wa Chama chetu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Tundu Antipas Lissu kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti kwa upande wa Bara na Mheshimiwa Issa Mohamed kwa upande wa Zanzibar. Pia nimpongeze Mheshimiwa John John Mnyika (Mtemi - Malonja) kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa CHADEMA kwa kipindi kijacho cha miaka mitano, sambamba na Manaibu wake Ndugu Benson Singo Kigaila na Ndugu Salum Mwalimu. Hongereni sana kwa kuaminiwa na wanachama wa CHADEMA katika kuhakikisha tunafikia malengo ya chama chetu ya kuchukua dola kupitia sanduku la kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki kama nitashindwa kuwatambua na kuwashukuru Mwenyekiti na Katibu wa Baraza la Wanawake la CHADEMA waliopewa tena dhamana ya kutufikisha pale ambapo tunatakiwa kufika kwa mujibu wa mpango mkakati wetu. Mheshimiwa Halima James Mdee, Mwenyekiti na pia Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi la Kawe na Katibu wake Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum. Aidha, kipekee niwapongeze Waheshimiwa Esther Nicolaus Matiko, Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini na Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kanda ninayotoka ya Serengeti. *(Makofi)*

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwisho lakini kwa umuhimu nitoe pole kwako pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Rashid Ajal Akbar, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, nasema Mwenyezi Mungu azidi kutupa roho ya ustahimilivu na pia tufahamu kuwa sisi sote njia yetu ni moja na hakuna ajuae muda wala saa atakayoitwa na Mwenyezi Mungu.

Napenda kuwakumbusha waheshimiwa viongozi wote mliomo humu ndani ya Ukumbi wa Bunge, kuwa Ibara ya 74(14) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kwamba; "Itakuwa ni marufuku kwa watu wanaohusika na uchaguzi kujiunga na chama chochote cha siasa. Isipokuwa tu kwamba kila mmoja wao atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika Ibara ya 5 ya Katiba hii". Kwa nukuu hii ya Katiba naomba viongozi kujitafakari je ni kweli Katiba tuliyo apa kuilinda tunailinda au tunaivunja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa utangulizi huo wa pongezi na salamu za mwaka mpya, sasa niangalie hoja iliyo mbele yetu inayohusu Marekebisho ya Sheria Mbalimbali zinazoletwa kupitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 8 wa mwaka 2019 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.8) Act, 2019)*.

Muswada huu unapendekeza Marekebisho ya Sheria 14 ambazo ni:

- (1) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sura ya 33;
- (2) Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20;
- (3) Sheria ya Tasnia ya Maziwa, Sura ya 262;
- (4) Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura ya 245;
- (5) Sheria ya Uvuvi, Sura ya 279;
- (6) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri Dhidi ya Serikali, Sura ya 5;
- (7) Sheria ya Mtoto, Sura ya 13;
- (8) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287;
- (9) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288;
- (10) Sheria ya Tasnia ya Nyama, Sura ya 421;
- (11) Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16;
- (12) Sheria ya Usimamizi wa Mirathi, Sura ya 352;
- (13) Sheria ya Chama cha Mawakili Tanganyika, Sura ya 307; na
- (14) Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura ya 318.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mabadiliko hayo ya sheria kuna Sheria ya Tasnia ya Maziwa, Sheria ya Uvuvi na Sheria ya Tasnia ya Nyama kwa maana nyingine ni kuwa mabadiliko katika sheria zinazoendesha sekta ya mifugo na uvuvi. Mifugo na Uvuvi ni sekta muhimu sana kwa uchumi na maendeleo ya nchi na Watanzania kwa ujumla. Sekta ndogo ya mifugo

inaweza kuchangia kwa kiwango kikubwa katika uchumi wa nchi kama uwekezaji utafanyika inavyotakiwa. Sekta hii inaajiri takribani 50% ya Watanzania ambayo ni watu takribani milioni 27 na inachangia 6.9% kwenye Pato la Taifa. Shughuli za Uvuvi zinachangia 2.2% ya Pato la Taifa. Kwa baadhi ya maeneo ya nchi yetu Uvuvi ndio shughuli kuu ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 sekta ya uvuvi imepata zaidi ya shilingi bilioni 25 na hadi kufika mwezi Machi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 walikusanya zaidi ya bilioni 23. Takwimu za hali ya uchumi za mwaka 2017 zinaonesha kuwa mapato yanayotokana na shughuli za uvuvi hapa nchini huchangia 2.2% ya pato ghafi la Taifa na tasnia nzima ya uvuvi inachangia 10% ya mauzo nje ya nchi kwa mujibu wa taarifa ya mwaka ya uvuvi ya 2014. Sekta hii ya uvuvi inaweza kufanya vizuri zaidi kwa kuivusha Serikali katika hali ya umasikini kama ingepewa kipaumbele kinachostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeonesha umuhimu wa sekta hii inavyofanyiwa marekebisho katika uchumi wetu na ambavyo inategemewa na Watanzania walio wengi, hivyo jambo lolote linalohusiana na sheria za uendeshaji wake ni lazima na muhimu ushirikishwaji wa wadau kuwa ni jambo la kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba Serikali haifanyi biashara ya uvuvi, haina mashamba ya mifugo kiasi cha kuzalisha nyama kwa utoshelevu wake pia Serikali haina viwanda vya maziwa. Wanaojihusisha na ambao ni wadau wakuu wa sekta hii ni watu binafsi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, kwa muktadha huo Kambi Rasmi ya Upinzani katika mapitio ya marekebisho ya sheria hizi tajwa itajaribu kuangalia ushirikishwaji wa sekta binafsi katika usimamizi wa sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya sheria hizo za uvuvi na mifugo kuna sheria nyingine ambazo nazo ni muhimu sana katika kuhakikisha kuwa wananchi nao wanatambuliwa na kupewa haki zao za msingi pale inapotokea sintofahamu baina yake na Serikali. Tukumbuke kwamba Serikali haiwezi kuwepo bila ya uwepo wa raia na raia ndio wanaotoa uhalali wa uwepo wa Serikali. Sheria hizo ni Sheria za Wakala wa Serikali, Sura ya 245; Sheria ya Mwenendo wa Mashauri Dhidi ya Serikali; Sheria ya Serikali za Mitaa na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji). (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria zilizotajwa hapo juu ni sheria ambazo zinahusisha moja kwa moja na wananchi na tukumbuke kwamba watendaji au wasimamizi wa sheria hizo ni binadamu na binadamu anaweza kutenda kwa kuangalia ubinafsi na hivyo kupindisha matakwa ya sheria na kanuni. Inapotokea hivyo muathirika wa maamuzi hayo anakuwa ni mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi inasikitika mno kwamba sheria nyingi ambazo tunazitunga ni kujitahidi kulinda Serikali na watendaji wake badala ya kuangalia maslahi ya wananchi kwa upana wake, kama Serikali kupitia taasisi zake imezembeka na kusababisha hasara kwa mwananchi tunatunga sheria zenye ukiritimba hadi mhusika apate haki yake na hivyo kusahau kabisa kuwa muda ni rasilimali, unavyomchelewesha mdai kupata haki yake unazidi kumtia umaskini. Jambo hili sio sahihi kabisa kwa Serikali inayojitanabaisha kuwa inajali wananchi wake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya vifungu katika muswada; Kambi Rasmi ya Upinzani itapitia marekebisho ya vifungu katika sheria zile tu ambazo imeona kuna umuhimu wa kufanyiwa marekebisho. Sheria ya Chama cha Mawakili Tanganyika, Sura ya 307; kifungu cha

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

51 cha muswada kinarekebisha kifungu cha 9 cha sheria mama kwa kufuta neno *elect* na badala yake kuongeza neno *appoint*.

Kifungu hicho cha 9 cha sheria mama kinahusu wanachama wa heshima kwa wanachama wa *TLS* (Chama cha Mawakili). Aidha, sheria ilikuwa inalipatia nguvu na mamlaka Baraza kuchagua mjumbe wa heshima kadri Baraza la Uongozi litakavyoona inafaa. Kwa mabadiliko ya sasa, muswada unapendekeza huyo mjumbe asichaguliwe na badala yake ateuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaona kwamba demokrasia ya kuchagua ni nzuri zaidi kuliko uteuzi. Hii inatokana na ukweli kwamba mjumbe anayechaguliwa anapitia mchakato mbalimbali hadi kuchaguliwa kwake. Sababu nyingine tunayoona ni bora kifungu hiki kibaki kama kilivyokuwa, hakuna sababu zozote ambazo zilikuwa zinaleta ugumu wa kuchaguliwa kwa wajumbe husika, kubadilishwa kwa kifungu hiki ili wajumbe wateuliwe kinaleta taswira ya kuogopa dhana ya uchaguzi na hivyo kuashiria nia ovu ambayo imejificha katika mabadiliko haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 52 cha muswada kinafanya marekebisho ya kifungu cha 15 cha sheria mama, kifungu kipya kinapendekeza na kinaingiza mambo mawili mapya, kwanza, kinaongeza idadi ya wajumbe wa Baraza la Uongozi kutoka wajumbe saba hadi nane baada ya Rais, Makamu wa Rais pamoja na Mweka Hazina, lakini kifungu hiki kinafuta dhana ya Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kinachofutwa kinahusu Baraza la Uongozi la Chama cha Mawakili, sitakisoma kwa *interest* ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano Mkuu wa mwaka wa Mawakili unafanya kazi nyingi, uchaguzi ni miongoni mwa shughuli za mkutano husika, inashangaza kwamba Serikali sasa, inataka Mawakili wanaokutana kujua maendeleo ya chama chao kwamba waanze kufanya hivyo kwa njia ya uwakilishi, kama ambavyo kifungu cha 57 cha muswada huu kinachofanya marekebisho cha 21 cha sheria mama kwa kukifuta na kuandika upya kama kilivyoielezwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo sababu nyingi ambazo zinatolewa kuhalalisha mapendekezo hayo, sababu ambazo hazina msingi wowote, tofauti na dhamira ya Serikali kujaribu kudhibiti Chama cha Mawakili, sababu hizo ni pamoja na gharama za mkutano, wingi wa Mawakili na sababu zingine ambazo hazisemwi wazi. (*Makofi*)

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunapenda kuikumbusha Serikali kwamba ziko nchi ambazo idadi ya Mawakili ni wengi kuliko idadi ya Mawakili ambao Tanzania Bara tunao, lakini wanakutana na kujadili masuala yanayohusu chama chao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo, zinaonesha kwamba idadi ya Mawakili hawazidi 9,000 wakati wenzetu majirani kwa mfano nchi ya Kenya, idadi ya Mawakili kwa nchi hiyo ni 15,000 lakini Mawakili wote hao huhudhuria mkutano mkuu wa mwisho wa mwaka na kwa mujibu wa kifungu cha 16(2) cha Sheria ya Mawakili wanaruhusiwa kukutana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchini Nigeria idadi ya Mawakili ni 105,406 na wote huhudhuria Mkutano Mkuu wa Mawakili. Hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 10 ya Katiba ya Chama cha Mawakili na Nigeria vivo hivyo. Kutokana na mifano hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufuta katika Muswada huu vifungu vyote vinavyotaka Mkutano Mkuu wa Mawakili

kufanyika kwa uwakilishi na badala yake sheria iwapatie fursa Mawakili kukutana na kujadili mambo yanayohusu chama chao, kwa utaratibu unaotumiwa na Chama cha Mawakili kipindi cha mikutano hiyo zikiwemo gharama za fedha na gharama za Mawakili wenyewe. Kwa mantiki hiyo Kambi Rasmi haioni mantiki yoyote ya kuwazuia Mawakili kushiriki mkutano wao kwa lengo la kujadili mambo yanayohusu chama chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 57 cha muswada kinarekebisha kifungu cha 21 cha sheria mama kwa kukifuta na kukiandika upya. Kifungu hicho kinahusu Mkutano Mkuu wa mwaka yaani *Annual General Meeting*. Kwa mujibu wa kifungu hiki, Mkutano huu unapendekezwa kuwa na wajumbe 591, miongoni mwa wajumbe hao wanachama wa kuchaguliwa wakiwa 123 sawa na 20% ya wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa mwaka, huku wajumbe wa kuteuliwa wakiwa 468 sawa na 80% ya wanachama wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia, kifungu cha 57 cha muswada kinarekebisha kifungu cha 21 cha sheria mama kwa kukifuta na kukiandika upya kifungu hicho kinachohusu Mkutano Mkuu wa mwaka. Kwa mujibu wa kifungu hiki, Mkutano Mkuu unapendekezwa kuwa na wajumbe 591, miongoni mwao wajumbe wa kuchaguliwa na wanachama ni 123 sawa na 20% ya wajumbe wote wa mkutano mkuu huku wajumbe wa kuteuliwa wakiwa 468 sawa na 80% ya wanachama wote. Kwa vyovyote vile wajumbe ambao hawakuchaguliwa na wanachama hawawezi kulinda au kutetea maslahi ya wanachama ambao ni Mawakili na badala yake watalinda na kutetea maslahi ya mamlaka zinazowateua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, madhara ya kifungu kipya cha 21(4) ni kwamba idadi ya wajumbe wa kuchaguliwa 123 haibadiliki wakati idadi ya wajumbe wa kuteuliwa inaweza kuongezeka kutokana na mamlaka za uteuzi kutoweka idadi ya mwisho ya wajumbe wa kuteua. Matokeo yake sasa, kutokana na kuzidi kuongezeka kwa idadi ya Mawakili, itafika sehemu na siyo mbali, idadi ya wajumbe wa kuchaguliwa itakuwa chini ya 1% ya wajumbe wote wa Mkutano Mkuu, jambo ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona halina afya kwa ustawi wa Chama cha Mawakili hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya uteuzi ambayo yamewekwa katika kifungu cha 21(4)(c) cha Muswada huu kinaweza kutumika vibaya na kanda kwa kanda kushindana kuunda kamati mbalimbali ili kupata wajumbe wa mkutano mkuu zaidi ya kanda nyingine. Matumizi hayo mabaya yana uwezekano wa kutokea zaidi kwa kanda ya Dar es Salaam ambayo hadi sasa kwa takwimu za Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaonesha Kanda hii ya Dar es Salaam ina takribani 70.12% ya wanachama wote wa Chama cha Mawakili. Hali hii pia inaweza kulikumba Baraza la Uongozi chini ya kifungu kipya kinachopendekezwa cha 21(4)(b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 21(4)(g) cha Muswada, kinalipa baraza la uongozi mamlaka yasiyokuwa na ukomo ya kuteua wajumbe wa Mkutano Mkuu wa mwaka, hata kama wajumbe hao siyo wanachama wa Chama cha Mawakili. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashangaa ni kwa namna gani Serikali wanaweza kuwa na muswada ambao una kifungu kama hiki, tena kwa sheria ya Chama cha Mawakili ambao ni wadau wakubwa wa sheria hapa nchini. Kwa udhaifu huo, basi Kambi Rasmi inapendekeza kwamba kifungu cha 21(5) kiruhusu Mawakili wote kuhudhuria mkutano mkuu wa mwaka ili kuwapatia haki yao ya kushiriki na kuamua mambo yanayohusu chama chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyodokeza hapo awali, zipo nchi nyingi nimezieleza hapo chini zinazoonyesha Mawakili wanahudhuria mikutano yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, kifungu cha 6 cha muswada kinachoongeza kifungu kipya cha 64 katika sheria, kifungu kidogo cha 64A(2)

sitakisoma kwa *interest* ya muda, katika kifungu hiki hoja yetu ni kwamba kwa kuwa sheria inatambua maridhiano baina ya pande mbili nje ya mahakama, hivyo basi badala ya jukumu la kutayarisha kanuni na taratibu na miongozo kuwa kwa Mheshimiwa Waziri ni vyema jukumu hilo likabaki chini ya mhimili wa Mahakama kwa maana ya *Chief Justice* (Jaji Mkuu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Tasnia ya Maziwa, kama ambavyo tumeainisha hapo juu kuhusu umuhimu wa tasnia hii ya maziwa kwenye jamii tunaona kwamba katika Muswada wa Serikali wamebadilisha kifungu cha 3 cha sheria mama na kuleta mapendekezo mapya ambayo yanaongeza tafsiri ya neno maziwa. Pamoja na nia njema, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza na kulikumbusha Bunge lako tukufu na Serikali kuwa changamoto kubwa ya wafugaji na wafanyabiashara wa maziwa siyo uzalishaji tu bali kukuza thamani ya zao la maziwa na masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi. Hivyo basi kupanua mawanda ya tafsiri ya maziwa wa wajumuishe maziwa yatokanayo na mifugo na mazao na hili linaweza lisiwe suluhisho, hoja ni kuongeza thamani na kutafuta masoko ya maziwa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha katika kifungu cha 10B imetolewa tafsiri ya neno *inspector* kuwa ni mtu atakayeteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 33B. Ni bahati mbaya sana kwamba Sheria hii ya Maziwa katika nyanja ya ubora ya kuanzia uzalishaji, vifaa, ufungashaji vinaratibiwa na Sheria ya TBS. Kwa marekebisho haya yanayopendekezwa na Serikali katika sheria hii ina maana tunakuwa na wakaguzi wa maziwa na bidhaa za maziwa hivyo kutakuwa na wakaguzi wa aina mbili kwa bidhaa moja, sambamba na uwepo wa maabara mbili za taasisi zitakazokuwa kuwa chini ya sheria mbili tofauti zitakazokuwa zinashughulikia jambo moja. Kwa mustakabali mwema wa uendeshaji wa tasnia ya maziwa ni muhimu sana sheria hii ikawa mipaka ya kiutendaji baina ya watendaji waajiriwa wa TBS japokuwa Sheria ya Maziwa bado inatambua Sheria ya TFDA katika kufanya *inspection*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 13 cha muswada kinachofuta na kuandika upya kifungu cha 9 cha sheria mama, kinahusu uundwaji wa Bodi ya Tasnia ya Maziwa. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa wadau wa sekta binafsi washirikishwe kwa kiasi kikubwa kwani wao ndiyo wazalishaji wakubwa wa maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Wakala wa Serikali; kifungu cha 19 cha Muswada kinachorekebisha kifungu cha 3 cha sheria mama na kuongeza kifungu cha 7 na kifungu kidogo kipyaa cha 8, sitasoma kwa ajili ya muda, Bunge limekuwa likisisitiza umuhimu wa kutenganisha malalamiko dhidi ya Mawakala wa Serikali na Serikali yenyewe hasa kwenye mashtaka ambayo wakala (*agencies*) wameyafanya kwa uzembe au kutowajibika. Kitendo cha Wakili Mkuu wa Serikali kuwa sehemu ya mashauri yote ambayo wakala anaweza kushtakiwa, kinatoa taswira au kuleta dhana kuwa Wakili Mkuu wa Serikali amewekwa pale ili kuhakikisha haki haitendeki au inachelewa kwa wananchi ambao kwa njia moja au nyingine wanakuwa wamenyimwa haki zao na wakala husika. Kambi Rasmi ya Upinzani inalishauri Bunge kutenganisha makosa ambayo Serikali inaathirika moja kwa moja ili kuleta uwajibikaji kwa taasisi zenye mahusiano ya moja kwa moja na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 21 cha muswada kinachorekebisha kifungu cha 8 cha Sheria ya Uvuvi na kufuta vifungu vidogo vya 4 na 5 na kuviandika upya ikisema pale itakapobainika kuna usimamizi mbaya wa tasnia ya uvuvi kutoka kwa Halmashauri, Waziri atasitisha au atapokonya Halmashauri hiyo usimamizi wa sekta ya uvuvi na atamtaarifu Waziri mwenye dhamana wa Serikali za Mitaa uamuzi wake huo na atateua chombo kingine kusimamia sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko wapi dhana ya ugatujaji madaraka kutoka Serikali Kuu? Tunawezaje kupoka madaraka ya usimamizi wa rasilimali za wananchi katika ngazi ya

Halmashauri kwa kosa la uadilifu? Kambi Rasmi ya Upinzani inafahamu kuwa Halmashauri zetu zinaendeshwa na zina mamlaka kamili ya kujiendesha chini ya usimamizi wa Baraza la Madiwani. Pale inapotokea idara ina matatizo, ufumbuzi sio kufuta idara bali kufanya mabadiliko kwa wale wanaoongoza idara hiyo na ukisema unaipokonya usimamizi wa kazi zote zinazohusiana na sekta ya uvuvi, kwa maana nyingine unaondoa hata mapato yaliyokuwa yanaingizwa kutokana na sekta ya uvuvi (*own source*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya yamejaribiwa katika Halmashauri gani na kuona matokeo yake? Tusitunge sheria kama mchezo kwa kubahatisha, hii ni hatari sana kwa uendeshaji wa Halmashauri zetu. Kambi Rasmi inayaona mapendekezo hayo sio tu yanakiuka Sera ya Ugatuuji madaraka, lakini pia ni muendelezo wa kuzipoka Halmashauri vyanzo vyake vya mapato, hasa ikizingatiwa kuna halmashauri ambazo zinategemea Sekta ya Uvuvi...

(Hapa kengele ililia kaushiria kuisha kw amuda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana, ndiyo muda wetu huo.

MHE. SALOME W. MAKAMBA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kwa kuhitimisha ni kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge na Bunge hili tuangalie kwa tafakuri pana marekebisho ya sheria zinazoletwa na ni ukweli kwamba mambo mengi yanayoletwa kupitia Miswada hii yanakuwa na hila na yanaweza kusababisha madhara makubwa katika Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NA.8 YA MWAKA 2019 (THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.8) ACT, 2019) KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI (Chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016)

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kuanza na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na nguvu kuweza kuingia mwaka huu wa 2020 nikiwa na utimamu wa mwili na akili, pia kuwapa/kuwatakia heri ya Mwaka mpya Wabunge wenzangu wote.

2. Mheshimiwa Spika, Katika muendelezo huo nitoe pongezi kwa uongozi mzima wa Chama changu kwa kufanikisha Mkutano Mkuu wa Chama na hatimaye kupatikana kwa Uongozi mpya kuanzia ngazi za Mabaraza ya Chama na Chama kwa ujumla. Nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, Mbunge wa Jimbo la Hai kwa kuchaguliwa tena na wajumbe wapatao elfu mbili wa Mkutano Mkuu wa Chadema kuwa Mwenyekiti wa Chama Chetu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Mheshimiwa Tundu Antipas Lissu kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti kwa Upande wa Bara na Mheshimiwa Issa Mohamed kwa upande wa Zanzibar. Pia nimpongeze Mheshimiwa John John Mnyika (Mtemi- Malonja) kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa CHADEMA kwa kipindi kijacho cha miaka mitano, sambamba na Manaibu wake (Ndugu Benson Singo Kigaila na Ndugu Salum Mwalimu) Hongereni sana kwa kuaminiwa na Wanachadema katika kuhakikisha tunafikia malengo ya chama chetu ya kuchukua dola kupitia sanduku la kura.

3. Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijatenda haki kama nitashindwa kuwatambua na kuwashukuru Mwenyekiti na Katibu wa Baraza la Wanawake wa Chadema waliopewa tena dhamana ya kutufikisha pale ambapo tunatakiwa kufika kwa mujibu wa mpango mkakati wetu, Mheshimiwa Halima James Mdee Mwenyekiti na pia Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi la Kawe na Katibu wake Mheshimiwa Grace Victor Tendega Mbunge wa viti maalum. Aidha kipekee niwapongeze waheshimiwa Esther Nicolaus Matiko (Mb) Jimbo la Tarime Mjini na Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba (Mb) kwa kuchaguliwa kwa Kishindo kuwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kanda ninayotoka ya Serengeti.

Mheshimiwa Spika, Mwisho lakini kwa umuhimu nitoe pole kwako pamoja na waheshimiwa wabunge wote kwa kuondokewa na Mbunge Mwenzetu Mheshimiwa Rashid Ajal Akbar, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, nasema Mwenyezi Mungu azidi kutupa roho ya ustahimilivu na pia tufahamu kuwa sisi sote njia yetu ni moja na hakuna ajuae muda wala saa atakayoitwa na Mwenyezi Mungu.

4. Mheshimiwa Spika, napenda kuwakumbusha waheshimiwa viongozi wote mliomo humu ndani ya Ukumbi wa Bunge, kuwa Ibara ya 74(14) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kwamba;

“Itakuwa ni marufuku kwa watu wanaohusika na uchaguzi kujiunga na Chama chochote cha siasa. Isipokuwa tu kwamba kila mmoja wao atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika Ibara ya 5 ya katiba hii”.

Kwa nukuu hii ya Katiba namba viongozi kujitafakari je ni kweli Katiba tuliyo apa kuilinda tunailinda au tunaivunja?

5. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa utangulizi huo wa pongezi na salaam za mwaka mpya, sasa niangalie hoja iliyo mbele yetu inayohusu marekebisho ya sheria mbalimbali zinazoletwa kupitia muswada wa marekebisho ya sheria mbalimbali namba 8 wa mwaka 2019 **(THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.8) ACT, 2019)**

6. Mheshimiwa Spika, muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho ya sheria kumi na nne (14) ambazo ni:

- i. Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sura ya 33;
- ii. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20;
- iii. Sheria ya Tasnia ya Maziwa, Sura ya 262;
- iv. Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura ya 245;
- v. Sheria ya Uvuvi, Sura ya 279;
- vi. Sheria ya Mwenendo wa Mashauri Dhidi ya Serikali, Sura ya 5;
- vii. Sheria ya Mtoto, Sura ya 13;
- viii. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287;
- ix. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288;
- x. Sheria ya Tasnia ya Nyama, Sura ya 421;
- xi. Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16;
- xii. Sheria ya Usimamizi wa Mirathi, Sura ya 352;
- xiii. Sheria ya Chama cha Mawakili Taganyika, Sura ya 307; na
- xiv. Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura ya 318.

7. Mheshimiwa Spika, katika mabadiliko hayo ya sheria kuna sheria ya Tasnia ya Maziwa, sheria ya uvuvi na sheria ya Tasnia ya Nyama kwa maana nyingine ni kuwa mabadiliko katika

sheria zinazoendesha sekta ya mifugo na uvuvi. Mifugo na Uvuvi ni sekta muhimu sana kwa uchumi na maendeleo ya nchi na Watanzania kiujumla. Sekta ndogo ya mifugo inaweza kuchangia kwa kiwango kikubwa katika uchumi wa nchi kama uwekezaji utafanyika inavyotakiwa. Sekta hii inaajiri takribani 50 % ya watanzania ambayo ni watu takribani milioni 27 na inachangia 6.9 % kwenye pato la Taifa. Shughuli za Uvuvi zinachangia 2.2 % ya pato la taifa. Baadhi ya maeneo ya nchi yetu Uvuvi ndio shughuli kuu ya uchumi.

8. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/18 sekta ya uvuvi imeipatia Serikali shilingi 25,727,659,157.00, na hadi kufikia mwezi Machi kwa mwaka wa fedha 2018/19, Serikali ilikusanya shilingi 23,901,862,510.79. Takwimu za hali ya uchumi za mwaka 2017 zinaonesha kuwa, mapato yaliyotokana na shughuli za uvuvi hapa nchini huchangia 2.2 % ya pato ghafi la Taifa (GDP), na tasnia nzima ya uvuvi inachangia 10 % ya mauzo nje ya nchi kwa mujibu wa Taarifa ya mwaka ya uvuvi ya 2014 (Annual fisheries statistics report 2014). Sekta hii ya uvuvi inaweza kufanya vizuri zaidi kwa kuivusha Serikali katika hali ya umasikini kama ingepewa kipaumbele kinachostahili.

9. Mheshimiwa Spika, tumeonesha umuhimu wa sekta hii inayofanyiwa marekebisho katika uchumi wetu na ambavyo inategemewa na watanzania walio wengi, hivyo jambo lolote linalohusiana na sheria za uendeshaji wake ni lazima na muhimu ushirikishwaji wa wadau kuwa ni jambo la kipaumbele. Tukumbuke kwamba Serikali haifanyi biashara ya uvuvi, haina mashamba ya mifugo kiasi cha kuzalisha nyama kwa utoshelevu wake pia Serikali haina viwanda vya maziwa. Wanaojihusisha na ambao ni wadau wakuu wa sekta hii ni watu binafsi kwa ujumla wake.

10. Mheshimiwa Spika, hivyo basi, kwa muktadha huo Kambi Rasmi ya Upinzani katika mapitio ya marekebisho ya sheria hizo tajwa itajaribu kuangalia ushirikishwaji wa Sekta binafsi katika usimamizi wa sheria hizo.

11. Mheshimiwa Spika, Mbali ya sheria hizo za sekta ya uvuvi na mifugo kuna sheria zingine ambazo nazo ni muhimu sana katika kuhakikisha kuwa wananchi nao wanatambuliwa na kupewa haki zao za msingi pale inapotokea sintofahamu baina yake na Serikali. Tukumbuke kwamba Serikali haiwezi kuwepo bila ya uwepo wa raia na raia ndio wanaotoa uhalali wa uwepo wa Serikali. Sheria hizo ni Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura ya 245; Sheria ya Mwenendo wa Mashauri Dhidi ya Serikali, Sura ya 5; Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287; na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288;

12. Mheshimiwa Spika, Sheria hizo tajwa ni sheria ambazo zinahusiana moja kwa moja na wananchi, na tukumbuke kwamba watendaji au wasimamizi wa sheria hizo ni binadamu na binadamu anaweza kutenda kwa kuangalia ubinafsi na hivyo kupindisha matakwa ya sheria na kanuni, na inapotokea hivyo muathirika wa maamuzi hayo analazimika kumingiza Mwanasheria Mkuu wa Serikali au katika mashtaka yake katika ngazi husika ya Serikali eti ni kulinda mali za Serikali. Suala la msingi mali ya mwananchi ambayo inaweza kuporwa na watendaji wa Serikali italindwa na nani? Tuangalie uhalisia wa mlolongo wa kupambana katika vyombo vya sheria ili haki kupatikana.

13. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika mno kwamba, Sheria nyingi ambazo tunazitunga ni kujitahidi kulinda Serikali na Watendaji wake badala ya kuangalia pia maslahi ya wananchi kwa upana wake, kama Serikali kupitia taasisi zake imezembea na kusababisha hasara kwa mwananchi tunatunga sheria zenye ukiritimba hadi mhusika apate haki yake, na hivyo kusahau kabisa kuwa muda ni rasilimali, unavyomchelewesha mdai kupata

haki yake unazidi kumtia umasikini. Jambo hili sio sahihi kabisa kwa Serikali inayojitanabaisha kuwa inajali wananchi wake.

B. MAPITIO YA VIFUNGU KATIKA MUSWADA NA MAONI YA KAMBI RASMI

14. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani itapitia marekebisho ya vifungu katika sheria zile tu ambazo imeona kuna umuhimu wa kufanyiwa marekebisho.

i. Sheria ya Chama cha Mawakili Taganyika, Sura ya 307

15. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 51 cha muswada kinarekebisha kifungu cha 9 cha sheria mama kwa kufuta neno “**elect**” na badala yake kuingiza neno “**appoint**”. Kifungu hicho cha 9 cha sheria mama, kinahusu uanachama wa heshima kwa wanachama wa TLS. Aidha sheria ilikuwa inalipatia nguvu na mamlaka baraza kuchagua mjumbe wa heshima kadri baraza la uongozi litakavyoona inafaa. Kwa mabadiliko ya sasa, muswada unapendekeza mjumbe huyo asichaguliwe na badala yake ateuliwe.

16. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaona kwamba, demokrasia ya kuchagua ni nzuri zaidi kuliko uteuzi. Hii inatokana na ukweli kwamba, mjumbe anayechaguliwa anapitia michakato mbalimbali hadi kuchaguliwa kwake. Sababu nyingine tunayoona ni bora kifungu hiki kibaki kama kilivyokuwa, hakuna sababu zozote ambazo zilikuwa zinaleta ugumu wa kuchaguliwa kwa wajumbe husika, kubadilishwa kwa kifungu hiki ili wajumbe wateuliwe kinaleta taswira ya kuogopa dhana ya uchaguzi na hivyo kuashiria nia oву ambayo imejificha katika mabadiliko haya.

17. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 52 cha muswada kinafanya marekebisho kifungu cha 15 cha sheria sheria mama, kifungu kipyakina chopendekezwa kinaingiza mambo mawili mapya, kwanza, kinaongeza idadi ya wajumbe wa baraza la uongozi kutoka wajumbe 7 hadi 8 baada ya Rais, makamu wa Rais pamoja na Mweka hazina, lakini pia kifungu hiki kinafuta dhana ya Mkutano Mkuu wa Chama Cha mawakili.

18. Mheshimiwa Spika, kifungu kinachofutwa kinahusu baraza la uongozi la chama cha mawakili, kilikuwa kinasomeka kama ifuatavyo “*For or the proper management of the affairs of the Society, there shall be a council consisting of a President, a vice President, a Treasure and seven others persons; all whom shall be members of the Society and elected annually by the Society in a general meeting*”. Kifungu kipyakina chopendekezwa sasa kinasema; “*for the purpose of governance of the affairs of the society, there shall be a council consisting of a President, Honorary Treasure and eight other members of the society duly elected during the General election*”

19. Mheshimiwa Spika, mkutano mkuu wa mwaka wa mawakili unafanya kazi nyingi, uchaguzi ni miongoni mwa shughuli za mkutano husika, inashangaza kwamba Serikali sasa, inataka mawakili wanaokutana kujua maendeleo ya chama chao, kwamba waanze kufanya hivyo kwa njia ya uwakilishi, kama ambavyo kifungu cha 57 cha muswada huu kinachofanyia marekebisho kifungu cha 21 cha sheria mama kwa kukifuta na kukiandika upya kinavyosema katika kifungu cha 21(3).

20. Mheshimiwa Spika, ziko sababu nyingi ambazo zinatolewa kuhalalisha mapendekezo hayo, sababu ambazo hazina msingi wowote, tofauti na dhamira ya serikali kujaribu kuthibiti chama cha mawakili. Sababu hizo ni pamoja na gharama za mkutano mkuu wa mawakili, wingi wa mawakili na sababu nyingine ambazo hazisemwi wazi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunapenda kuikumbusha serikali kwamba, ziko nchi ambazo idadi ya mawakili ni wengi kuliko

idadi ya mawakili ambao Tanzania Bara tunao lakini wanakutana kujadili maswala yanayohusu chama chao.

21. Mheshimiwa Spika, taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo, zinaonesha kwamba idadi ya mawakili hawazidi 9,000 wakati wenzetu majirani kwa mfano nchi ya Kenya, Idadi ya mawakili kwa nchi hiyo ni 15,000 lakini mawakili wote hao huhudhuria mkutano mkuu wa mwisho wa mwaka kwa mujibu wa kifungu cha 16(2) cha sheria ya mawakili wa Kenya, yaani "section 16(2) of the law society of Kenya, Act, 2004". Nchini Nigeria idadi ya mawakili ni 105,406 na wote huhudhuria mkutano mkuu wa mawakili na hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 10 ya katiba ya chama cha mawakili wa Nigeria yaani Article 10 of the constitution of Nigerian Bar Association, 2015.

22. Mheshimiwa Spika, kutokana na mifano hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kufuta katika muswada huu vifungu vyote vinavyotaka Mkutano mkuu wa mawakili kufanyika kwa uwakilishi na badala yake sheria iwapatie fursa mawakili kukutana na kujadili mambo yanayohusu chama chao, kwa utaratibu unaotumiwa na chama cha mawakili kipindi cha Mikutano hiyo, zikiwemo gharama za fedha ni gharama za mawakili wenyewe, kwa mantiki hiyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni mantiki yoyote ya kuwazuia mawakili kushiriki Mkutano Mkuu kwa lengo la kujadili mambo yanayohusu chama chao.

23. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 57 cha muswada kinarekebisha kifungu cha 21 cha sheria mama kwa kukifuta na kukiandika upya. Kifungu hicho kinahusu Mkutano mkuu wa mwaka, yaani "Annual General Meeting". kwa mujibu wa kifungu hiki, Mkutano Mkuu unapendekezwa kuwa na jumla ya wajumbe 591, miongoni mwao wajumbe wa kuchaguliwa na wanachama wa TLS wakiwa ni 123 sawa na 20% ya wajumbe wote wa mkutano Mkuu wa mwaka, huku wajumbe wa kuteuliwa wakiwa 468 sawa na 80% ya wanachama wote, kwa vyovyote vile wajumbe ambao hawakuchaguliwa na wanachama hawawezi kulinda au kutetea maslahi ya wanachama ambao ni mawakili na badala yake watalinda na kutetea maslahi ya mamlaka zinazowateua.

24. Mheshimiwa spika, kama hiyo haitoshi, madhara ya kifungu kipya cha 21(4) ni kwamba idadi ya wajumbe wa kuchaguliwa 123 haibadiliki wakati idadi ya wajumbe wa kuteuliwa inaweza kuongezeka kutoka na mamlaka za uteuzi kutowekewa idadi ya mwisho ya wajumbe wa kuteua. Matokeo yake sasa, kutokana na kuzidi kuongezeka kwa idadi ya mawakili, itafika sehemu na siyo mbali, idadi ya wajumbe wa kuchaguliwa itakuwa chini ya 1% ya wajumbe wote wa mkutano mkuu, jambo ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona halina afya kwa ustawi wa chama cha mawakili hapa nchini.

25. Mheshimiwa Spika, mamlaka ya uteuzi ambayo yamewekwa katika kifungu cha 21(4)(c) cha muswada huu kinaweza kutumika vibaya na kanda kwa kanda kushindana kuunda kamati mbalimbali ili kupata wajumbe wa mkutano mkuu zaidi ya kanda nyingine. Matumizi haya mabaya yana uwezekano wa kutokea zaidi kwa kanda ya Dar es salaam ambayo hadi sasa kwa takwimu za Kambi, inaonesha Kanda hii inatakrabani 70.12% ya wanachama wote wa chama cha mawakili. Hali hii pia inaweza kulikumba baraza la uongozi chini ya kifungu kipya kinachopendekezwa cha 21(4)(b).

26. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 21(4)(g) cha muswada, kinalipatia baraza la uongozi mamlaka yasiyo na ukomo ya kuteua wajumbe wa mkutano Mkuu wa Mwaka, hata kama wajumbe hao siyo wanachama wa chama cha mawakili. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashangaa ni kwa namna gani Serikali wanaweza kuwa na muswada ambao una kifungu kama hiki, tena kwa sheria ya chama cha mawakili, ambao ni wadau wakubwa wa sheria

hapa nchini. Kwa udhaifu huo basi Kambi Rasmi inapendekeza kwamba kifungu cha 21(5) kiruhusu mawakili wote kuhudhuria mkutano Mkuu wa mwaka ili kuwapatia haki yao ya kushiriki na kuamua maswala yanayohusu chama chao.

27. Mheshimiwa Spika, kama tulivyodokeza hapo awali, nchi zote za jumua ya madola, Mikutano Mkuu ya mwaka ya vyama vya mawakili wa nchi husika uhudhuliwa na mawakili wote, Tanzania tumekumbwa na tatizo gani katika hili, Tunapenda kuikumbusha Serikali kurejea sheria mbalimbali kutoka katika mataifa yafuatayo ambayo, sheria zilizoanzisha vyama vya mawakili kwa nchi hizo, zinawataka **mawakili wote** kuhudhuria mikutano Mkuu ya mwisho wa Mwaka, nchi hizo ni kama ifuatavyo

- i. Nchi ya Uganda kupitia kifungu cha 17 cha sheria ya mawakili wa Uganda, Sura ya 276,
- ii. Zanzibar, kupitia Zanzibar law society, kifungu cha 15(3) cha sheria ya "Zanzibar law society Act, 2019.
- iii. Botswana kupitia chama cha mawakili kinachoitwa Law society of Botswana na kifungu cha 65 & 66 vya sheria inayoitwa "the legal practitioner Act, Cap 61:01
- iv. Swaziland kupitia chama cha mawakili Swaziland law society na kifungu cha 41 cha sheria inayoitwa Legal Practitioner Act, 1964
- v. Lesotho kupitia Law society of Lesotho na kifungu cha 10(5) cha sheria inayoitwa Law society Act, 1983.
- vi. Namibia kupitia chama cha mawakili kinachoitwa society of Advocate of Namibia na kifungu cha 44(5) cha sheria inayoitwa The legal Practitioner Act, 1995
- vii. Zambia kupitia chama cha mawakili kinachoitwa "Law Association of Zambia" na sheria 'rule 8(9) of the Laws Association of Zambia (General) Rules 1996.
- viii. Ghana, chama cha mawakili kinaitwa Ghana Bar Association na ibara ya 16(2) ya katiba ya Ghana Bar Association 1994, inaruhusu mawakili wote kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Mwaka wa mawakili.
- ix. United Kingdom, ambako Law society of England and wales Rule 27(1) of the by-laws of the law society of England and wales, 2012.
- x. United Kingdom- General Bar Council of England and wales, Rule 3 of schedule III of the constitution of the General council of the Bar of England and wales 2017.

28. Mheshimiwa Spika, nchi zote hizo zinavyama vya mawakili na wote wanahudhuria mikutano mkuu ya mwisho wa mwaka kujadiliana mambo yanayohusu chama chao, Tanzania tumekumbwa na jambo gani hadi tunahisi mawakili hawapaswi kukutana na kujadili maswala ya ustawi wa chama chao pamoja na maswala yanayohusu tasnia ya sheria hapa nchi. Ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba kifungu husika kiruhusu mawakili wote kuhudhuria mkutano Mkuu wa mwaka.

ii. Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, Sura ya 33

29. Mheshimiwa Spika, kifungu cha sita (6) cha muswada kinachooongeza kifungu kipya cha 64A katika sheria, kifungu kidogo cha 64A(2) kinachosema kwamba;

“For the purposes of facilitating conciliation, negotiation na mediation the Minister may make rules, prescribing for procedures, forms and other matters relating to conciliation, negotiation and mediation.”

30. Mheshimiwa Spika, katika kifungu tajwa hapo juu, hoja yetu ni kwamba, kwakuwa sheria inatambua maridhiano baina ya pande mbili nje ya mahakama, hivyo basi badala ya jukumu ya kutayarisha kanuni, taratibu na miongozo kuwa la Mheshimiwa Waziri, ni vyema jukumu hilo likabaki kuwa chini ya Mhimili wa Mahakama; Tunaposema Mhimili wa Mahakama maana yake ni kuwa Jaji Mkuu ndiye awe na mamlaka ya kutayarisha utaratibu wa namna maridhiano (**usuluhishi, mazungumzo na upatanishi**) yatakavyofanyika nje ya Mahakama badala ya Waziri. Tunaamini kuwa kuendelea kumfanya Waziri kujiingiza katika jukumu hili ni kupoka jukumu la kutafsiri na utoaji wa haki ambalo ni jukumu la msingi la Mhimili wa Mahakama.

ii. Sheria ya Tasnia ya Maziwa, Sura ya 262

31. Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumeainisha hapo awali kuhusu umuhimu wa tasnia hii ya maziwa na umuhimu wake kwa jamii, tunaona katika muswada Serikali imefanya marekebisho katika kifungu cha 3 cha sheria mama kwa kuleta mapendekezo kupitia kifungu cha 10 (a) cha Muswada kwa kuongeza maana ya “Maziwa” ikijumuisha yale yasiyotokana na mifugo.

Pamoja na nia njema, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kulikumbusha Bunge lako tukufu na Serikali kuwa changamoto kubwa ya wafugaji na wafanyabiashara wa Maziwa sio tu uzalishaji bali pia kukuza thamani ya zao la maziwa na masoko ya uhakika ndani na nje ya Nchi. Hivyo basi kupanua mawanda ya tafsiri ya maziwa kwa kujumuisha maziwa yatokanayo na Mifugo na mazao inaweza isiwe suluhisho kwa zao hili hasa kwa kipindi hiki ambacho Serikali imejikita katika tozo, adhabu na ukiritimba mkubwa kwa wakulima badala ya kuwajengea uwezo, kuongeza thamani na kutafuta masoko ya maziwa ndani na nje ya nchi.

Kambi rasmi ya upinzani Bungeni inaishauri serikali kuboresha Mazingira ya zao la Korosho na Soya kwani dunia imenza kuzalisha maziwa kupitia zao hilo, na tunaikumbusha Serikali kumaliza mgogoro na wakulima wa Korosho ili iwe motisha kwa maeneo mengine waweze kuwekeza kwenye zao hilo tupate maziwa ya kutosha.

32. Mheshimiwa Spika, aidha katika kifungu cha 10(b) imetolewa tafsiri ya neno **“inspector”** kuwa ni mtu atakayeteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 33B. Ni bahati mbaya sana kwamba sheria hii ya Tasnia ya Maziwa katika Nyanja ya ubora kuanzia uzalishaji, vifaa vya ufungashaji (vifungashio) vinaratibiwa na sheria ya TBS. Kwa marekebisho haya yanayopendekezwa na Serikali katika sheria hii ina maana tunakuwa na wakaguzi wa maziwa na bidhaa za maziwa na hivyo kutakuwa na wakaguzi wa aina mbili kwa bidhaa tasnia hii ya maziwa. Sambamba na uwepo wa maabara mbili za taasisi zitakazokuwa kuwa chini ya sheria mbili tofauti zitakazokuwa zinashughulikia jambo moja.

33. Mheshimiwa Spika, kwa mustakabari mwema wa uendeshaji wa Tasnia hii ya Maziwa ni muhimu sana sheria hii ikaweka mipaka ya kiutendaji baina ya watendaji waajiliwa wa TBS japokuwa sheria hii ya Maziwa kifungu cha 10(s) bado kinatambua sheria ya TFDA katika kufanya **“inspection”** na hawa wakaguzi ambao watakuwa wanafanyakazi kwa niaba ya Bodi ya Maziwa ambao watapewa mamlaka kwa mujibu wa kifungu cha 33B cha sheria ya Tasnia ya Maziwa, Sura 262.

34. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona hapa kuna uwezekano mkubwa wa muingiliano wa majukumu jambo ambalo linaweza kuzalisha mazingira ya rushwa na ukiritimba katika tasnia hii.

35. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 13 cha muswada kinachofuta na kuandika upya kifungu cha 9 cha sheria mama, kinahusu uundwaji wa Bodi ya Tasnia ya maziwa, ambapo kifungu hicho kinaonesha kutakuwa na wajumbe 7 katika bodi na kati ya hao wajumbe wawili (2) tu ndio wanawakilisha wadau na waliobakia 5 wanawakilisha taasisi za Serikali. Ni muhimu wakati tunafanya marekebisho tukaelezwa bodi inayofutwa iliyokuwa na wajumbe 12, tatizo lake lilikuwa nini hasa mpaka muundo unabadilishwa? Kambi Rasmi Upinzani kama ilivyoeleza hapo awali kwamba hii tasnia kwa asilimia kubwa inaendeshwa na sekta binafsi, kwa mustakabali huo ni muhimu pia katika Bodi ya uendeshaji wa tasnia hii ya maziwa, sekta binafsi ikawa na uwakilishi wenye uwiano unaolingana na uwepo wa sekta binafsi katika tasnia hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri wadau katika Bodi wawe watatu na Serikali iwe na wajumbe watatu na Mwenyekiti hivyo kufanya upande huo kuwa na wajumbe wanne.

36. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 14 cha muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha 16(5)(a) cha sheria mama kinapendekeza marekebisho kwa wadau wa tasnia ya maziwa ambao watahitajika kuwa kwenye regista ya msajili wa Bodi ya maziwa, miongoni mwa wadau hao ni; milk retailers, milk collectors, na milk traders. Kambi Rasmi inafahamu kuwa hawa wadau ili wafanye kazi ni lazima wapate vibali au leseni kutoka kwa mamlaka husika. Tuangalie hali halisi ya wadau wa tasnia yetu na je wale wafanyabiashara wadogo wadogo nao ni lazima wawe kwenye regista ya Msajili wa Bodi ya Tasnia ya maziwa?

37. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 15 cha muswada kinachorekebisha kifungu cha 17(2) cha sheria mama kinachohusu usajili, pia kwa hoja ambazo tumezieleza hapo awali kuhusu usajili kwa wadau ambao watakuwa wanajihusisha na maziwa kwa ujumla wake, ni muhimu kuwa na takwimu zinazohusu biashara nzima ya maziwa, lakini tukumbuke serikali iliibua hoja ya wajasiriamali wakauziwa vitambulisho visivyo na jina wala anuani je ni mfumo gani utatumika kuhakikisha nao wanatambuliwa na kuingizwa kwenye regista kama sehemu ya wadau wa Maziwa Nchini?

iii. **Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura ya 245**

38. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 cha muswada kinachorekebisha kifungu cha 3 cha sheria mama kwa kuongeza kifungu kipya cha 7 na 8. Kifungu kidogo kipya cha 8 kinasema kwamba;

“Where a decree is to be executed against property in possession of an Executive Agency, procedure to execute decree against Government property under the Government proceedings Act shall apply”

39. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikisisitiza umuhimu wa kutenganisha malalamiko dhidi ya Mawakala wa Serikali na Serikali yenyewe hasa kwenye mashtaka ambayo wakala (Agencies) wameyafanya kwa uzembe au kutowajibika. Kitendo cha Wakili Mkuu wa Serikali kuwa sehemu ya mashauri yote ambayo wakala anaweza kushitakiwa, kinatoa taswira au kuleta dhana kuwa Wakili Mkuu wa Serikali anawekwa pale ili kuhakikisha haki haitendeki au unachelewa kwa wananchi ambao kwa njia moja au nyingine wanakuwa wamenyimwa haki zao na wakala husika. Kambi Rasmi ya Upinzani inalishauri Bunge kutenganisha makosa ambayo Serikali inaathirika moja kwa moja ili kuleta uwajibikaji wa taasisi zenye mahusiano ya moja kwa moja na serikali na pia kujenga imani kwa wananchi kuwa serikali haifungamani na upande mmoja bali ipo kulinda maslahi ya mlalamikaji pia.

iv. **Sheria ya Uvuvi, Sura ya 279**

40. Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 21 cha muswada kinachorekebisha kifungu cha 8 cha sheria ya uvuvi kwa kufuta vifungu vidogo vya 4 na 5 na kuviandika upya kwamba, pale itakapobainika kuna usimamizi mbaya wa tasnia ya uvuvi toka kwa Halmashauri, Waziri atasitisha au ataipokonya Halmashauri hiyo usimamizi wa sekta ya uvuvi na atamtaarifu Waziri Mwenye dhamana na Serikali za Mitaa uamuzi wake huo na atateua chombo kingine kusimamia sekta ya uvuvi katika halmashauri husika.

41. Mheshimiwa Spika, iko wapi dhana ya ugatuuji madaraka kutoka Serikali Kuu? Tunawezaje kupoka madaraka ya usimamizi wa rasilimali za wananchi katika ngazi ya Halmashauri kwa kosa la uadilifu? Kambi Rasmi ya Upinzani inafahamu kuwa Halmashauri zetu zinaendeshwa na zina mamlaka kamili ya kujiendesha chini ya usimamizi wa Baraza la Madiwani, na pale inapotokea idara ina matatizo, ufumbuzi sio kufuta idara bali ni kufanya mabadiliko kwa wale wanaoongoza hiyo idara. Na ukisema unaipokonya usimamizi wa kazi zote zinazohusiana na sekta ya uvuvi, kwa maana nyingine unaoondoa hata mapato yaliyokuwa yanaingizwa kutokana na sekta ya uvuvi (OWN SOURCE). Mapendekezo haya yamejaribiwa katika Halmashauri gani na kuona matokeo yake? Tusitunge sheria kama mchezo wa kubahatisha, hii ni hatari sana kwa uendeshaji wa Halmashauri zetu.

42. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inayaona mapendekezo hayo sio tu yanakiuka Sera ya Ugatuuji madaraka lakini pia ni muendelezo wa kuzipoka Halmashauri vyanzo vyake vya mapato, hasa ikizingatiwa kuna Halmashauri ambazo zinategemea Sekta ya Uvuvi kama chanzo chake kikuu cha fedha. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalishawishi Bunge hili tukufu Isipitishie kifungu hiki kinachodhalilisha mabaraza yetu ya madiwani na badala yake tunaishauri serikali kuhusha mfumo wa Ufatiliaji na Tathmini (Monitoring and Evaluation) ambao utatoa taarifa mapema kwa waziri juu ya usimamizi wa Sekta ya uvuvi nyenzo hii itamuwezesha Waziri kuchukua hatua mapema kabla sekta haijaathirika.

43. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 22 cha muswada kinachorekebisha kifungu cha 40(1) (a) cha sheria mama kwa kufuta maneno **“ten thousand shillings”** na kuweka maneno **“one million shillings”**. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona hiki ni kiwango kikubwa sana cha adhabu, uhalisi uwezi kutoka elfu kumi ukaruka hadi milioni moja, huu ni ukatili mkubwa sana kwa baadhi ya makosa kati ya yale makosa matano yaliyomo kwenye jedwali la sheria husika. Mfano kosa namba 2 la kuvua samaki au mazao ya samaki bila kibali. Pia kosa namba 5 katika jedwali linasomeka kwamba, **“Possession of sea shells, shell product, aquarium fish for trade or for public display and commercial purposes without valid document”**

44. Mheshimiwa Spika, ukitafakari makosa tajwa hapo juu na hali halisi ya wadau wanaojihusisha katika tasnia hiyo ni dhahiri kuwa kiwango kilichowekwa kwa makosa yote yaliyomo kwenye jedwali lililotayarishwa chini ya kifungu cha 40 cha sheria mama ni kutokuwatendea haki kwa wahusika wa makosa tajwa hapo awali.

45. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 23 muswada kinachotoa adhabu kwa makosa ambayo yanahusiana na uvuvi usiokuwa wa kisheria na adhabu yake hayajaelezwa kwenye sheria mama. Kambi Rasmi inasema kama makosa hayajafanuliwa kwenye sheria maana yake ni yale ambayo uwezo wake wa kusababisha madhara kwenye tasnia nzima unaweza kuwa ni mkubwa au mdogo sana. Hivyo basi, adhabu ya shilingi Milioni 10 mpaka 50 kama inavyoelezwa kwenye kifungu kipyua cha 47(a) inakosa msingi wa Kisheria na inaweza kutumika vibaya. Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ni kuwa Serikali ibainishe aina ya makosa ili

kuhalalisha (to justify) adhabu na sio kuweka kifungu cha jumla na kisicho na matumizi kwa muktadha wa sasa. Kama hapo baadae yataibuka makosa mengine ambayo hayakuwekwa kwenye sheria hii basi Bunge litarejea kufanya marekebisho kwa kuongeza makosa hayo na adhabu zake. (A Law must be specific and must intend to cure a specific problem)

v. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287

46. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 31 cha muswada kinacho rekebisha kifungu cha 190(1) cha sheria mama, na kukiandika upya, kwa kubadilisha masharti ya utoaji wa notisi ya kuishtaka Mamlaka ya Serikali za mitaa kitoka siku 30 hadi siku 90 kimalizike.

47. Mheshimiwa Spika, wakati Dunia ikielekea katika ulimwengu wa Sayansi na teknolojia, ulimwengu wenye kurahisisha mifumo ya kiutendaji na kuongeza uwajibikaji wa serikali kwa wananchi sisi tunaongeza urasimu kuchelewesha huduma kwa wananchi.

48. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona notisi ya siku 90 ili kuweza kuishitaki Serikali (Serikali kuu na Serikali za mitaa) imepitwa na wakati na inaleta upendeleo kwa Serikali na kumkandamiza Mwananchi (Mlalamikaji) Tunasema imepitwa na wakati kwani sasa Dunia inaendeshwa na sayansi na Teknolojia na ni hivi karibuni Serikali imejinasibu kwenda kwenye mfumo wa kieletroniki (e-Government), Halmashauri zote zina wanasheria na walau kila Mkoa una mawakili wa serikali waliokasimiwa mamlaka na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

49. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalishawishi Bunge hili Tukufu kukataa mapendekezo ya serikali ya kubadili muda wa notisi badala yake ubaki kuwa siku 30 kama ilivyokuwa mwanzo na tunamshauri Mwanasheria mkuu wa serikali kuleta mabadiliko ya muda wa notisi kwa serikali kuu kuwa siku 30. Ikumbukwe **Justice delay is Justice deny.**

vi. Sheria ya Tasnia ya Nyama, Sura ya 421;

50. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 35 cha muswada kinachorekebisha kifungu cha 2 cha sheria mama, kwa kuongeza kifungu kidogo(subsection) kipyua cha 3 kinachoeleza mipaka ya matumizi ya sheria hii kuwa ni ndani ya Tanzania Bara tu. Maana ya kifungu hiki ni kwamba pale nyama iwe ya kuku, ng'ombe,mbuzi, kondoo n.k itakapokuwa inatoka Bara au Zanzibar kuja upande wa pili wa Muungano itakuwa ni sawa na kufanya baishara na nchi jirani. Jambo hili linapunguza au kuweka vikwazo kwa soko letu la ndani na hii ni kuzidi kuhujumu sekta ya mifugo badala ya kuiendeleza. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba, njia pekee na muhimu ya kuendeleza sekta ni uwepo wa soko la uhakika, sasa tukianza kuwekeana vikwazo sisi kwa sisi ni kutoa fursa kwa jirani zetu kushindana na sisi.

51. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 40 cha muswada kinachoongeza kifungu kipyua cha 33A ambacho kinaweka marufuku ya kuagiza na kutoa nyama Tanzania Bara. Mashaka yetu ni kwa wenzetu wa Tanzania Visiwani, kwani badala ya kuweka mazingira ya biashara wezeshi kwa wadau wa tasnia ya nyama inakuwa ni vikwazo.

vii. Sheria ya Usimamizi wa Mirathi, Sura ya 352

52. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 45 cha muswada kinachorekebisha kifungu cha 108 cha sheria mama kwa kuongeza kifungu kidogo kipyua cha 3 kinachoweza katazo la kugawa ardhi au nyumba kwa mtu ambaye si raia wa Tanzania kwa njia ya mirathi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaangalia kifungu hiki kwa tafakuri kama ikiwa mhusika wa mirathi amempatia urithi mwanae ambaye alizaliwa nje ya nchi na anaishi nje ya nchi na hivyo Wazazi wake ni watanzania na yeye kwa kile kinachoitwa kutafuta maisha yuko nje na amepata uraia. Hoja ya msingi ni kuharakisha utambuzi wa kile ambacho kinajulikana kama uraia pacha. Kwa mustakabali wa marekebisho haya pendekezwa na Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona yafutwe kwani

yanapoka haki ya msingi ya mhusika kwa kumnyima urithi wa mzazi au yeyote aliyehitaji apate nyumba au ardhi.

B. HITIMISHO

53. Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha ni kwamba, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa rai kwa waheshimiwa wabunge na Bunge hili tuangalie kwa tafakuri pana marekebisho ya sheria zinazoletwa na Serikali ili kupata ridhaa ya kuwa sheria.

54. Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba mambo mengi ambayo yanakuwa na hila mara nyingi yanaletwa kupitia miswada hii ya marekebisho ya sheria mbalimbali, kwani kwa njia hizi ni uhakika kwamba kamati za kissekta kwa baadhi ya sheria zinazokuwa zinafanyiwa marekebisho hazipatiwi nafasi kujadili kwa kina marekebisho husika, jambo hilo linafifisha tafakuri ya kina kuhusu marekebisho yanayokuwa yanaletwa na wizara au sekta husika.

55. Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha!

.....
SALOME WYCLIFFE MAKAMBA (MB)

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

28 Januari, 2020

MWENYEKITI: Ahsante na tunakushukuru sana Mheshimiwa Salome Makamba. Wewe ni Wakili wa Mahakama Kuu ya Tanzania? Ni Wakili wa Mahakama Kuu? Haya kaa, umevaa vazi lako ni nadhifu sana, lakini ungelivaa ile nyeupe ingelipendeza sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nina wachangiaji wa hoja hii kwa uwiano wa vyama vyetu wanane upande wa Chama cha Mapinduzi (CCM), wawili CHADEMA na mmoja CUF. Nianze na CUF, Mheshimiwa Ally Saleh Ally, dakika sita kama siyo chini ya hapo.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwangu mimi leo ni moja katika siku ya unyonge na *it's a dark day* kwa sababu ya sheria ambayo tunakwenda kupitisha na sheria ambayo inaonekana Serikali ikiikazia kuhusu *Tanganyika Law Society*. Nahisi kila tunavyokwenda tunazidi kuibana taasisi hii muhimu ili isiweze kufanya kazi zake kama inavyotarajiwa na badala yake Serikali iwe na *control* kubwa sana. Kwa maana nyingine tunazidi kubana *public space* na tukilaumiwa na wenzetu wengine huko nje kwamba Tanzania tunabana *public space* tunakuwa tunalalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu ya vipengele ambavyo kama ambavyo hotuba ya Kambi ya Upinzani hata katika Kamati tulikubaliana kwa kiasi fulani kwamba kuna tatizo la Serikali kutaka kufanya namna ambavyo taasisi hii ya kitaaluma inavyokutana. Mambo yanayofanywa kwingine kote hayafanywi katika taasisi nyingine za kitaaluma, kwa mfano madaktari wanaweza kukutana kama walivyo wako elfu tano wako elfu sita wanakutana kama walivyo. Lakini kwa upande wa *Tanganyika Law Society* wanaambiwa wakutane kwa *zone*, *zone* hizo hatujui baada ya kupitisha kanuni zitakuwa na mfumo gani. Serikali ilikuja na *package* ya *compromise*, lakini haikuridhisha sana kwa mfano, walipoulizwa kwamba asilimia sabini ya wanasheria pengine wapo Dar es Salaam, wakasema inawezekana tukafanya *special zone* kama vile kuna *special zone* ya kipolisi na *special zone* nyingine kwa maana nyingine inawezekana Dar es Salaam kukawa na *zone* nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna tatizo la uwakilishi wenyewe, wenyewe wanasheria wanasema mkutano wao mkuu wakikutana wana mambo mawili; wana mkutano wao wa kujadili masuala yao wenyewe ya kimaendeleo, lakini pia mkutano ule una chagua

viongozi, sasa Serikali wanatoa nje ile aspect ya wao kukutana kama wanachama au watu wa aina moja ili waweze kujadili mambo yao, kwa maana nyingine hili pia linapingana na Katiba ya haki ya kujikusanya, kwa sababu wao ni *entity* moja huwezi kusema uwapeleke kwa mafungu hakuna sababu ya kuridhisha iliyofanywa hivyo. Baada ya mjadala katika Kamati, Serikali ikasema ikaja na lile linaloitwa andiko, andiko lenyewe lilifanywa *within two days* bila ya utafiti ya uhakika au utafiti mpana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaja na hoja nyingi ya za kuzungumzia juu ya namna ambavyo kwa nini wana *cartel power* za *Tanganyika Law Society* kwa sababu tu haijafanyiwa mabadiliko ya siku nyingi na kwa sababu ni sheria ya zamani sana lakini badala ya kuifungua demokrasia tunafunga kwa sababu tu sheria hii ni ya zamani na kwa sababu Serikali ina hofu ya uanaharakati ambao unatokea ndani ya *TLS*.

Mheshimiwa Spika, lakini ukweli uanaharakati ule ni suala la muda tu, inawezekana leo Rais wa *TLS* au Kamati ina uanaharakati lakini kesho au pengine wanaounga *opposition*, lakini kesho inawezekana Rais wa *TLS* ambaye anaunga mkono CCM. Kwa hiyo, unazuia nini wakati hata kama atakuwa mwanaharakati bado ni ndani ya haki yake, bado hajavunja sheria bado anatomikia wananchi wa nchi hii. *TLS* imefanya kazi kubwa, *imagine*, *TLS* inakufa kifo cha ghafla ina maana kwamba tasnia nzima ya sheria imekufa ndani ya nchi hii, lakini unachofanya unauwa pole pole tasnia ya sheria kwa sababu ya vikwazo vingi ambavyo vinakuwa *created* kila siku nafikiri sheria hii haitupeleki mbali bali inaturudisha nyuma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kingine ambacho nataka kusema nje ya jambo hili ni hili la Serikali mashitaka dhidi ya Serikali, Serikali imekwenda kuingia katika mamlaka ambayo tayari yako kwa halmashauri, kwanza imeongeza siku au muda kuomba *fear* kuishitaki Serikali kufikia siku 90 ambapo pengine huyu mtu aliyeathirika ni muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sasa hivi tunataka kumshusha *Solicitor General* awe *involved* ashirikishwe aunganishwe katika kila kesi ya kisheria ambayo iko katika kiwango cha chini na siyo tena kule juu. Rais wa *TLS* Ndgw Nshalla alitahadharisha katika Kamati alisema kwa maana hii sasa kama *Solicitor General* anaunganishwa ina maana Serikali Kuu imeingia ina maana mtu *part* ya *grief* wakitaka *attach* mali, wanaweza waka *attach* mali katika lengo lengo la kitaifa, inawezekana Mtanzania sasa akasema anazuia ndege, akasema anazuia *train*, akasema anazuia *property* ya Serikali kwa sababu Mwanasheria Mkuu amekuwa *involve* katika ngazi ya Halmashauri jambo ambalo hivi sasa halina jambo la kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili unajjuliza juu ya utekelezaji wake Halmashauri zipo nyingi, makosa katika Halmashauri yanafanywa kila siku, halmashauri inashitakiwa kila siku, je, huyu *Solicitor General* atakuwa na *manpower* ya kuweza kuyafanya yote hayo au itakuwa ni yale yale kwamba wanadumbukiza makesi, raia wanaumia hakuna linalofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na jambo la mwisho nataka kusema juu ya *peace mill*...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa George Malima Lubeleje atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Joseph Mkundi.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na niweze kutoa mchango wangu na nina mambo mafupi. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwa kuleta marekebisho ya sheria hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kuhusu marekebisho ya sheria mwenendo wa madai ni kwamba mdai na mdaiwa wanaweza kukubaliana kwamba walimalize shauri lao nje ya mahakama au namna gani. Lakini kuna mashauri mengine ya madai ni magumu mpaka yanafika polisi. Sasa mimi nauliza k? Maana sheria ya madai ni madai na ukienda mahakamani kwenye *court proceedings* ni kwamba kama mtu anadaiwa hakimu anamuuliza je, wewe unauwezo gani wa kulipa madai ya mdaiwa kwa hiyo, mahakama inaweza kutoa *court decree* au ikatoa maamuzi kwamba umlipe kila mwezi au umlipe kila wiki kiasi fulani. Shida yangu ni kwamba kwa nini haya mashauri wakati fulani yanabadilika na kuwa *criminal case*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni marekebisho ya Sheria ya Mtoto, unapoleta marekebisho ya Sheria ya Mtoto lazima Mwanasheria Mkuu ungeleta vilevile marekebisho ya Sheria ya Ndoa, ungeleta vilevile marekebisho ya Sheria ya Mirathi kwa sababu ndoa na mirathi marekebisho ya sheria ni ya muda mrefu sana, tumewahi kuomba sisi Wabunge kwamba kwa sababu kuna mgogoro mkubwa sana katika ndoa na mirathi, kuna baadhi ya makanisa, kuna baadhi ya mila ambayo wanakatazwa wanawake wasimiliki mali. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri Mwanasheria Mkuu nakuomba sana Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mirathi uandae muswada ili uweze kufika hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Seneta Lubeleje kwa ombi lako na ushauri. Tunaendelea Mheshimiwa Mkundi atafuatiwa na Mheshimiwa Adamson Mwakasaka na Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba ajiandae.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii, nimpongeze Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na wawasilishaji wote waliowasilisha marekebisho ya sheria, nina mchango kwenye eneo moja, eneo la marekebisho Sheria ya Uvuvi, Sura 279, kwenye marekebisho haya kwenye Sura 279 sehemu ya 21 kwenye marekebisho yanaongelea juu ya iwapo *Local Authority* itashindwa ku-manage shughuli za uvuvi, Wizara ya Uvuvi itainyang'anya mamlaka na kupewa mamlaka nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia marekebisho haya mbali na kwamba inapora mamlaka ya Halmashauri hizi za Wilaya kwa mujibu wa ugatuuji wa madaraka, lakini si kutendea haki wananchi wa Halmashauri zinazousika na maeneo haya. Kwa sababu haiwezekani, kosa na tatizo *individual* kushindwa kutimiza wajibu wake akashindwa kufanya shughuli za uvuvi kuzisimamia vizuri halafu Halmashauri nzima ikaazibiwa kwa kunyanganywa mamlaka ya kusimamia shughuli zote zinazousu uvuvi halafu baada ya kunyanganywa alafu baada ya kunyang'anywa ndiyo waziri sasa aende kwa Waziri anayeshughulika na *Local Government* kumtaarifu uamuzi aliyechukua, *this is not fair*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri badala kufanyika jambo hili kama itaonekana na Wizara ya Uvuvi ikajiridhisha kwamba *authority* imeshindwa ku-manage shughuli za uvuvi iwasiliane kwanza na Waziri anayeusika na Serikali za Mitaa halafu baada ya hapo sasa itoe mapendekezo nini kifanyike ili usimamizi uweze kwenda vizuri kama ambavyo Wizara ya Uvuvi ingekuwa inatarajia. Lakini inapofanya uamuzi wa kuchukua mamlaka ikawanyang'anya mamlaka ya kusimamia uvuvi halafu ndiyo ikaenda kutoa taarifa kwenye Wizara inayoshughulika na Serikali za Mitaa hii si kuitendea haki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiendelea kwenye sehemu ya 22 inaongelea juu ya adhabu, hivi ni wavuvi wapi tunaowaongelea hawa? Ni wavuvi hawa hawa Watanzania

ninaowafahamu mimi ninayetoka kwenye eneo la uvuvi? Wavuvi ambao siku zote kwa sababu wamezaliwa, wamekua, wanafanya *local fishing*, leo kwa sababu moja mbili tatu tunaona kwamba kuna *modern fishing* hii waliokuwa wanafanya *traditional fishing* tunaona kwamba haipaswi, halafu tunawaukumu mvuvi huyu wa kawaida, mvuvi mdogo apigwe *fine* ya milioni moja, milioni kumi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwatendea haki wavuvi hawa, adhabu hii ni kubwa sana kwa wavuvi ninaowafahamu mimi na zaidi ya hapa kinachofanyika hapa kuna mambo mawili ama sehemu kubwa ya wavuvi zaidi ya asilimia 90 ninaweza nikafikiri labda wataishia magerezani au tunatengeneza mwanya mkubwa sana wa rushwa kama zile ambazo zilikuwa zinafanyika wakati wa *operation* wa uvuvi haramu. (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mvuvi gani wa kawaida atakaye mudu kutoa milioni 10 mpaka milioni 50 kwa sababu tu amekutwa anafanya shughuli za uvuvi haramu tunajua wavuvi wetu, wanaenda kule ziwani wanavua furu, wana kamtego ka shilingi sijui 2,000 halafu umpige *fine* ya shilingi milioni 10 itawezekana wapi? Mazingira haya siyo ya Tanzania haya tuangalie upya sheria hii lakini adhabu hizi ni kubwa sana kwa mvuvi mkubwa ninayemfahamu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nichangie kwenye maeneo hayo tu tunahitaji kuangalia sheria hii na haya marekebisho ili tunachokibadili na tunachokitaka kiendane na mazingira halisi ya wavuvi wetu tulionao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nashukuru sana kwa fursa ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mkundi, sasa Waheshimiwa Wabunge mnatoa ushauri mzuri sana kwa Serikali, lakini niwaambie tusiishie tu hapo maana hatua ya kutunga sheria tutakapoingia Kamati ya Bunge Zima hayo uliyoyasema Mheshimiwa Mkundi na wengine kama wanamawazo ya namna hiyo lazima yaje katika fomu ya *schedule of amendment*. Haya tunaendelea, Mheshimiwa Mwakasaka.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuleta mabadiliko haya ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 8 ya mwaka 2019. Ni kweli toka mwaka 1954 ni muda mrefu tulikuwa tunahitaji marekebisho haya ningeomba nipitie maeneo machache tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba nianze na hili la Sheria ya Mawakili Sura 307 hata kwenye Kamati eneo hili lilikuwa na mambo mengi sana, lakini wakati tupo kwenye Kamati kulikuwa na tatizo la baadhi ya wadau ambao walikuwa wakihoji kwanini kuwe na Sheria ya Uwakilishi, kwa kawaida hawa ma-*advocate* wanakwenda kwa kura moja moja hata kwenye hiyo *General Meeting* yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni kwamba pamoja na mambo ya gharama hata kama serikali haichangii bado ile fedha inahitajika kwenye shughuli zingine. Uwakilishi siyo kwenye vyama tu hivi au *TLS* peke yake, hata sisi kama vyama vya siasa hatuendi wote kwenye mikutano yetu mikuu, uwakilishi upo siyo kwa *TLS* peke yake, kwa hiyo, suala kwamba *TLS* labda kuna ajenda labda imefichwa hiyo kitu sidhani kwamba ni sahihi. Lakini pia serikali imeridhia mapendekezo mengi ya kamati ambayo yanaonekana kwenye Jedwali la Marekebisho, kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kuzingatia hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuonesha kwamba Serikali haina nia mbaya na Muswada huu kwenye marekebisho ya sheria hizi ukienda kwenye Sura 16 ambayo inarekebisha kifungu

cha 138(c) cha kuwalinda watoto wa kiume kwa kawaida sheria ambayo ipo ilikuwa ni ya mtoto wa kike, hapa tunaongelea mtoto wa kiume chini ya miaka 18, wengine maarufu wanaita *vi-ben ten*, wapo kwenye sheria hii, kwamba sheria iwepo kwa sababu tulikuwa hatuongelei chochote. Kweli kuna wavulana wanakuta wana miaka 16, 17 wanadhalilishwa na mambo haya ya kujamiana na mambo mengine, haikuwepo sheria ya kuwalinda. Sasa Serikali imeleta sheria hii ya kuwalinda watoto wa kiume wa namna hiyo, naipongeza sana Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna Ibara ya 13 ya Tasnia ya Maziwa lakini pia Ibara 38 ya Tasnia ya Nyama tulikuwa tunachanganya kidogo kwenye zile bodi tulijaribu kuuliza kwanini Bodi hizi Mwenyekiti wao atokane na mapendekezo ya Waziri wa uteuzi wa Waziri kwanini bodi hizi zisiwe kama bodi zingine ambazo Mwenyekiti wake anateuliwa na Mheshimiwa Rais, lakini Serikali ilitoa maelezo mazuri kwamba hawa watakuwa ni washauri zaidi na siyo kama kwenye bodi zingine.

Kwa hiyo, naishukuru Serikali kwa mapendekezo hayo na sisi kama Kamati tuliridhia na naomba niseme kwa hoja hizi chache naunga mkono hoja ya mapendekezo haya kwa asilimia mia moja, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Shukrani na ahsante sana kwa mchango wako, Mheshimiwa Dkt. Tizeba atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama na Mheshimiwa Upendo Peneza ajiandae.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, lakini pia nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uwasilishwaji mahiri sana. Bila kwenda mbali naomba niseme hali niliyonayo kwamba najjuliza nitachangia vipi kwa sababu wakati fulani nilisimamia sheria hizi na leo nalazimika kuzizungumzia kwa upande mwingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ambalo napenda nilichangie ni hili la *suspension* za *Local Governments* watakapoonekana wameshindwa kusimamia shughuli za uvuvi. Nilikuwa naangalia *definition* ya *Local Government* katika *context* hii, nimeshindwa kuelewa ni wale watumishi *individual* au ni mamlaka nzima ya Halmashauri inayozungumziwa? Kama ni suala la mtumishi moja moja, sina tatizo nalo kwamba yule akikosea wanaweza wakam-*suspend* na niungane na Mheshimiwa Mkundi kwamba *suspension* ile ifanyike baada ya *consultation* na TAMISEMI, isije ikawa sasa watumishi walio katika mamlaka nyingine wanapewa adhabu na mamlaka nyingine ambayo haiwaajiri wao ninaelewa usimamizi wa *professional ethics* uko katika Wizara ya Kisekta, lakini suala la kinidhamu linapohusu lazima mwenye kumwajiri yule ndiye atoe mamlaka ya kum-*suspend*. Kama ni ku-*suspend* Halmashauri nzima kwa ujumla kwamba isijihusishe tena na usimamizi wa uvuvi, naona hapa tunakwenda ndivyo sivyo. Hili ni suala la Kikatiba, mamlaka za mitaa haziwezi zikawa zinanyang'anywa mamlaka zake kirahisi rahisi namna hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, ni hizi adhabu zinazopendekezwa, ni kweli uvuvi haramu si jambo jema, hakuna mtu anaweza kushabikia uvivu haramu. Hakuna mtu anaweza kushabikia, mimi tatizo langu katika mapendekezo haya la kwanza ni kufananisha makosa. Wako watu wanavua kwa pamoja kama vikundi, lakini wakikamatwa kwa mujibu wa sheria hii watahukumikiwa mmoja mmoja. Pili, makosa yanayofanywa na mchuuzi hayawezi kamwe yakalinganishwa na mvuvi haramu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaoishi kwa asilimia 90 tukitegemea uvuvi, wananchi wengi shughuli zao ni za uvuvi na biashara zinazohusiana na uvuvi. Sasa kuna mambo ambayo lazima tuwe makini sana, hivi mama wa kawaida na sikuona kama iko *provided for* kwenye hii

sheria, hiyo *exception*. Samaki hali ya hewa ikibadilika wanakufa tu wanaelea, siyo lazima wamevuliwa na mtu na watu hawazuliwi kuokota samaki wa hivi. Akikutwa ameokota anawauza kwa mujibu wa sheria hii, mama au kijana yeyote atakuwa amevunja sheria na anatakiwa afungwe miaka isiyopungua miwili au faini kati ya shilingi milioni 10 mpaka milioni 50. Hili halifanani na ukweli wa nchi hii. Niombe sana hizi adhabu ziwe *graduated*, watu wenye makosa makubwa katika uvuvi na yanafahamika, wale kweli tunaweza kwenda nao kwenye adhabu hizo za milioni 10 au ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wanaofanya *petty offences, petty!* Sasa zote zimejumlishwa zimewekwa kwenye kapu moja. Sidhani mtu anayeibia nchi hii bilioni 100, bilioni 50 ni mwizi ndiyo, lakini hafananishwi na mwizi aliyeba shilingi 20,000 kwenye mfuko wa mtu ndugu zangu. Hata adhabu humu tumeziweka tofauti yule mwingine tumemweka kwenye kundi la uhujumu uchumi na hawa wengine wameachwa ni wezi tu wadogo wadogo ambao kila siku Mheshimiwa Rais anawaachia baada ya kukaa jela miezi miwili, mitatu wanaambiwa wamepata msamaha wa Mheshimiwa Rais wanatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku tulivyoliweka linavyoletwa hili pendekezo adhabu hizi zimekwenda tu kama vile makosa haya yanafanana, aliyefanya kuuza furu watano atahukumiwa milioni 10 mpaka 50 na aliyefanya kuvua makokoro, kumwaga sumu majini na yeye atahukumiwa milioni 10 mpaka milioni 50, hili haliko sawa. Limewekwa hivyo, sasa linaleta mashaka kwamba ni mitego ya rushwa kwa sababu *latitude* ya adhabu inavyokuwa kubwa namna hii inampa mtu anayetoa hukumu kishawishi cha ku-*negotiate*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikiria mtu amekamatwa ana gunia la dagaa wa *size* ndogo, kwa mujibu wa sheria inavyopendekezwa huyu amefanya kosa ambalo atastahili adhabu ya kati ya milioni 10 mpaka milioni 50. Hivi kinamzuia nini huyo *prosecuting officer* kumwambia hebu tu-*negotiate* hapa au yule anayesikiliza hili shauri kusema tu-*negotiate* badala ya milioni 50 nikwambie leta milioni tano nikuachie, nikupige faini ya milioni ngapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana hili jambo liangaliwe upya, liangaliwe upya kabisa. Nimekusikia unasema tulate *schedules of amendment* lakini bahati mbaya sijui kama muda unatutosha sasa kufanya hivyo. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Dkt. Tizeba kwa ushauri wako, muda wetu ndiyo huo. Tunaendelea na Mheshimiwa Mhagama Joseph.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada wa Sheria ya Marekebisha ya Sheria Mbalimbali (Na. 8). Kwa maslahi ya muda nitakwenda moja kwa moja kwenye hoja yangu, nataka kwanza nijikite kwenye hii Tasnia ya Maziwa, Sura ya 262.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya ajenda kubwa za Serikali ya Awamu ya Tano, Serikali ya Jemedari Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ni kuhakikisha kwamba tunaifikisha Tanzania yetu kwenye uchumi unaotegemea viwanda. Moja katika maeneo makubwa ambayo yatachangia safari ya kuipata Tanzania ya viwanda ni sekta ya mifugo hususan eneo la maziwa na nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya kuanzisha maabara ya maziwa, kifungu kipya cha 33A kinalenga kuipata Tanzania ya viwanda. Baadhi ya wadau wamechangia hapa hasa hotuba ya Kambi ya Upinzani wakati wanachangia ilionesha kuwa na maabara hii ni kama kupoteza rasilimali kwa sababu tuna maabara ya *TBS*. Ikumbukwe

kwamba maabara ya TBS kazi yake ni kuangalia ubora na viwango katika ujumla wake, lakini tunapotaka kutengeneza bidhaa ambayo inataka kwenda kushindana kimataifa, tunataka kwenda kuuza kwenye *ISO Standards* ni lazima tuwe na maabara maalum ambazo zinajibu mahitaji ya masoko ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, tayari tunazo maabara kama hizo hapa nchi, tuna maabara ya samaki ambayo inaitwa *Water Quality Lab*. Hii inalenga kuhakikisha kwamba samaki wanaovuliwa Tanzania kokote wanakokwenda kuuzwa ndani na nje ya nchi ubora wao kwa maana ya maji yaliyotumika unafahamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limefungua sana soko letu la samaki nje ya nchi, samaki wetu wameaminiwa nje ya nchi kwa sababu aina ya maji yanayotumika kuwakuza hao samaki inafahamika na imekubalika kimataifa. Tuna maabara za maji zipo mbili, ambazo nazo zinatumia *ISO Standards*, kwa maana hiyo maji yanayozalishwa kwa viwango hivyo yanaweza kuuzwa kokote dunia. Sisi Tanzania tunapotaka kwenda kwenye masoko ya kimataifa lazima bidhaa zetu zipate sifa hizo za viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika zao ambalo litatupeleka katika masoko ya kimataifa ni zao hili la maziwa, kwa hiyo, niseme tu kwamba kwa Mheshimiwa Waziri kuleta marekebisho haya ameyaleta wakati muafaka kabisa na naomba Bunge lako tukufu liunge mkono kuanzisha maabara kwa kifungu cha 33A.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mfano wa maabara nyingine *TFDA* pamoja na majukumu mengine waliyonayo wana maabara ya *food quality*. Pamoja na TBS wapo lakini *TFDA* wana maabara, kwa hiyo, maabara hii isieleweke kwamba ni maabara mpya kabisa kwa maana ya kwamba hakuna *practice* hiyo nchini. *Practice* hiyo nchini ipo na inatusaidia kwenda kushindana kuzifanya bidhaa zetu zishindane kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili katika Sheria ya Tasnia ya Maziwa ni kuhusu Bodi ya Maziwa kifungu cha 9. Aina ya bodi iliyopendekezwa hapa ni Bodi ya Ushauri, Bodi hii ni tofauti na bodi ambayo ningesema ni *executive*. Ni bodi ambayo ina maamuzi na ni bodi ambayo inaweza kuchukua maamuzi. Bodi iliyopendekezwa hapa ni bodi ambayo kimsingi haiwezi kuchukua maamuzi zaidi ya kumshauri Mheshimiwa Waziri. Kwa vile tunataka kujenga Tanzania ya viwango, kuipata Tanzania ya viwanda, naishauri Serikali kwanza ianzishe hii bodi, lakini bodi hii ibaki kuwa *interim* tu, tuendeleo na mchakato sasa wa kuwa na bodi ambayo ni *executive* ambayo uteuzi wake utamhusu Mheshimiwa Rais na itakuwa na meno na itaweza kuisaidia sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama muda utaniruhusu naomba nichangie kidogo kwenye Sheria ya Chama cha Mawakili Tanganyika, Sura ya 307, kifungu cha 22 kinachoitaka tasnia hii mkutano mkuu ushiriki wake uzingatie uwakilishi. Chama cha Mawakili kinazidi kukua kwa idadi ya wanachama, kama kitaachwa hivi kilivyo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba kuunga hoja mkono na ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mhagama kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Upendo Peneza, atafuatiwa na Mheshimiwa Sixtus Mapunda na Mheshimiwa Peter Msigwa ajiandae.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kabla sijaendelea na mchango wangu ningependa kuleta ombi katika meza yako ambalo pia litawakilishwa kwa Mheshimiwa Spika, kwamba tunakuwa kwenye Kamati zetu lakini kwa bahati mbaya kamati pekee ambayo inachukua rekodi ya mambo ambayo yamezungumzwa kwenye Kamati ni Kamati ya Bajeti peke yake. Kamati nyingine hakuna rekodi ya kazi ambazo zimefanyika kwenye Kamati na ni rahisi hata humu ndani kuingia na hata Serikali kutokukubaliana na vitu kwenda tofauti kwa sababu hatuna maandishi kimsingi ambayo yanatunza rekodi pamoja na michango ya Wabunge kupitia ndani ya Kamati zao. Nasema tu hivyo ili tulinde na tuweze kusaidia zaidi wananchi kwamba Kamati ilifanya nini na Serikali imeleta nini ili kuweza kutoa mwongozo katika majadiliano mbalimbali ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuomba kwamba Mheshimiwa AG yuko hapo na amesikiliza watu ambao tunatoka Kanda ya Ziwa jinsi gani ambavyo sheria hii ambayo inawagusa wavuvi, ni namna gani ambavyo siyo rafiki kwa wavuvi ambao ni watu wa chini, ni watu wadogo katika maeneo yetu. Sheria hii pia siyo hata rafiki kwa halmashauri zetu ambazo tunatoka kwa maana halisi ya kimapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo basi, unaona kabisa kuna ukinzani mkubwa katika sheria ambayo imeundwa. Unaniambia kwamba Waziri anayehusika na Uvuvi akasimamisha kazi watu ambao watu wako TAMISEMI, watu wasiomhusu, watu ambao hakuwajiri, watu ambao hawasimamii, watu ambao hawana namna nyingine tu kukutana nao unamsimamisha mtu halafu unatoa taarifa kwa Waziri wa TAMISEMI ili amfanye nini sasa! Ampime aonekane vipi au baadaye akimrudisha kazini inakuwaje! Kwa hiyo, kimsingi bado kuna nafasi AG labda anaweza akaona namna kwamba anaweza akaamua hiyo aka-*withdraw* bado hatujachelewa kabla hatujafika mwisho kabisa kwa maana ya hii sheria kupitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee katika upande wa mabadiliko yaliyokuja katika tasnia ya wataalam wetu wanasheria. Kama ambavyo mnafahamu kwamba tuna vyama mbalimbali, tuna Vyama vya Madaktari, tuna Vyama vya Wauguzi, tuna vyama mbalimbali ndani ya nchi yetu. Lakini mkazo mkubwa sana na Serikali inauleta katika Chama cha Wanasheria na imekuwa ni kazi sasa ya Serikali nadhani kwa sasa ni kama miaka mitatu au minne iliyopita tangu Mheshimiwa Tundu Lissu alivyogombea, imekuwa ni kama ni chombo ambacho kinaangaliwa na Serikali kwa jicho lingine. Kama ni chombo ambacho kinaikosoa Serikali, kama ni chombo ambacho kinaweza kikaleta sura tofauti wanapokuwa waki-*deal* na Serikali. Kabla hatujafikiria kubadilisha uwakilishi wa wanasheria katika kupiga kura na kuchagua viongozi wao tuwaangalie katika majukumu ambayo chama hiki kimepewa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majukumu ambayo kimepewa kisheria yanasema chama hiki kina wajibu wa kisheria wa kulinda na kusaidia jamii katika masuala ya kisheria. Kwa hiyo, si kosa Mwenyekiti wa TLS akizungumzia uvunjwaji wa haki za binadamu ndani ya nchi hii. Si kosa Mwenyekiti wa TLS akizungumza kwamba Tanzania tuna uchaguzi ambao siyo huru, si kosa Mwenyekiti au kiongozi wa TLS akizungumza kuhusu mauaji au shida mbalimbali ndani ya nchi hii, si kosa. Si kosa kwa sababu ni wajibu anaopewa yeye ndani ya sheria ambayo imeweka TLS katika nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kusema kwamba sasa viongozi watakuwa wanachaguliwa ni watu ambao wametoka kwenye *chapters*, tukiangalia hizi *chapters* wanachaguana vipi, *chapter* ni kitu gani, hii kanda ni kitu gani, inaundwa na watu gani ambao hasa ndio wanaokuja kuwa hao viongozi ambao wanaenda kuwachagua viongozi kule juu.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikiangalia mfano Geita wale wanasheria iwe ni kumi, kumi na tano wataungana na sehemu nyingine, wanasheria wengi wako Dar es Salaam. Hiyo kanda tunaziundaje na uwakilishi wa maana tunaupata namna gani vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanaosema hata CCM na CHADEMA watu hatuji kote, lakini tunasahau kwamba hivi ni vyama vikubwa. Tunaanzia ngazi ya matawi, wanachama wanachagua, tunaenda ngazi ya kata viongozi wanachagua, tunaenda mpaka ngazi ya Taifa. Hizi ni chaguzi za kanda ambazo hazitakuwa na *grassroot levels*, hazina *grassroot levels* unazifananishaje na chama cha siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nashawishika kusema kwamba, umefika wakati nchi hii haipendi mambo mazuri, umefika wakati nchi hii tunaharibu vitu vizuri ambavyo vipo, hatutaki sauti tofauti, hatutaki sauti ya kuwatetea wananchi, ndiyo maana tunataka kuharibu mpaka uongozi unaotengeneza hiyo TLS. Kwa hiyo, hebu tuwe watu wa tofauti kidogo tuangalie na kwenye Kamati ya AG walitusomea kwamba wanabadilisha TLS kwa sababu ya mambo ya kimaadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni watu wazima, mimi nina zaidi ya miaka 18, humu Bungeni tunajuana vizuri, hivi utasema Upendo nisiwe mbunge kwa sababu ya suala la kimaadili! Haiingii akilini tusije Dodoma kwa sababu ya masuala ya kimaadili, haiingii akilini, kwa sababu ya gharama hawa ni watu wanaokutana kwa fedha zao, wanalipa na michango wenyewe, mnasema kuna gharama. Tena kibaya zaidi ni kwamba tukiwachagua kwenye *chapters* itabidi wale viongozi sasa walipiwe nauli ili waende wakakae kama ni watu 300, watu 500 *then* wachague uongozi ambao unahusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba sana kwamba tufanye utaratibu ambao ...*(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Upendo kwa mchango wako na ushauri wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Sixtus Mapunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Msigwa na Mheshimiwa Joseph Kakunda ajiandae.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.8) wa mwaka 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa muda naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye eneo ninalotaka kuchangia hususan mabadiliko ya sheria kwenye Chama cha Mawakili Tanzania (TLS).

Mheshimiwa Spika, hiki chama kiliundwa mwaka 1954 kikiwa na Mawakili 14 au chini au *plus* au *minus*. Katika kipindi kile iliwezekana kabisa hao watu wakakaa katika chumba kimoja wakajadiliana, wakamaliza kila kitu, nadhani ule ndiyo ulikuwa msingi wa aina ya demokrasia wanayoongelea na mimi naikubali kabisa. Ndiyo msingi wa historia ya demokrasia hata kule Athens, Ugiriki walipoanza kushiriki kidemokrasia walikuwa wanakutana pamoja, wanajadiliana pamoja na kutoa masuluhisho pamoja. Walipozidi kuongezeka na changamoto za wingi wao zilipokuwa kubwa wakalazimika kuwa na uwakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa kwenye Kamati, wadau walitueleza sasa wanafika 8,000 na watakwenda 10,000 ikifika mwishoni mwa mwaka huu. Kwa jinsi Vyuvo vya Sheria

vinavyoongezeka na *performance* inavyozidi kuendelea kuna uwezekano ndani ya miaka michache tukawa na wanachama zaidi ya 25,000. Kwa watu wote wenye busara na wanaoangalia mbali na wenye mtazamo mpana wanajua kabisa sheria ya mwaka 1954 iliyoweka pamoja wakikutana wakiwa 14, leo wakiwa 8,000 imethibitisha pasipokuwa na shaka lolote inatakiwa ifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yawezekana tu mazoea kama ilivyokuwa kawaida watu huyakimbia mabadiliko, lakini ukweli wa mambo wametudhibitishia kwenye kamati ingawa wako 8000 haijatokea mkutano hata mmoja wao waliwahi kufika 2000 *attendance*. Tafsiri yake ni nini, tafsiri ya kwanza hawa watu wanahitaji uwakilishi, kama walikuwa 8000 kwa sheria hii hii hawakuwahi hata siku moja kwenye mkutano wao mkuu kule Arusha waliwahi kufika 2000 tafsiri yake wanahitaji uwakilishi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kuna watu wanasema kutengeneza *chapters* katika uwakilishi aidha katika *level* ya mkoa au katika *bar* yoyote ile ipe tafsiri yoyote ile inasema watu wanasema unawapunguzia watu uhuru wao wa kushiriki na kuamua mambo. Mimi bado sielewi unaposema mimi nikiwakilishwa na watu wangu nikienda kusema mambo ya watu waliyonituma ni kwamba nimepunguza uwakilishi. Kama hiyo, ndio kesi basi tukubaliane humu ndani hatuwakilishi watu tumebana nafasi ya watu wa majimboni kwetu wangukuja wote wakae hapa Bungeni tujadiliane, lakini hii haiwezi ikawa hoja, tunajadili *TLS* ambao ni mdau mkubwa wa sheria nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mkutano wa watu 8,000 mtajadili nini? Mtakaa siku ngapi? Tuna *experience* hapa mikutano yote mkuu tuchukue tu chama cha siasa ambacho okay kuna mmoja hapa amesema sisi tuna historia ya *grassroot* tumepatikana tumechaguana kwenye shida ile sio hoja, hoja hapo ni uwakilishi, umepatikana vipi jinsi ya taasisi yako ilivyo ndivyo itakavyokutafsiri. Hoja ya msingi kwenye *congress* mnapokutana kwenye mkutano wenu mkuu wa CHADEMA au mkutano wetu mkuu wa CCM au mkutano mkuu wa CUF, mkakutana pale watu 2,000 mnajadili nini ndio kwa maana uwakilishi baada ya kujua taasisi yenu ina watu wengi sana ili mwakilishe vizuri, ili mjadiliane vizuri, ili *m-digest* kila kitu vizuri kama taasisi mahususi ya kisheria nchini lazima uwakilishi uwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi yangu hata ukaweka hizi hoja nyingine zote ukaweka pembeni mimi naitizama *TLS* katika ukubwa wake katika miaka kumi ijayo. Naitizama *TLS* ikiwa na wanachama 50,000 halafu muone ugumu wa kupata *congress*, watalazimika kukaa kwenye uwanja wa mpira watu 50,000 itakuwa ni shida huku mbele, lakini si hoja itasumbua vilevile hata kwenye akidi kama hii ya leo tu 8,000 hawakuwahi kufika 2,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali na niipongeze kwenye hili tunapo pa kuanzia watu wa *TLS* wameshatudhibitishia katika 8,000 hawakuwahi kufika 2,000 wanahitaji uwakilishi vilevile ni mfumo bora utakaofanya wajadiliane vizuri. (Makofi)

Kuhusu asilimia 70 ya mawakili wote kuwa Dar es Salaam ni hoja ya kawaida kabisa, inatafutwa utaratibu unaowezekeka ili uwakilishi wa Dar es Salaam uwe mkubwa zaidi. Haiwezekani watu wa Dar es Salaam wako asilimia 70 wakafanana na watu wa Songea, mimi ninaamini kanuni zitatupelekea...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kw amuda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mapunda kwa ushauri wako.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana tunaendelea Mheshimiwa Peter Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi nataka nizungumzie kifungu cha 31 cha muswada kinarekebisha kifungu cha 190(1) cha sheria mama kinachotaka mtu akitaka kuishtaki Halmashauri (*Local Government*), badala ya kutoa *notice* ya siku 30 atoe *notice* ya siku 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekuwa nikijiuliza swali Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu duniani kote sasa hivi ulimwengu unataka sheria ambazo ni rafiki kwa raia sio kandamizaji na sheria zilivyotungwa zinatungwa lazima *zi-relate* na uchumi. Sheria kama hii ni sheria ambayo inataka raia waogope Serikali, waone ni dudu fulani sio la kuliuliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kukwepa jinsi ambavyo wananchi wana-*interact* na Serikali yao. Ukienda kwenye *Local Government* kule kuna watu wanazika, watu wanafanya biashara, wanaiuzia *Local Government*, wakandarasi wanafanya shughuli zao. Sasa Serikali mara nyingi imeshindwa kulipa fedha kwa mfano watu wanaidai Serikali. Sasa badala ya kupunguza muda namna ya hawa watu kupata haki zao Serikali inaongeza muda zaidi kuwapa ugumu hawa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, raia wengi wana madeni, wamekopa benki, wanataka wafanye biashara zao, uchumi ukue, Serikali inaweka mazingira magumu ili hawa watu wasipate haki zao. Ulimwengu wa leo unataka vitu vinavyokwenda haraka haraka.

Mimi sielewi Mwanasheria Mkuu hii sheria unayotuletea mabadiliko haya yanaturudisha nyuma, tunaenda *backward* kimsingi na nakumbuka hapa mlipoleta Sheria ya Takwimu ilikuwa sio *computable* kimataifa ndio maana mkabanwa tena mkaja mkairudisha hapa. Ni sawa na sheria hii sasa katika ulimwengu wa leo wa kiuchumi mnapowabana hawa watu maana yake mnawatengenezea mazingira magumu. Mtanzania wa kawaida hakwepi kui-*interact* na Halmashauri yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili wawekezaji waje katika nchi, ili watu wafanye biashara lazima waone kwamba kuna urahisi wa kupata haki zao na kwa bahati mbaya katika nchi hii mtu akiipeleka Serikali mahakamani anaonekana sio mzalendo na ndio maana mnaweka hizi sheria nzito ili mtu aonekane kwamba haishimu Serikali, mnaweka mazingira magumu siku 90, lakini ukienda hata kwenye Serikali Kuu mwanzoni walikuwa wameweka zile siku 90 Mheshimiwa Chenge utakubaliana na mimi kabla ya hapo ilikuwa lazima uripoti/utoe taarifa kwa Waziri. Baadaye mkabadilisha kwa sababu mazingira hayo yalikuwa magumu kwamba kwa nini mtoe ripoti kwa Waziri ili kuishtaki Serikali lakini bado sababu nyingine *State Attorney* walikuwa wachache sasa hivi hawa *State Attorney* wako kila mahali kwa nini tunaweka mlolongo huu wa kuongeza shida kwa wananchi kuishtaki Serikali yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kibaya zaidi hiyo *Local Government* ikitaka kumshtaki mtu binafsi kesho tu inamshtaki, lakini Serikali inataka ipewe muda wa siku 90 huu ni ukandamizaji na ukandamizaji ambao unawaonea raia wa kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii sio *monarchy*, tukumbuke dunia inaenda mbele, dunia hairudi nyuma, dunia imekuwa ikikua ikipevuka hii nchi sio *monarchy*. Wakati wa utawala wa kifalme mfalme hata watu wanakuwa ni mali yake, mfalme anataka watu wamuogope, hii ni *republic* kwenye *republic* kuna *liberty*. Ukisoma Thomas Jefferson anasema; "*When the people fear the Government there is tairan when the Government fears the people there is liberty.*" Ulimwengu wa leo tunazungumzia *liberty* unapokuwa na *liberty* maana yake watu wanafanya kazi kwa raha, kwa haki, bila uonevu na kama kumetokea *dispute* waone kuna uharaka wa

kwenda kupata haki zao na ndio maana kama haki zao hazipatikani kwa urahisi watu huwa wanaamua kuchoma watu moto, watu wanachukua sheria mikononi kama vyombo vya haki havitendi haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mnapotoa kutoka siku 30 kupeleka siku 90 maana yake mnaweka mazingira magumu ya watu kudai haki zao na bado hata kama hizi msingeweka Serikali bado ina nafasi ukipeleka hizo 90 bado ukienda mahakamani kama hujajiandaa unaweza ukamwomba Jaji kwamba akuongezee muda na bado unapewa siku 21, ukipewa siku 21 tena anakupa muda mwingine kwa nini tunaweka mazingira magumu ya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini linalofanana na hili ni hili la Chama cha Wanasheria; pamoja na maelezo mazuri ambayo yanazungumzwa sio siri Serikali mnataka kuwadhhibiti wanasheria ambao hawa ni Maafisa wa Mahakama ambao wanatakiwa wasaidie wananchi kujua haki zao kuna ubaya gani wananchi wakijua haki zao, wanapojua haki zao wananchi wanaweza kuiadabisha Serikali na maana yake watumishi wa umma wanakuwa na nidhamu kwa wananchi wao wanafuata taratibu, kanuni na sheria tulizojiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawahitaji hawa wanasheria wasiingiliwe katika mambo yao. Kwa nini tunataka kuwabana, kwa nini tunataka kuwaminye? Tunataka kuwaminye kwa sababu tunataka Serikali iwe ni lidude fulani linaloogopwa, linalotisha ambalo... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Msigwa. Tunaendelea Mheshimiwa Joseph Kakunda.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, awali ya yote napenda kutangaza kwamba naunga mkono hoja hii ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini napenda nitoe maoni yangu kwenye maeneo mawili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni eneo la kuweka utaratibu wa usuluhishi kwenye kesi za madai. Suala hili ni zuri sana kwa sababu kwanza litapunguza mlundikano wa kesi katika mahakama zetu, lakini wasiwasi wangu uko katika wakati Waziri atakapokuwa anatunga kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Waziri atatunga kanuni inayoweka msuluhishi awe Jaji au Hakimu ambaye hajapangwa kusikiliza kesi hiyo bado huyo Jaji au Hakimu atakuwa hajatoka nje ya mfumo wa mahakama. Kwa hiyo, mimi nilikuwa napendekeza wakati Waziri atatunga kanuni asiweke msuluhishi ambaye hatoki ndani ya mfumo wa mahakama akawa huru kabisa anatoka ka wananchi maana yake anaweza akawa *bias* anaweza akawa anachukua upande kwa hiyo akaumiza upande fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza wakati Waziri atakapokuwa anatunga kanuni akumbuke kuweka mtu mwenye *status* ya ulinzi wa amani ambaye ana madaraka ambayo yanamfanya (*yanam-pin*) aweze kutenda haki katika usuluhishi huo, hilo ndio jambo la msingi ambalo nilikuwa napendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kuweka utaratibu utakaomhusisha Mkurugenzi wa Halmashauri kwenye mashauri yanayohusu Serikali za Vijiji na maamuzi yake kisheria ikiwemo hitaji la *notice* ya siku 90; hili nalo ni zuri sana kwa sababu kwenye Serikali za Mitaa kuna ngazi mbili, kuna ngazi ya juu ya Serikali za Mitaa ambao ni Halmashauri ya Wilaya au ya Mji au ya Jiji. Wale wamekuwa wakilindwa sana kwenye kesi kwa kutetewa na wanasheria wa Halmashauri husika. Sasa hii Serikali ya chini kwa maana ya Serikali za Vijiji na maamuzi yake imekuwa mara

nyingi wanaachwa nje kama kuna shauri lolote katika mahakama wanasheria wengi katika Halmashauri na wa Serikali wamekuwa wakisema hayo mashauri hayo kwa sababu yamefanyika kijijini yanawahusu wao wenyewe. Kwa hiyo, baadhi ya vijiji na baadhi ya Wenyeviti wa Vijiji na baadhi ya Wenyeviti wa Vitongoji wamekuwa wakishtakiwa mahakamani *in person*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kweli naipongeza sana Serikali kwa kuchukua hatua hii ya kuhakikisha kwamba maamuzi ya kisheria, maamuzi yoyote yanayofanywa katika ngazi ya Serikali za chini za mitaa, nao walindwe na wanasheria wa Halmashauri na wanasheria wa Serikali Kuu. Hilo suala limekuwa ni zuri sana na litasaidia utendaji kwenye Halmashauri zetu nyingi za vijiji na vitongoji na watafanya kazi zao kwa kujiamini kwa sababu sasa watakuwa wanalindwa na sheria, lakini watakuwa wanalindwa na mfumo wetu wa sheria kwa kutefewa na wanasheria wa Serikali. Hili jambo kwa kweli ni zuri sana na naliunga mkono kwa asilimia 100 tumechelewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono hoja teba nashukuru sana kwa nafasi hii. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Kakunda kwa ushauri na mchango wako mzuri.

Sasa nimehitimisha, mtoa hoja atatanguliwa na Mheshimiwa Ulega, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa muda usiozidi dakika sita ujielekeze kwenye maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wame-express concern ambayo ni muswada *clause* 21 na 22 nadhani ndio hayo, lakini *your free* upanue uwanja karibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia. Nashukuru kwa michango ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia na nimezisikia hoja zao, lakini kwenye muswada huu kifungu hiki cha 21 sisi tumeboresha sheria mama. Ukisoma sheria mama ambayo ni Sheria ya Uvuvi namba 22 ya mwaka 2003 kuanzia *section number 8(3)(a),(b),(c)* na kipengele cha 4 ambacho sisi sasa ndio tumekiboresha tayari vifungu vyote hivi vilishatoa huu uelekeo. Hapa kuna maboresho madogo.

Waheshimiwa Wabunge ni kwamba sheria mama ilikuwa tayari inatupa sisi mamlaka toka hapo mwanzo. Ukisoma kifungu cha 3 na 4; kifungu cha 3 tayari kimemtaja Mkurugenzi na mamlaka yake ya kuisimamia sekta ya uvuvi katika maeneo yote ya nchi yetu na ku-oversight namna ya shughuli za usimamizi na ulinzi wa rasilimali tayari imetaja. Tulichokifanya sisi katika maboresho haya ni kwamba kile kifungu cha 4 ambacho ndio tumekirekebisha tumeongeza mambo kadhaa na mambo yenyewe mwanzo Waziri wa Uvuvi alikuwa hawezi kuchukua hatua hata unapokuwa uvuvi haramu umekithiri katika eneo lile na ikumbukwe kutokana na utaratibu wetu wa *D by D* asilimia 80 ya shughuli zote za uvuvi zinasimamiwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi tukasema kwa kuwa jambo hili limeonekana halifanyi vizuri tukampa meno Waziri wa Uvuvi achukue hatua, akishamaliza kuchukua hatua ndio sasa atawasiliana na Waziri wa TAMISEMI washauriane juu ya nani atakayesimamia shughuli ile na hapa kuna *options* mbili. Ya kwanza atakayesimamia atakuwa ni jirani yake kwa mfano Halmashauri ya Ukerewe jirani yake na ikijuonekana kwamba yuko mbali atakayesimamia itakuwa ni Wizara na katika sheria hiyo sheria mama maana Mheshimiwa Makamba alisema kwamba je, mapato ya Halmashauri ile inayonyang'anywa yanakwenda wapi?

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria mama kifungu kidogo cha 6 kinaeleza wazi iko hapa ni nani atakayesimamia hayo mapato na sisi hatujaigusa ile ya nani atakayesimamia mapato iko vilevile katika sheria mama. Kwa hiyo, kimsingi hapa maboresho tuliyoyafanya ni kumpa meno Waziri wa Uvuvi aweze kuisimamia sekta vizuri ili kusudi Halmashauri ambazo zinaonekana suala hili kwa mfano Halmashauri ya Ukerewe over 90% ya mapato yake yanatokana na shughuli ya uvuvi, lakini angalia ni kiasi gani ambacho wanakirudisha kwenda kusimamia hiyo shughuli ya uvuvi utakuta kwamba ni kiasi kidogo sana au hakuna kabisa. Kwa hiyo, hii ndio hoja ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili lile la *fines* naomba niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kwamba katika sheria mama kifungu cha 47 kili-generalize mvuvi mdogo kabisa na yule mzalishaji wa nyavu kiwandani au mwenye kiwanda cha ku-process minofu wote walikuwa wanachukuliwa na sheria moja hiyo hiyo. Sasa tunadhani kwa sheria ile ya shilingi 100,000 mpaka 1,000,000 hawa wahalifu wakubwa tumekuwa tukiwakosa, watu wanaingiza samaki wenye sumu makontena na makontena, lakini akiingia unakwenda na sheria hii namba 47 faini yake ni shilingi 100,000 hadi 1,000,000. Kwa hiyo, matokeo yake sisi kama Taifa tunapata hasara, ndio maana tukasema tugawanye ndio tukaja sasa na sheria hii ya *amendment* namba 23 ambayo Mheshimiwa Makamba alileta *clause* ile ya kwamba tuiondoe, tukasema tu-categorize tuweke mafungu mawili; wale wahalifu wakubwa na wahalifu wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahalifu wakubwa tukasema watapigwa faini isiyopungua milioni 10 mpaka milioni 50 isizidi hawa ni mapapa, wanaozalisha nyavu ambazo zinaenda kuwaumiza wavuvi wadogo. Hawa wadogo tukasema watalipa shilingi laki mbili na isizidi milioni 10 ndio sheria hii hapa namba 47 mapendekezo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha ahsante sana naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye hilo ungelibasaidia tu kusoma kifungu cha sheria kuhusiana na faini vinavyosomeka sasa hivi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kifungu cha sheria mama, kinasema kama ifuatavyo kwa ruhusa yako naomba kunukuu; “ Any person who contravenes the provisions of this Act other than those who specify penalties, upon conviction should be liable to a fine of not less than 100,000 shillings and not more than 1,000,000 shillings.” Ime-generalize wote ndiyo tukasema tu-categorize kwa sababu hapa kuna kundi kubwa la wahalifu tunalikosa ambalo ndilo linawafanya wavuvi wetu wadogo waingie katika makosa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo katika *consultation*, mimi na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika ile sheria ya kwanza namba 21 kimsingi tumekubaliana. Mwanzo sheria mama ilikuwa inataka mimi nifanye *consultation* na Waziri wa TAMISEMI, lakini jambo hili lime-prove *failure*. Sasa tukaamua sisi tuta-suspend, tukishamaliza ku-suspend zile shughuli tutawasiliana na Waziri wa TAMISEMI tukubaliane ni nani atakayesimamia shughuli zile baada ya kuwasiliana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali tumekubaliana tuiboreshe kidogo. Kabla ya ku-suspend Mwanasheria Mkuu wa Serikali analeta *amendment* kwamba mimi nitam-notify Waziri wa TAMISEMI juu ya nia yangu ya kusimamisha Halmashauri ile inayoonelana haifanyi vizuri.

MWENYEKITI: Sawa sawa, nadhani tunaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, una muda usiozidi dakika 15.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala huu unaohusu Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 8 ya mwaka 2019. Tumepata jumla ya michango 11 kwa mdomo lakini pia kwa maandishi kuna Waheshimiwa Wabunge watano waliochangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na mchango wa hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ambayo nitajielekeza hasa kwenye hoja inayohusu sheria ya Mawakili ndiyo imejitokeza kwa nguvu zaidi lakini pia wachangiaji wengine wameigusia na kuna hili suala la mikutano ya mawakili na Kambi Rasmi ya Upinzani na baadhi ya wachangiaji wanapendekeza turudie utaratibu wa zamani, lakini na baadhi ya wachangiaji wameeleza vizuri. Uzoefu unaonesha kwamba utaratibu huo wa zamani wa kukutana mawakili wote sio tu kwamba hauna tija, lakini umekuwa haufanyi kazi na matokeo yake maamuzi yamekuwa yanaishiwa kufanywa na kikundi cha watu wachache na tunaona mazingira kama haya yakitokea kwenye vyama vingine vya namna hiyo njia bora ni kwenda kwenye uwakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia palikuwa na aina fulani ya tuhuma kwamba Serikali inaingilia Chama cha Mawakili. Labda nianze kwa kueleza kwamba Chama hiki cha Mawakili sio chama cha kibinafsi kwa asilimia 100, si kweli! Kwa sababu chama chenyewe kimeanzishwa kwa Sheria ya Bunge, hakikuanzishwa kwa labda *memorandum of understanding, constitution* au namna yoyote. Imeanzishwa kwa Sheria ya Bunge maana yake ni kwamba Bunge lilikaa likapitisha sheria ya kuanzisha chama hiki. Kwa hiyo, isifike mahali wanachama wa chama hiki wakaisahau historia na wakaanza kudai kwamba ni chama binafsi kwa asilimia 100, si kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia zipo sababu kwa nini Serikali ni lazima iangalie hiki chama kinafanya nini, kwa sababu Mawakili hawa ni Maafisa wa Mahakama (*Officers of the Court*), lakini pia ni *notaries public*, ni watu wanaoshuhudia viapo na ni *commissioners for oath* yaani wanashuhudia viapo na nyaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti haya kimsingi yanajulikana ni majukumu ya Serikali, lakini Serikali imeyakaimisha majukumu hayo kwa mawakili binafsi na ndiyo maana miongoni mwa mawakili hawa binafsi kuweza kuteuliwa hata Majaji na tunafahamu wako wengi wameteuliwa kutoka miongoni mwa mawakili hawa. Kwa hiyo, ni lazima Serikali iangalie chama hiki kinajiendesha namna gani na kama zikionekana dosari na kasoro ni lazima Serikali izifanyie kazi kwa sababu kama huko ndiyo unaweza ukatoa Majaji, hawa ndiyo wanashuhudia viapo, wana majukumu mengi sana makubwa huwezi ukawaacha wakaenda wanavyofikiri wanaweza kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mchango ulitoka kwa Mheshimiwa Ally Saleh alizungumzia hivyo hivyo Chama cha Mawakili, lakini maelezo ndiyo hayo niliyokwisha yatoa.

Aidha, Mheshimiwa Lubeleje alizungumzia mabadiliko kwamba una suala la madai, lakini baadae linageuka kuwa jinai, nilitaka kueleza tu kwamba inategemea na matukio yanayotokea mle.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano watu wanaweza kuwa wanashtakiana kwa masuala ya ardhi, lakini mmojawapo ameingia tena inaitwa kabisa ameingia kwenye ardhi ile kwa jinai kwa hiyo kutakuwa na kesi hapo ya kudaiana nani mmiliki hasa wa ardhi, lakini pia inaweza ikaibuka jinai kwa sababu mmojawapo wa wale watu aliingia kwa jinai kwenye ardhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya Sheria ya Mtoto ameyazungumzia pia Mheshimiwa Lubeleje, lakini akasema ni vyema kufanya mabadiliko ya Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kurudia kwenye sheria hizi kile ambacho Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ameshazungumzia. Unapogusa Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mirathi zina changamoto kubwa sana. Sheria hizi zinagusa imani za dini, mila na desturi na kwa hiyo, huwezi kufanya haraka yoyote katika kuzibadilisha. Kuzibadilisha kwake kunahitaji mashauriano mapana katika jamii na ni lazima muwe na muafaka ambao utazingatia hizo hisia za kidini au misimamo ya kidini, mila na desturi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mkundi amezungumzia suala la sheria ya uvuvi na lile suala la kuiondolea Halmashauri mamlaka ya kusimamia sekta na pia kiwango cha faini. Kwenye kiwango cha faini Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi amelieleza, lakini kwenye hili suala la kuiondolea Halmashauri mamlaka ya kusimamia sekta ya uvuvi, napenda kusema kwamba baada ya mashauriano ndani ya Serikali kwa haraka tumeona ni vyema tufanye mabadiliko kidogo. Kwa hiyo, tuna *further schedule of amendments* ambayo italetwa na Serikali kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwakasaka amezungumzia juu ya *Tanganyika Law Society* kwa ujumla. Mheshimiwa Dkt. Tizeba amerudi kwenye suala la uvuvi na faini na nimekwishaeleza, Mheshimiwa Mhagama amezungumzia maabara ya maziwa na kutoa pongezi na pia suala la Chama cha Mawakili Tanganyika. Namshukuru sana kwa kueleza kwamba uhalisia ndiyo huu kwamba chama hiki sasa kinakuwa na kitakuwa na wanachama wengi zaidi, haitawezekana kuwa na mikutano yenye tija wanapokutana mawakili wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Peneza amezungumzia suala la Chama cha Mawakili Tanganyika na anasema nafikiri Serikali inakiangalia chama hiki kwa jicho hasi, si kweli hata kidogo, nimeshaeleza kwa kirefu. Ni lazima Serikali iangalie chama hiki kinakaa katika misingi ya *professionalism* na si vinginevyo na inapona viashiria vyovyote vya kuipora ajenda ya chama hiki na kukipeleka kwenye uelekeo ambao si sahihi ni lazima ichukue hatua. Kama ilivyoelezwa sheria ilipotungwa kulikuwa na mawakili 14 sasa hivi ni 9,000. Mazingira yamebadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sixtus Mapunda naye amezungumza na ninamshukuru sana kulieleza vizuri suala la uwakilishi. Mheshimiwa Msigwa amezungumza suala la kuishtaki Halmashauri sasa ni siku 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze kidogo hapa, tatizo tulilokuwa nalo limekuwa ni tafsiri ya neno Serikali kwa sababu utaratibu wa kisheria wa kutoa *notice* wa siku 90 unapoishtaki Serikali umekuwepo siku zote kwenye *Government Proceedings Act* na unajulikana, lakini shida ilikuwa ninii tafsiri ya neno Serikali. Sasa tukirudi kwenye Ibara ya 6 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iko wazi, Serikali ni pamoja na Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Kwa hiyo, tulichofanya ni kurekebisha tu hiyo dosari ambayo imekuwepo na siku 90 bado ni muhimu sana kwa sababu siku hizi pia Serikali inapenda pia kufanya uchunguzi juu ya madai yanayoletwa dhidi yake kuona kama ni sahihi kwa sababu pia yamekuwepo madai mengi *fake* dhidi ya Serikali, lakini pia kama kuna madai sahihi Serikali pia inapenda siku hizi kufanya majadiliano. Kwa hiyo, ndani ya hizo siku 90 Serikali inaweza ikaamua kwamba nadhani hapa inafaa kufanya majadiliano badala ya kwenda kwenye mlolongo mrefu wa Kimahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwisho Mheshimiwa Kakunda ametoa pongezi kuhusu suala la usuluhishi, lakini akatoa tahadhari kwamba zinapotungwa kanuni basi msuluhishi asiwe Jaji au Hakimu. Hapa nieleze kidogo tu kwamba tofauti na mifumo iliyopo kwa sababu ipo tayari mifumo ya usuluhishi na inatambulika kisheria. Kuna usuluhishi ambao unahusisha na Mahakama (*Court Amnesty Mediation*), kuna usuluhishi kwenye mambo ya ndoa, upo utaratibu wake wa kisheria, kuna usuluhishi kwenye mambo ya kazi, kuna usuluhishi wa mambo ya ardhi.

Sasa sheria au mabadiliko haya yanagusa ule usuluhishi mwingine ambao hauguswi au hauingii katika maeneo hayo niliyoyataja ambayo yana sheria zake. Sasa kwenye usuluhishi huu unaotengenezewa haya mabadiliko ya sheria hapa wale wahusika wenyewe katika mgogoro ndiyo wataamua wanauendeshaje usuluhishi wao na mwisho watakapokubaliana wakielewana, wakipenda wataweza ku-register yale makubaliano yao. Kwa hiyo, kwenye hili hawatapangiwa awe Jaji au Hakimu, watapanga wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri na tumeipokea na tutaendelea kupokea ushauri huu mzuri unaotoka kwa Waheshimiwa Wabunge na kuufanyia kazi ndiyo maana baada ya mashauriano na Kamati ya Katiba na Sheria iliyopitia Muswada huu, Serikali imeleta Jedwali la Marekebisho (*schedule of amendments*) hata muda mfupi uliopita tena tumeongeza *further schedule of amendments* na hii inaonesha kwamba Serikali ina usikivu na kupokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kutoa tena hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maelezo yako mazuri. Sasa twende kazini, Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 8 wa Mwaka 2019 (*The Writen Laws (Miscellaneous Amendment No. 8) Bill, 2019*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. BAKARI KISOMA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Kamati yako ijielekeze kwenye Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 8, 2019. Na sasa tujielekeze ukurasa wa tano wa Muswada huo.

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 6

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, eneo hili lina marekebisho ya Serikali, unaangalia marekebisho ambayo yamefanywa na Serikali, tumuone na Mheshimiwa Salome anasema nini kwenye eneo hilo. Mheshimiwa Salome.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba tu nianze kwa kusema kama sitaridhishwa na majibu ya Serikali nitaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono.

Katika kifungu hiki Serikali hasa kifungu cha 6 ambacho kinarekebisha kifungu cha 64(a)(2) wanasema; *for purposes of facilitating, conciliation, negotiation and mediation, the Minister may make rules prescribing for procedures, forms and other matters relating to conciliation, negotiation and mediation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu nilikuwa naiomba Serikali sehemu ya *Minister* waweke *Chief Justice* kwa sababu pamoja na maelezo aliyoyatoa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema kwamba *Minister* atatengeneza *rules* na *regulation* kwenye mambo mengine mengine, lakini sheria tunayojadili hapa ni *civil procedure code*, ni sheria ambayo inatumiwa na Mahakama katika kuendesha makosa ya madai. Sasa hayo makosa mengine mengine ni yapi, sheria iliyopo hapa *Chief Justice* ndiyo *custodian* dniyo anaitumia sana, Mahakama ndiyo inaitumia. *Minister* hawezi ku-make *regulation* kwa ajili ya kuendesha Mahakama.

Kwa hiyo nilikuwa naomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali anikubalie kwamba badala ya kuweka neno *Minister* tuweke neno *Chief Justice*.

MWENYEKITI: Kwa maana nyingine wewe huna tatizo na *additions* ya vifungu viwili vipya vya 3 na 4 vya marekebisho ya Serikali ambayo Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu ameyafafanua vizuri wakati ana *wind up*, wewe uko katika ile 2 ambayo inamtaja Waziri, wewe unapendekeza iwe Jaji Mkuu. Mheshimiwa AG.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kama Mheshimiwa Salome Makamba angekuwa amejielekeza kwenye *schedule of amendments* ile ya Serikali hasa ile namba 4 angeona kusingekuwa na umuhimu wowote wa kuleta mabadiliko aliyopendekeza. Ile namba 4 naomba niisome; *The provisions of this section shall not apply to any matter for which the manner and procedure or settlement has been stipulated in any other written law.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwenye majumuisho yangu nimeeleza yale maeneo mengine ambayo *mediation* au *negotiation* au *conciliation* kuna sheria na *procedure* imeshakuwa *provided*. Kinachokuwa *introduced* hapa ni *process* ambayo haijafika kwenye Mahakama *per se*. Hizi ni *process* zinazofanyika kabla hujafika kwenye Mahakama *per se* ndiyo maana nikasema ni *parties* wao ndiyo wataamua usuluhishi. Tulikuwa hatuna sheria inayotambua hicho mbali na yale maeneo manne au matano niliyoyaeleza ambayo yana sheria yake. Usuluhishi mwingine ulikuwa hautambuliki, kwa hiyo, sasa tunataka kuutambua kisheria. Lakini hizi hatua zote tunazosema *conciliation, negotiation and mediation* zinafanyika kabla hujafika mahakamani na kwa hiyo ipo nje ya wigo wa mamlaka ya *Chief Justice*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namuelewa *Attorney General* anachotaka kukifanya, lakini sheria nyingi yaani ukisoma sheria za kila Wizara kwa mfano Wizara ya Uvuvi au Wizara ya Madini wana taratibu zao ambazo zimewekwa kwenye sheria zao ambazo *Minister* yupo *responsible* kufuata kama anataka kusuluhisha. Hii sheria ni *Civil Procedure Act* na *Civil Procedure Act* ina utaratibu mzuri tu wa *mediation* na *reconciliation* ambayo wanaita ni *Court Arbitration* na *Court Mediation* zipo, sasa labda kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali ana kitu anachokifikiria ambacho mimi sikioni, lakini ukisema unataka kuingiza *Minister* kwenye *Civil Procedure Code* wakati kuna *Chief Justice* na kuna *Court Mediation and Arbitration* ambazo zipo *governed* na hiyo sheria, mimi sikubaliani na anachokisema Mwanasheria wa Serikali. (Makofi)

MWENYEKITI: Kwa hiyo?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba Wabunge wenzangu najua *this is very technical* kama wamenielewa kile ninachotaka kukisema waniunge mkono.

MWENYEKITI: Hujaungwa mkono kwa hiyo, mmeelewa hoja lakini?

WABUNGE FULANI: Ndio.

MWENYEKITI: Haya umeungwa mkono basi. Haya nisionekane kwamba na-*bulldoze* Waheshimiwa Wabunge. Haya imeungwa mkono tuone nani wanataka kusaidia upande wa Serikali, AG mwenyewe ataliweza hili, hii *very technical* mimi ningependa amelieleza vizuri tu. Mheshimiwa Mwakaganda siku hizi na wewe mwanasheria? Haya changia, Mheshimiwa Msigwa hajasimama sasa mna..., kuunga mkono hoja ama? Mimi nilidhani unataka kuunga mkono tu.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisimama tumekaa tu.

MWENYEKITI: Haya bwana. Mheshimiwa Msigwa ndio tunaanza na wewe, dakika tatu tu.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo analojaribu kulizungumza...

MWENYEKITI: Ujielekeze kwenye hoja ndio maana nimeuliza...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Eeh! nazungumzia hoja hiyo hiyo. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja anayoizungumza Mheshimiwa Salome Makamba kwanza kabisa Waziri sio lazima awe mwanasheria, hatutegemei kwamba lazima Rais amteue mwanasheria. Kwa hiyo, kumtwika wakati mwingine Waziri masuala ambayo ya kisheria kwa kuamini kwamba lazima awe mwanasheria ni kuitendea makosa kubadilisha/ kifungu cha sheria. Kwa hiyo, naunga hoja ya Mheshimiwa Makamba kwamba kipengele/kifungu hicho mapendekezo ya Mheshimiwa Makamba yakubaliwe ili tusiumingize Waziri kwenye shida ambayo inaweza ikawa sio yake, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Sophia.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa hii nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi ninamuunga mkono Mheshimiwa Salome Makamba, ninamuelewa anapozungumzia kwamba sisi kama Wabunge na watunga sheria ni lazima tuamini mamlaka za kimahakama na hasa anapotaka kusema *Chief Justice* liwekwe pale badala ya Waziri. Sisi sote tumeona Mawaziri wanaweza wakakaa ndani ya miezi sita wakabadilishwa Mawaziri zaidi ya mara tano, hii italetta mtafaruku katika utungaji wa sheria mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninakuomba Mheshimiwa Salome Makamba kile anachokisema lazima tukifuatilie, ahsante. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wasaidie tena kwa kifupi tu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa utatuzi wa migogoro unaweza ukaanza kabla ya kufika kwenye mahakama na mara nyingi mahakama ni hatua ya mwisho. Kwa kifupi kabisa tunachozungumzia hapa ni utatuzi wa migogoro kabla hujafika kwenye mahakama. Hata zile namna nyingine za utatuzi wa migogoro zimesemwa zimewekewa tu *platform* ya utatuzi wa migogoro, lakini sio mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye *commission for mediation and arbitration* sio mahakama *per se* ni *platform* ya utatuzi wa migogoro. Sasa kwa sababu hapa tunazungumzia suala la utatuzi wa migogoro kabla ya kufika mahakama ni suala la kijamii na kisera. Linapokuwa suala la kijamii/kisera lipo chini ya Waziri wa Katiba na Sheria; likishakuwa suala la kimahakama linaingia kwenye wigo wa Jaji Mkuu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Salome tunasema kisheria amejiipotosha mwenyewe na ningepotosha asijipotoshe zaidi, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Salome hitimisha hoja yako.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe hoja yangu kwa kusema kwamba anachokisema *Attorney General* kwamba Waziri anaweza akatunga kanuni za usuluhishi kwenye *Ministry* yake, weka kwenye sheria ya Wizara yake, lakini ukiweka kwenye *CPC* halafu unasema Waziri atunge kanuni, *CPC* yenyewe inazo kanuni za usuluhishi wa migogoro kabla ya mahakama, sijui kama ananielewa kwa hilo. Mwisho wa siku *Criminal Procedure Act* na *Civil Procedure Act* ni *tool* inayotumika mahakamani na kwa mawakili na *it is not true*, anadanganya kwamba hizi *mediation* zinazofanyika *arbitration* eti ni nje ya mahakama!

Mheshimiwa Mwenyekiti, utanisaidia *court arbitrator* anakuwa *appointed* na Jaji, kwa hiyo ukisema kwamba haijafika huko sio kweli. Kwa hiyo, kuingiza hiki kifungu kipya kwamba *Minister* ataingia kwenye mambo ya kanuni za uendeshaji wa kimahakama kwenye kesi za madai analeta *contradiction* ndani ya ibara ya mahakama. Kwa hiyo, kama anataka akaweke kwenye Sheria ya Uvuvi *for example* au Sheria ya Mazingira, *Minister* atunge huko ili wakishindwa walete mahakamani tufuate *court procedures* za kuendesha kesi ya madai na jinai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi sikubaliani na mawazo ya AG.

MWENYEKITI: Tuamue haukubaliani, tuamue tu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa tuamue hakuna tatizo.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Lakini kwa sababu tunatunga sheria lazima twende vizuri.

Kifungu cha 4 cha marekebisho yaliyoletwa na Serikali ndio yanasaidia kukufafanulia hicho *the provision of this section shall not apply to any matter for which the manner and procedure of settlement has been stipulated in any other written law.* Hiyo ndio inaweka wigo ule, wala usihangaike ni la kisera hili bado huku wananchi wanalalamika huko lazima Waziri aweke utaratibu. Ndio maana yale yaliyopo kwenye CPC sasa hivi ni utaratibu tu wa kujaribu kuipunguzia mahakama yetu mzigo wa kesi, lakini nadhani tuliamue tu.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)

Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 17

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)

Ibara ya 18

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 19

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)

Ibara ya 20

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 21

MWENYEKITI: Muangalie Waheshimiwa Wabunge, Serikali imekuja na *a further schedule of amendment*, lakini na Mheshimiwa Salome naye kwenye eneo hili ameleta mapendekezo yake. Mheshimiwa Salome.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena. Kwenye ibara hii Waheshimiwa Wabunge wenzangu ndio ile ibara ambayo Waziri wa Uvuvi ana nguvu ya kwanza kum-suspend mtumishi wa uvuvi kwenye Halmashauri ambaye ameshindwa kusimamia vizuri suala la uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio tu kum-suspend akishamaliza kumsimamisha kazi Waziri wa Uvuvi, mtumishi wa Halmashauri ameajiriwa na TAMISEMI lakini kama hiyo haitoshi anasema baada ya kum-suspend atamfahamisha Waziri wa TAMISEMI. Na mimi nasikitika Mheshimiwa Waziri Ulega wakati anatuelezea hapa ametupotosha sababu utungaji wa sheria *government moves on paper*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema kwamba wamebadilisha wanasema atam-notify halafu hakuna *amendment* yoyote ambayo imeletwa mpaka sasa hivi hapo, sijaiona. Kwa hiyo, hayo atatusaidia yeye kusema alikuwa anasema kwa *basis* gani au sivyo atakuwa alikuwa analipotosha Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, okay, atasimamisha, lakini kama haitoshi ibara hii nimependekeza hiki kifungu kifutwe kwa sababu kinaonesha kwamba wakiwa watumishi wa Halmashauri hawasimamii vizuri mapato ya Serikali yanayotokana na uvuvi kwenye Halmashauri, ana uwezo wa kuwanyang'anya mamlaka ya usimamizi na Mheshimiwa Waziri ameongezea hapa maneno yake ambayo hayapo kwenye sheria kwamba atawapa Halmashauri jirani wa-operate. Hiyo sheria ya wapi? Yaani hiyo sheria haipo popote, kwa hiyo, niombe maelezo ya Serikali na nisiporidhika wanajua hili Wabunge wenzangu wamenielewa na wataniunga mkono.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mabadiliko ya awali ukiangalia katika muswada yalikuwa yanasema; *the principle act is amended in section 8 by deleting sub-sections 4 and 5 and substituting for them the following*; ndio yanafuata hayo maelezo aliyoyaeleza Mheshimiwa Salome japokuwa hayakuwa na usahihi kwa sababu hayazungumzi ku-suspend mtumishi wa *local authority*, yalikuwa yanazungumza ku-suspend *the Local Government Authority from further operations and management of fisheries*. Kwa hiyo, ilikuwa ni ku-suspend *Local Government Authority* na sio ku-suspend mtumishi na inaendelea kama ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye *further schedule of amendments* Serikali imeleta nini; tumesema; *the principle act is amended in section 8 by deleting subsection 5*; kwa hiyo, sasa tuna-delete *only sub-section 5* kwa maana hiyo kwamba *sub-section 4* ambayo hapo awali pia tulikuwa tumeindoa inabaki, lakini sasa tunabadilisha *sub-section 5* peke yake na tunasema tui-substitute it with the following. Sasa hiyo *sub-section 5* mpya itakuwa inasomeka; *subject to sub-section 4, The Minister for Local Government Authority shall if satisfied that there is mismanagement of the functions related to the fisheries by the local authority take necessary measures to remedy the mismanagement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome umeelewa? Lazima kile ki-sub-section 4 ambayo ipo kwenye sheria sasa hivi na ndio inakuwa 5 hii inakuwa *predicated* yaani inaambiwa lazima uitambue inasema nini, ulisomewa na Mheshimiwa Ulega wanaweza wakarudia tena; tunatunga sheria hapa, sheria si unayo?

Sasa hivi mapendekezo ya Serikali kwenye eneo hili kifungu cha 8 badala ya kufuta vifungu viwili cha 4 na 5 sasa wanafuta cha 5 na kukiandika kama ilivyo kwenye *further schedule of amendment*. Kwa maana hiyo kile cha 4 kwenye sheria kifungu kidogo cha 4 kinabaki kama kilivyo. Ili uelewe sasa kinachopendekezwa na Serikali lazima ukisome hicho *subject to sub-section 4*, umechelewa sisi tunaendelea kuamua hapa, mimi nakusaidia tuelewe kwamba *you know* ngoma hii ni nzito. Umeridhika wewe? (Makofi)

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika.

MWENYEKITI: Sasa kama hujaridhika twende mbele.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya natoa hoja Wabunge wenzangu waniunge mkono.

MWENYEKITI: Hawajafika hata 10 jamani, mnahamasishana, hamna hiyo. Lakini Waheshimiwa tunatunga sheria, mimi nasema tuwe *consistent*, AG amelieleza vizuri sana *effort* ya Seikali kujaribu kujibu *concern* za Wabunge. Sasa kama hata sheria yenyewe hunayo mbele hapo si ni shida? Haya mimi *I have to be strict* kwa sababu tunatunga sheria. Ndio mnachangia wawili hao? Mheshimiwa Dkt. Sware.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria mama ya uvuvi ya mwaka 2003 inaonesha dhahiri kwamba mamlaka ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi zipo *under the fisheries officers* ambao wanaajiriwa na Mkurugenzi wa Halmashauri, hiyo ipo na Mheshimiwa Ulega ameshasema. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapo wanachokiongeza kama Wizara kwenye sheria hii wanasema sasa inampa mamlaka Waziri wa Mifugo na Uvuvi kama hajaridhika na ripoti inayotolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri kwenye kusimamia hizo rasilimali za uvuvi basi Waziri husika huyo wa Uvuvi ana-*suspend*, anamtoa, anasimamisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika shughuli za usimamizi wa uvuvi. Sasa mkanganyiko unakuja, na baada ya kum-*suspend* sasa ndio anamtaarifu Waziri wa TAMISEMI kwa hicho alichokifanya, baada ya kumpa hiyo taarifa...

MHE. RICHARD P. MBOGO: Taarifa

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: ...sasa ndio anamu-*advice the way forward* kwamba wa-*take over* hiyo mamlaka au watafute/wa-*nominate* mtu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa...

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa.

TAARIFA

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi, mchangiaji anayechangia dada yangu nampa taarifa kwamba tuna *further schedule of amendment* ambayo imetolewa na Serikali imeweza kubeba mapungufu tuliyoyaona awali. Kwa hyo, waisome kwanza ndio arudi kuchangia. (Makofi)

MWENYEKITI: Unasemaje na taarifa hiyo?

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashindwa ku-respond kwa sababu sijui hayo mapungufu anayosema na ninachangia kutokana na wakati Waziri husika ana-sum up alikuwa anasema bado wanaichukulia hii kama ilivyo. Sasa huwezi kuwa na Wizara mbili tofauti; TAMISEMI ndio anayeajiri, huyu ndio mwenye sera, yule mwenye sera anaenda ku-suspend another Wizara kufanya ile shughuli ambayo ile Wizara husika TAMISEMI anafanya, *how does it work?* (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa Wabunge muda wetu ndio huo, kwa mamlaka niliyonayo naongeza muda wa shughuli zetu muda usiozidi dakika 30 ili tuweze kumaliza shughuli zetu. Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ambayo Mheshimiwa Salome anaizungumzia hapa, hizi ni Wizara mbili zenye mamlaka tofauti na kila Wizara inafanya kazi yake, lakini kama vile haitoshi *Local Government* zina own source ambazo zinategemea na vyanzo kutokana na mazingira yaliopo. Kwa hiyo, waliopo kwenye bahari wengine wapo kwenye misitu hawaingiliwi na Wizara zingine. Kwa hiyo, hii itakuwa *constitutional crisis*, Waziri wa Wizara nyingine...

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Taarifa nampa Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

MWENYEKITI: Taarifa unampa Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, sio mimi. Taarifa.

TAARIFA

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Naomba nimpe taarifa mzungumzaji wa sasa hivi, ni kweli Serikali ime-take care of tunachoki-discuss, kwa hiyo hakuna haja ya kuendelea ku-discuss. Tunaipongeza Serikali kwa kulichukulia hatua. (Makofi)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado.

MWENYEKITI: Umeikubali taarifa yake?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nimeikubali lakini nina tatizo lingine. Katika...

MWENYEKITI: Aaah, Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni utaratibu tu, tunatunga sheria.

MWENYEKITI: Lakini...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Tatizo liko, hiyo taarifa nimeikubali.

MWENYEKITI: Sawa, lakini mimi ninakuuliza hivi, kile kifungu kidogo cha sheria hii tunayoongelea umekisoma?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

MWENYEKITI: Cha nne, nisomee kinasema nini.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sio hilo, ni kusaidia tu hiyo. Kwenye kutunga sheria, wameleta hii sheria ina *typing error*, hatuwezi kutunga sheria kuna *typing error* hapa, nataka irekebishwe.

MWENYEKITI: *Typing error* kwanza niambie.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Kwenye hii *schedule of amendments*.

MWENYEKITI: Ehee, ninayo mbele yangu.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Unayo hapo? Kwenye 21 pale chini inasema *subject to sub-section four, the Minister for Local Government Authorities shall*, pana comma, halafu *if*, hilo neno linalofuata ni neno gani?

MWENYEKITI: *If such...*

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tutunge kwa hivyo...

MWENYEKITI: Sasa haya ni ya kiuandishi, hawa wanajua.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa si ndiyo nilikuwa naleta hapa.

MWENYEKITI: Haya, naona hapa hakuna hoja.

Mheshimiwa Salome, unataka kuendelea kwa kitu ambacho so obvious?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko vizuri, nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa AG.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya rekodi sahihi iingie katika *Hansard* kwamba kifungu hiki kimerekebishwa kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho la Pili lililoletwa na Serikali.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)

Ibara ya 22

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)

Ibara ya 23

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni ndogo tu kwenye ibara hii na ninapendekeza ibara hii ifutwe kwa sababu; naomba niisome maana na hivi vidude hivi vinachanganya kidogo. Ibara ya 23 inayorekebisha ibara ya 47 inasema; *any person who contravenes the provision of this Act to which no specific penalty is prescribed commits an offence and shall, upon conviction, be liable-*

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(a) in the case of offences involving unlawful fishing or fish trading or facilitating unlawful fishing or fish trading, to a fine of not less than ten million shillings but not exceeding fifty million shillings; na

(b) in the case of offences other than offences under paragraph (a), to a fine of not less than two hundred thousand shillings but not exceeding ten million shillings, or imprisonment of a term not less than two years but not exceeding ten years.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kimeshakuwa *addressed* tayari, nimeomba kifutwe kwa sababu kiko kwenye sheria mama ambayo inaelezwa na maelezo aliyoytoa Mheshimiwa Waziri kama yangukuwa yameandikwa kwenye sheria hii ningeruhusu kiendeleo, lakini maelezo aliyoyasema hajaleta *schedule of amendments*, yamebaki ya kwake tu kama mchango na yaliyobaki hapa inaonekana tu watu watapigwa faini, hajaeleza kwamba hawa ni wahalifu wakubwa au wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ninachokitaka, Serikali ama ikifute ikakiandike upya au walete mabadiliko ambayo haiwezekani, muda umeshakwenda, wa-specify hawa wahalifu, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri, hayo ndiyo malengo yao basi walete *specifically* kwenye sheria, lakini kisibaki kama kilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiporidhika nitaomba Wajumbe wenzangu waniunge mkono.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Mheshimiwa *Attorney General*.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena nasema kama Mheshimiwa Salome Makamba angekuwa amesikiliza maelezo ya Mheshimiwa Waziri, pasingekuwa na hoja hapa.

Mheshimiwa Waziri alianza kueleza sheria ilivyo sasa inasema nini na ili tusiwe na ubishi naomba noisome, inasema; *any person who contravenes the provision of this Act other than those with specified penalties, upon conviction, shall be liable to a fine of not less than one hundred thousand shillings and not more than one million shillings, or to imprisonment for a term of not less than two years and not more than five years or to both such fine and imprisonment.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza vizuri, kwamba sheria kama ilivyo sasa hivi haitenganishi kuna wakosaji wakubwa na wakosaji wadogo. Sasa mabadiliko haya yanasemaje; *the Principle Act is amended by repelling Section 47 and replacing it with the following; any person who contravenes the provisions of this Act to which no specific penalty is prescribed commits an offence, and shall, upon conviction, be liable-*

(a) in the case of offences involving unlawful fishing or fish trading or facilitating unlawful fishing or fish trading to a fine of not less than ten million shillings but not exceeding fifty million shillings. Na hapa naweka emphasis kwa msimamo wa Wizara na maono haya ni makosa makubwa.

(b) in the case of offences other than offences under paragraph (a) yale niliyokwishayasoma sasa, to a fine of not less than two hundred thousand shillings but not exceeding ten million shillings, or to imprisonment for a term of not less than two years but not exceeding ten years.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani alichokisoma Mheshimiwa AG ndicho nilichokisoma mimi, na nikasema Waziri wakati anajieleza hata tukiangalia *Hansard*...

MWENYEKITI: Majibu ya AG ndiyo muswada ambao tunaangalia hapa, sio maelezo ya Mheshimiwa Ulega.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nasema maono ya Wizara au matamano sio sheria. *A law must be specific* na humu hawaja-specify kwamba hapa tunalenga mapapa, hapa tunalenga wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema tu...

MWENYEKITI: Toa hoja basi.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja Wabunge wenzangu waniunge mkono.

MWENYEKITI: Haijaungwa mkono. Tuendeleo.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 24

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 25

Ibara ya 26

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)

Ibara ya 27

Ibara ya 28

Ibara ya 29

Ibara ya 30

Ibara ya 31

Ibara ya 32

Ibara ya 33

Ibara ya 34

Ibara ya 35

Ibara ya 36

Ibara ya 37

Ibara ya 38

Ibara ya 39

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 40

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)

Ibara ya 41

Ibara ya 42

Ibara ya 43

Ibara ya 44

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 45

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ibara hii inahusu ile Sheria ya Mirathi na Serikali, sijui walikuwa wanafikiria nini, walileta mapendekezo kwamba Mtanzania ambaye amezaa mtoto ambaye ana uraia wa nchi nyingine, *say for example* mimi niolewe na mzungu mtoto wangu awe ni raia wa Uingereza hataruhusiwa kurithi ardhi, siwezi kumuandika kwenye mirathi...

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu Utaratibu; Kanuni ya ngapi?

KUHUSU UTARATIBU

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni 68(7).

MWENYEKITI: Haya, endelea Mheshimiwa AG.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *schedule of amendments* imekiondoa kifungu hicho, kwa hiyo hakuna kifungu anachokijadili Mheshimiwa Salome.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa *Attorney General*; Mheshimiwa Salome unafahamu kuwa *courteous* kwa kitu ambacho mwezako amekifanya kizuri unasema hivyo kwamba ndiyo wanasheria tumefunzwa hivyo.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru *Attorney General* na Serikali kwa kufikiria mara mbili kwa sababu kifungu hiki kilikuwa kinakwenda kukiuka Katiba kabisa, kwa hiyo namshukuru kwa kukitoa.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa na Serikali)

Ibara ya 46

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ibara ya 47
Ibara ya 48
Ibara ya 49

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)
Ibara ya 50

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji kwenye Ibara hii, tunatunga sheria; Mheshimiwa *Attorney General*, nawaomba sana kwenye ibara hii mnatumia neno *for the time being resident in Tanzania*, mimi nawaombeni sana *terminology* hii ya Tanzania, *in Tanzania* tuiache kwa sababu ukichukua sheria ya tafsiri za sheria, sheria inatoa tafsiri ya neno *United Republic*. Inatumia sura mbili; sura ya kwanza maana ya *United Republic* ambayo ni *United Republic of Tanzania*, lakini ukisema *United Republic* maana yake ni kipindi chote kuanzia tarehe 11 Desemba, 1964 mpaka leo. Halafu inakwambia ina maana pia kipindi cha kuanzia siku ya Muungano, tarehe 26 Aprili, 1964 mpaka tarehe 11 Desemba, 1964. Kwa hiyo ukiandika *in Tanzania* inaleta ukakasi na wengine wanaweza kukwambia kwamba mnafikiria kuna Serikali tatu hapa. Kwa hiyo naombeni hapa tuelewane kabisa, *resident in the United Republic*. Kama mna maana hiyo, kama unataka *u-restrict* kwa *Mainland* semeni hivyo. Sasa nakuachia wewe maana wewe ndiyo muswada wako huu, unasemaje?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, angalizo hilo limepokelewa vizuri, lakini kwa sababu ni suala la *rectification* litafanyiwa kazi kwa mujibu wa mamlaka aliycopewa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenye *law revision*. Ahsante.

MWENYEKITI: Haya, muendeleo, mimi kazi yangu ni kuwakumbusha.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 51
Ibara ya 52
Ibara ya 53

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)
Ibara ya 54

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)

Ibara ya 55
Ibara ya 56
Ibara ya 57
Ibara ya 58

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 59

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)

Ibara ya 60
Ibara ya 61

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ibara ya 62

Ibara ya 63

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 64

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)

NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya marekebisho kwa kupanga upya Ibara ya 46 hadi 64 kuwa 45 hadi 63.

MWENYEKITI: Yote hayo yanakubalika ni utaratibu.

NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa Hoja, taarifa.

TAARIFA

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 8) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.8) Bill, 2019*] ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.8) wa Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.8) Bill, 2019*] kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono karibu na Bunge zima, kwa hiyo nitawataka sasa muiamue wenyewe hoja hii.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

MWENYEKITI: Walioafiki wameshinda. Katibu.

NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali zipatazo kumi na nne kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza katika sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo (A Bill for an Act to amend certain written laws).

(Kusomwa Mara ya Tatu)

(Muswada wa Sheria wa Serikali Ulipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, napenda nitamke rasmi kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.8) wa Mwaka 2019 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.8) Bill, 2019*) sasa umepitishwa rasmi na Bunge hili na zinafuata hatua zingine za Kikatiba kukamilisha kazi nzuri mliyoifanya.

Mimi niwashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya kuanzia kwenye Kamati ya Katiba na Sheria kwa uchambuzi huu, maoni ya Kambi ya Upinzani lakini pia na michango yenu mliyoendelea kuboresha sheria hii, na upande wa Serikali kwa kuwa *very fast* katika ku-react na maeneo ambayo ni ya msingi sana. Tunatunga sheria za nchi kwa faida ya Watanzania wa makundi yote, kwa hiyo, mimi naishukuru sana Serikali kwa kuliona hilo, lakini pia na Waheshimiwa Wabunge kwa jitihada zenu za kuleta *schedule of amendments* na ndiyo hiyo; Mheshimiwa Salome umefurukuta eeh? *Very good*. Mimi kazi yangu na Mheshimiwa Spika ni kulea vijana muweze kufanya vizuri zaidi, mtaweza tu.

Kwa hiyo, mimi sina ya ziada, tumefanya vizuri, na sina matangazo hapa, niwatakie tu jioni njema.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kumbe nilikuwa nimeletewa tangazo naliona hapo; Mheshimiwa Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, asubuhi hakumbuki ni wapi lakini ni humu ndani, kama umeona saa ambayo unaamini sio ya kwako, naamini Mheshimiwa kama huyu, naomba tu mjue kwamba saa ile ni ya kwake, naombeni Waheshimiwa Wabunge, ni humu humu ndani... hapana sijasema hivyo mimi, ni humu humu ndani.

Baada ya kutoa tangazo hilo, hakuna cha mwongozo, baada ya tangazo hilo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho, siku ya Jumatano tarehe 29 Januari, 2020 saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.02 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 29 Januari, 2020 Saa Tatu Asubuhi)*